Ufafanuzi Wa Agano Jipya

Wakorintho 1 na 2

Na Dorothy Almond

mwisho na Askofu Francis Ntiruka

www.africanpastors.org

Ufafanuzi Wa
Agano Jipya

Wakorintho 1 na 2

Dorothy Almond

© African Pastors Fellowship 2010

Kimetolewa na:
AFRICAN PASTORS FELLOWSHIP
Station House, Station Approach, Adisham
Canterbury, Kent CT3 3JE
United Kingdom

www.africanpastors.org

WARAKA WA KWANZA
KWA WAKORINTHO

YALIYOMO

UTANGULIZI
(a) Mji wa Korintho
(b) Uhusiano wa Paulo na Wakorintho
(c) Tarehe ya kuandikwa kwa Waraka wa kwanza
(d) Sababu za Paulo kuwaandikia Wakorintho

UFAFANUZI
1:1-9 UTANGULIZI
1: 1-3 Salaam
4-9 Shukrani

1:10 – 4:21 FARAKANO KATIKA KANISA 1:
10-17 Habari na hali ya farakano
18-25 „Upuuzi" wa ujumbe wa Injili
2: 6-16 Injili ni ufunuo uliotoka kwa Mungu
3: 1-9 Wakristo hawakukua kiroho, hivyo hawakuelewa namna ya kuwawaza wahudumu
10-17 Msingi na jengo
3:18-4:13 Wahubiri ni watumishi wadogo
4: 14-21 Paulo kama baba wa imani yao anawasihi kibinafsi

5:– 6:20 ULEGEVU MKUBWA KATIKA KANISA
5: 1-8 Uzinifu na waumini hawakujali
9-13 Kuwaeleshwa maana ya barua iliyotangulia
6: 1-11 Kudhulumiana na kushtakiana mbele za wasioamini
12-20 Zinaa
7:1-40 NDOA
7: 1-7 Mambo ya kuoa/kuolewa na kutokuoa/kutokuolewa
8-9 Wasiooa/wasioolewa na wajane
10-11 Waliooa/walioolewa
12-16 Muumini aliyeoa/aliyeolewa na asiyeamini
17-24 Kuishi maisha kufuatana na jinsi mtu alivyo
25-38 Wanawake walio mabikira
39-40 Wajane

8:1 – 11:1 KANUNI YA KUUTUMIA UHURU KATIKA KRISTO
8: 1-6 Ujuzi wa sanamu 8:1-6
7-13 Ndugu dhaifu wa imani 8:7-13
9: 1-27 Kielelezo cha Paulo 9:1-27
10: 1-13 Kielelezo cha Waisraeli zamani 10:1-13

14-22 Hamna ushirikiano kati ya karama ya Kikristo na ya sanamu
10:23-11:1 Matokeo kiutendaji

11:2 – 14:40 IBADA ZA KIKRISTO NA WAO KUKOSA UTARATIBU
11: 2-16 Wanawake kuvaa taji
17-34 Chakula cha Bwana
12:1-14:40 Karama za Roho

15:1-58 UFUFUO WA MWILI
15: 1-11 Ufufuo wa Kristo
12-19 Matokeo ya kuukana ufufuo wa wafu
20-28 Matokeo ya ufufuo wa Kristo
29-34 Ushuhudu aina nyingine
35-49 Uwezekano wa mwili kufufuka ukioneyeshwa kwa mfano wa mbegu na mimea na kwa Maandiko
50-58 Kushindwa kwa mauti

16:1-24 MWISHO
16: 1-4 Changizo
5-9 Mipango ya Paulo
10-12 Timotheo na Apolo
13-14 Kuwasihi
15-18 Ombi lake wawajali watu kama Stefana na wenzake
19-24 Salaam za mwisho

U T A N G U L I Z I

(a) Mji Wa Korintho

Jiografia: Mahali pake palihakikishia mafanikio yake. Ulijengwa kwenye shingo la nchi, mahali pembamba, pakiwa na bahari upande wa magharibi na upande wa mashariki. Zilikuwepo bandari mbili, moja ya Lenkrea upande wa magharibi na ya pili Kenkrea upande wa mashariki. Bidhaa zilishushwa kwa moja na kupandishwa kwa ya pili, na meli ndogo zilivutwa kutoka moja hadi ya pili. Kwa njia hii muda mwingi wa kuizungukia pwani ndefu ya kusini uliokolewa, ilikuwa pwani ya hatari sana, yenye visiwa vidogo vidogo vingi na miamba mikubwa, na dhoruba kali zilitokea-tokea mara nyingi.

Wakati wa Kaisari Nero walijaribu kuujenga mfereji wa maji bila kufaulu, ila baadaye walifaulu. (Tazama ramani ili kupata picha ya mahali pake)

Utawala: Mji wa Korintho wa zamani ulichomwa moto KK 146 na baada ya kukaa hali ya magofu kwa miaka mia, Kaisari Julio aliujenga upya KK 46. ukapewa heshima ya kuwa koloni la Kirumi. Ndipo mwaka KK 27 umuhimu

wake uliongezwa na liwali wa Kirumi alipoweka kikao chake pale na makao makuu ya Jimbo la Akaya yaliletwa pale. Akaya lilipata kusimama peke yake kama Jimbo mbali na Jimbo la Makedonia, kaskazini yake.

Sifa: Mji wa Korintho wa zamani ulikuwa na sifa mbaya na huo mpya uliirithi sifa hiyo mbaya. Kama ilivyo katika miji mikubwa na miji ya pwani, mahali pa mikusanyiko mikubwa ya watu wa kila aina na mahali pa kupitia wengi, ubaya na uchafu ulizidi. Katika usemi wa siku zile watu walipotaka kuuelezea ubaya wa mtu walizoea kusema „kama Mkorintho" na katika viigizo kila mara mlevi au mwasherati alionekana kama ni mkorintho. Pia neno jipya liliundwa, „kukorinthianiza" maana yake "kuuzidishia ubaya"

Iwapo sifa yake kwa upande wa maisha ya watu haikuwa njema hata hivyo mji ulikuwa „hai" ki-uchumi. Wengi walivutwa kuja Korintho. Ufundi aina aina ulisitawi pale, na mji ulijaa watu.

Wataalamu hukisia idadi ya wakazi wake kwa tofauti. Baadhi wanafikiri walizidi laki 6, na baadhi husema ilikuwa kama laki moja tu. Ni vigumu kuihakikishia idadi hiyo. Warumi walikuja kuishi pale kwa sababu ya mji kuwa „koloni" lao. Wenyeji wa asili, Wayunani, walirudi kuishi sehemu zile walipoona usitawi wake. Wayahudi walikuwa wabingwa wa biashara, kwa hiyo walikuwapo wengi pale.

Dini: Wayahudi waliifuata dini yao, wakiwa na sinagogi lao na ibada zao, wakishuhudia kuwepo kwa Mungu mmoja tu, aliye hai, ambaye hakubaliani kwa vyo vyote watu wazichonge sanamu za aina yo yote. Walikuwa na maandiko yao ya Agano la Kale, na mkazo wa kuishi maisha ya kuzishika sheria za Torati yao. Warumi waliiabudu miungu mingi na kuijengea mahekalu na sanamu. Maisha si kitu mradi to wameituliza miungu yao kwa kuitolea sadaka. Warumi walikuwa hodari wa uongozi na mipango.

Wayunani pia walikuwa na miungu mbalimbali na kuijengea mahekalu. Moja kubwa kwa Afrodito, mungu wa kike, mungu wa pendo na kizazi, lilijengwa juu ya mwinuko wa mji, nalo lilivuta waabuduo wengi, yasemekana kwamba makuhani wa kike elfu moja waliwekwa kama makahaba „watakatifu" na upeo wa ibada ulikuwa katika kushirikiana nao kimwili. Wayunani walikuwa na tabia ya kupenda „filosofia", kisomo na ubingwa wa usemaji na kujiona kuwa wenye hekima.

Pamoja na watu hao makabila mengine kutoka mashariki walivutwa na „uhai" na mafanikio ya Korintho, na wasafiri wengi walipitia pale, wakikaa kwa muda na kuondoka tena.

Michezo: Kila baada ya miaka mitatu, karibu na mji wa Korintho, ilifanyika Michezo mikubwa ya Isithimia iliyowavuta wachezaji wabingwa wengi.

(b) Uhusiano wa Paulo na Wakorintho

Kwa kufika kwake: Tunajua Paulo alifika Korintho kwa mara ya kwanza katika Safari kubwa ya pili ya Injili. Habari hiyo yapatikana katika Matendo ya Mitume, sura ya 18. Alikaa na Priska na Akila, Wayahudi wenzake, walio washonaji mahema kama yeye. Alianza kazi ya kuihubiri Injili katika sinagogi la Wayahudi. Baada ya muda wakaja Sila na Timotheo waliokuwa wamebaki Makedonia ndipo Paulo alizidi kuwa hodari akikazana kabisa kuwashuhudia Wayahudi kwamba Yesu aliyesulibiwa ndiye Masihi wao wa kweli. Wengi walikwazwa na kumpinga kiasi cha kumfanya akate shauri la kuwaacha katika kutokuamini kwao, akawageukia wamataifa.

Aliitumia nyumba ya mwongofu mmoja Tito Tusto, ambaye nyumba yake ilikuwa jirani na sinagogi. Wengi waliamini, Mdo. 18:8, pamoja na Myahudi mashuhuri, Krispa, mkuu wa sinagogi. Paulo alizidi kupata nguvu na kutiwa moyo, hasa alipotokewa na Bwana Yesu aliyemwambia aendelee bila kuogopa, asinyamaze, kwa kuwa wengi wataokolewa na huduma yake.

Alipoingia liwali mpya, jina lake Galio, Wayahudi walichukua nafasi hiyo kwa kumshtaki Paulo mbele yake, lakini Galio hakujali, hakuhesabu mambo ya dini kuwa yanamhusu yeye, akawaondoa pale mahakamani; ndipo palepale wenyeji walionyesha chuki yao kwa Wayahudi, wakampiga mkuu wa sinagogi. Sosthene. Taz.Mdo.18:12-17. Hayo vote yalimsaidia Paulo, naye aliendelea kukaa siku nyingi Mdo.18:18. Kisha aliondoka pamoja na Priska na Akila, wakaenda Efeso, na hapo Paulo aliachana nao, akaenda mpaka Yerusalemu na kurudi Antiokia mahali alipoanzia safari ya pili.
Ndipo Apolo alikuja Efeso, akakutana na Priska na Akila nao walimchukua na kumwelimisha zaidi juu ya Yesu Kristo. Baadaye Apolo akaondoka Efeso kwenda Korintho ili awasaidie kwa kufundisha Wakristo na hasa walio Wayahudi, maana alifahamu sana Agano la Kale akawa mfafanuzi hodari wa Maandiko. Mdo.18:24-28. Ndiyo maana ya maneno ya Paulo katika 1 Kor.3;6 „mimi nalipanda na Apolo akatia maji".

Kwa barua: Paulo aliposikia habari ya kuwa wakristo wanashirikiana na wazinzi walio ndugu aliwaandikia - taz. 1 Kor.5:9-13 - hatuna barua hiyo. Wao walimwandikia kuhusu mambo fulani wakitoa mawazo yao na kutafuta mawazo yake - taz. 1 Kor.7:1. Huenda sura zilizofuata pia zilihusu mambo waliomwulizia, naye aliwajibu kwa kuwaandikia waraka huo wa kwanza.

Kwa kuonana na baadhi yao: Pia uhusiano ulijengwa kwa kuja kwake watu kama Stefana na wenzake 1 Kor.16:17 na watu wa nyumbani mwa Kloe - taz., 1 Kor.1:10. Kwa watu hao wote alipata picha ya jinsi mambo yanavyoendelea pale Korintho.

(c) Tarehe ya Kuandikwa kwa Waraka wa Kwanza

Tunao msaada mkubwa wa kujua tarehe hiyo. Lipo jiwe lenye maandishi yanayotuambia kwamba Galio alikuwa liwali wa Korintho mnamo BK51, na kwa kawaida uliwali ulikuwa kwa mwaka mmoja tu. Pamoja na hayo tunajua kwamba Paulo alikuwa Efeso alipouandika Waraka huo, akikaribia kuimaliza huduma yake pale hali ameisha kukaa muda mrefu. taz. 1 Kor.16:8 na Mdo 19:10
Kwa kulinganisha hayo yote tarehe yaweza kuwa kama BK.54 au BK.55
Waraka unao ushuhuda mwingi wa Paulo kuwa mwandishi

(d) Sababu za Paulo Kuwaandikia Wakorintho

Tumekwisha kuona ya kuwa Paulo alikuwa amewaandikia kuhusu ushirikiano wao na wazinzi, nao wamekosa kumwelewa vema. Kwa hiyo ilimbidi awaeleweshe zaidi juu ya maana yake.

Wao walikuwa wamemwandikia kuhusu mambo mbalimbali, wakitoa mawazo yao na kutaka maoni yake.

Watu wa mama mmoja aliyeitwa Kloe wamempasha habari ya farakano lililopo kati yao, kwa hiyo Paulo alitaka litengenezwe haraka iwezekanavyo.

Pia, watatu walimfikia kutoka Korintho, 1 Kor.16:17, nao wamempasha habari ya matatizo mbalimbali, hayo nayo yalihitaji mashauri yake.

U F A F A N U Z I

1:1-9 UTANGULIZI

1:1-3 <u>Salaam</u>

Katika kuuanzia waraka Paulo alifuata kawaida ya siku zile kwa kujitaja halafu kuwataja anaowaandikia na kuwasalimia.

Alijitaja kuwa mtume wa Kristo kwa mapenzi ya Mungu. Mapema sana katika waraka aliwakumbusha huduma yake na mamlaka ya ki-mitume aliyo nayo. Alitumwa kwao na Mungu Mwenyewe.

Pia Sosthene alitajwa katika salaam. Iwapo hatujui Sosthene ni yupi kwa vile wengi walikuwa na jina hilo, ni wazi alijulikana kwa wakristo wa Korintho, yawezekana alikuwa mmojawapo aliyeongoka na huduma ya Paulo alipokuwa pale. Wengine wamewaza kwamba alikuwa mkuu wa sinagogi aliyetajwa Mdo.18:17.

Katika salaam wakristo wameelezwa kuwa „kanisa la Mungu" maana yake ni watu ambao Mungu amewakusanya Kwake ili wawe mali yake na milki yake. Neno „kanisa" kwa Kiyunani ni „ekklesia" na tafsiri yake ni „kusanyiko".

Kusanyiko hilo liko Korintho, kwa hiyo, kiroho wamo katika Yesu Kristo na kimwili wako Korintho.

Tena wameelezwa kama „waliotakaswa katika Yesu Kristo", kwa hiyo wakristo ni watu waliooshwa dhambi zao katika damu ya Kristo.

Tena wameelezwa kama „walioitwa wawe watakatifu" kwa hiyo wakristo ni watu walioitwa kujitenga na dunia kwa kusudi la kufanya mapenzi ya Mungu.

Ni wakristo wote walio na wito huo, wote ni watakatifu, wala sio wito kwa wachache tu.

Tena wameelezwa kama „wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo" kwa hiyo wakristo ni watu wanaomwomba Bwana Yesu, wanamwita awasaidie. Kila mahali wapo watu wanaoliitia Jina hilo.

Aliwatakia heri zipi katika salaam zake? Heri mbili, neema na amani. Amani ni tunda la neema. Neema ni nini? ni kipawa cha kupokelewa na Mungu bila masharti, „bure", kwa sababu ya, na kwa njia ya upatanisho alioufanya Kristo msalabani.

1:4-9 <u>Shukrani</u>

Kama tutakavyoona baadaye hao wakristo walikuwa na matatizo mengi na shida zao zilimhuzunisha Paulo na kumpa uzito wa hali. Hata hivyo Paulo hakukosa kumshukuru Mungu kwa ajili yao na kuwaombea. Bila shaka alikumbuka jinsi alivyoujia huo mji mkubwa, mwenye sifa mbaya, uliojaa watu wengi wa kila aina na kutokana na mahubiri yake wengine walimgeukia Mungu aliye hai na kumpokea Yesu Kristo. Alifahamu ni Mungu aliyekuwa pamoja naye na kufanya kazi mioyoni mwao. Pia Mungu aliwamiminia vipawa vingi vya Roho, thibitisho la ukweli wa ujumbe aliowahubiri na wa yeye mhubiri wa ujumbe huo.

Katika shukrani zake ameendelea kuwaelezea wakristo. Wakristo ni watu „wanaongojea kufunuliwa kwa Bwana Yesu Kristo". Wanasubiri kurudi kwa Bwana wao ili atakaporudi wawe tayari kwenda Kwake.

Tena katika kif.9 wameelezwa kama „walioitwa katika ushirika wa Mwanawe" kwa hiyo wakristo ni watu walioitwa washirikiane na Mwana wa Mungu kama ndugu wa Baba mmoja. Kwa hiyo kuwa Mkristo hasa si kushika sheria kadha wala kufuata taratibu fulani bali ni jambo la ki-binafsi la kushirikiana na Yesu ki-binafsi.

Katika utangulizi huo tunayo mafundisho mapana sana juu ya Wakristo kuwa watu wa aina gani. Maelezo hayo yanahusu wakristo wote wa mahali pote na wakati wote.

Tunajifunza nini juu ya Paulo na kazi yake? Kwanza tunajifunza kwamba Paulo alilowesha mahubiri yake na kazi yake katika „maji ya maombi ya sikuzote!".

Tunajifunza kwamba matatizo yakitokea ni vema kuchukua hatua za kuyatengeneza mara, ama kwa barua, au kwa kwenda, au kwa kumtuma mwingine anayefaa. Si vema kuyaachia na kubaki kulaamu watu.

Zaidi tunaona tumaini la Paulo na tegemeo lake ni katika uaminifu wa Mungu kif.9. Alikuwa na uhakika kwamba Mungu akilianzisha neno jema hawezi kuliachia hewani.

1:10 - 4:21 FARAKANO KATIKA KANISA
Inaonekana Paulo aliliwaza farakano katika Kanisa la Korintho kuwa neno zito. Alilizungumzia kabla ya matatizo mengine. Pia alilizungumzia kwa kirefu sana kuanzia sura ya kwanza mpaka sura ya nne, hali akichimba chini sana na kuyafafanua mambo makubwa ya ujumbe wa Injili na wahudumu wake.

1:10-17 <u>Habari na hali ya farakano</u>
Paulo alipashwa habari yake na watu wa nyumbani mwa mama mmoja Kloe wakati alipokuwa Efeso. Farakano halikuhusu mafundisho ya kikristo bali wahudumu,ila si wahudumu wenyewe waliogombana bali wakristo, waliogombana juu ya wahudumu.

Wengine walisema „sisi ni wa Paulo" na ni rahisi kuona sababu yao, maana ni Paulo aliyewaletea Injili kwa mara ya kwanza akizivumilia taabu nyingi. Wengine walidai kuwa „wa Apolo". Apolo alimfuata Paulo, alikuwa na utaalamu mwingi katika Maandiko ya Agano la Kale na mbingwa katika kufundisha. Wengi walijengwa katika imani yao, wala si ajabu walimpenda. Halafu baadhi walidai kuwa „wa Kefa" yaani Petro. Hatuna habari ya Petro kuwa Korintho. Haidhuru kama walikuwa wamemwona au siyo watu walifahamu ni yeye aliyeitwa na Bwana Yesu Mwenyewe alipokuwa duniani, alikuwa shahidi wa kuyaona mengi kwa macho yake. Huenda ni Wayahudi waliokuwemo katika kundi hilo, ila tusisahau Paulo mwenyewe alikuwa Myahudi halisi - Fil. 3:3-6. Kisha wengine walisema „sisi ni wa Kristo". Walijiondoa katika shida za wenzao, hata hivyo, wamejiunga pamoja kuwa kundi.

Paulo alihesabu wote kuwa wakosaji. Hakuwahurumia wale waliosema „sisi ni wa Paulo" iwapo bila shaka alijaribiwa kujiona na kutokuwakemea. Kosa la wote ni katika kugombana na kufarakana.

Paulo aliutoboa ubovu wa farakano lao kwa kuwaulizia maswali matatu makali. Kwa kweli wahudumu wamewaletea Injili na kuwajenga kwa mafundisho, hata hivyo chanzo kabisa ni Yesu Kristo aliyekufa msalabani na kuwakomboa. Bila Kristo na kazi yake wahudumu wasingalikuwa na habari njema ya kuwaletea na mafundisho ya imani ya kuwajenga. Walipobatizwa walitiwa katika ufuasi wa

Yesu Kristo kwa kubatizwa katika Jina lake, waliahidi kumfuata Kristo si mtu. Kwa hiyo aliyewabatiza asikuzwe.

Haiwezekani kumgawa Kristo vipande vipande na kumshika kwa sehemu tu.

Tunajifunza nini kuhusu hekima ya Paulo ki-kazi?

Tunajifunza kwamba alitambua tabia yao ya ugomvi na fitina, hivyo alifanya tahadhari ya kuwaachia wengine kazi ya kubatiza. Ling. na Yn 4:2 na Petro kwa Kornelio. Mdo.10:47-48.

1:18-2:5 ‘<u>Upuuzi’ wa ujumbe wa Injili</u>

Wayunani walithamini sana ufasaha wa maneno na ubingwa wa utungaji wa hotuba na kukuza elima, filosofia, na kisomo. Wayahudi walithamini nguvu ya Mungu iliyoonekana katika historia yao, hasa alipowatoa Misri kwa mapigo makuu, tena pale Sinai, Torati ilipotolewa kwa ngurumo na umeme na tetemeko la nchi. Lakini Habari Njema ni habari ya mtu aliyeitwa Yesu Kristo ambaye kimwili hakuwa na sifa za „kisomo", alionekana kama maskini, aliishi bila anasa, alifanya kazi ya mikono ndipo baadaye alitembea hapa na pale bila starehe. Aliwindwa na wakuu wa dini, alishtumiwa na kushtakiwa mengi, ndipo mwishowe alihukumiwa kuwa mhalifu wa hali ya juu, aliuawa kwa kusulibiwa, kifo kikali sana kupita vifo vyote, chenye maumivu makali sana na aibu nyingi, na kwa Wayahudi ni kifo chenye laana ya Mungu ndani yake.

Kwa upande mwingine wengi walimpenda na kumfuata, alikuwa na sifa nyingi kuwa mponyaji mkuu na mwalimu mstadi, mfanya miujiza n.k. Lakini habari njema inahusu hasa kifo chake na kufufuka kwake.

Inaonekana ni upuuzi mkubwa kudai kwamba kwa kifo hicho kibaya wanadamu waweza kuokolewa katika dhambi, na kwa kumuumini Kristo na kazi aliyoifanya msalabani mtu husamehewa dhambi zake na kufanywa kuwa kiumbe kipya. Ajabu ni kwamba ndivyo ilivyo kwa sababu ni mapenzi ya Mungu kuwa hivyo, Yeye huandamana na ujumbe huo na nguvu zake zatenda kazi kubwa kwa yule anayeiamini Habari hiyo - taz. 2:18 - Injili NI nguvu ya Mungu.

Kwa hiyo hekima ya watu imewekwa nje na Mungu, uwezo wa aina yo yote umewekwa nje na Mungu, ni neno la msalaba tu lifanyalo kazi ya kuokoa. Kwa nini? kwa sababu Mungu katika hekima yake amekusudia iwe hivyo, ili wote wawe na nafasi sawa ya kuliitikia kwa imani, na kwa sababu ni kwa kuamini hatuleti cho chote kingine isipokuwa dhambi zetu, kusudi nafasi zote za kujisifu zizibwe.

Twapata hekima na haki na utakatifu na ukombozi katika kumpokea Kristo, hekima ni ile ya Mungu si ya dunia hii na haki ni haki ya Kristo si haki yetu.

Katika kugombana wao kwa wao juu ya Paulo na Apolo na wengine, wamekwenda kinyume cha Injili waliyoipokea. Yote waliyo nayo kiroho yamepatikana katika Kristo. Paulo alipowafikia kwa mara ya kwanza alikuwa mwangalifu sana hali akijua tabia yao. Hakujionyesha kuwa mjuzi wa mambo, hakuja kama mtu ajuaye mengi, bali alijibana aihubiri Habari Njema na hasa mkazo juu ya msalaba wa Kristo. Pia alijihadhari na lugha aliyoitumia 2:1-2. Tena kwa hali ya kimwili hakujionyesha kuwa hodari k.3. Alimtegemea Roho wa Mungu kuuthibitisha ujumbe wake.

Tunajifunza nini na hali ya Paulo alipowafikia Wakorintho? Hasa tunajifunza kuwa wanyenyekevu kwa sababu ni Mungu afanyaye kazi mioyoni mwa watu, na Yeye hupinga wenye kiburi. Twapaswa kumtegemea Mungu wala si elimu wala uwezo wetu. Kama tumejaliwa kuendelezwa kwa masomo, tumshukuru Mungu, na kuzidi kumtegemea. Tukumbuke kwamba Paulo alikuwa msomi sana, lakini hakuacha kumtegemea Mungu.

2:6-16 <u>Injili ni ufunuo uliotoka kwa Mungu</u>

Bila shaka tunafahamu kwamba hekima ya Mungu inazidi hekima ya wanadamu. Lakini tunahitaji kutambua ya kuwa katika mpango wa wokovu Mungu ameiweka nje hekima ya wanadamu. Injili ni siri iliyofichwa, ambayo hufunuliwa kwa njia ya kumuumini Kristo. Mkristo anafunuliwa na Roho Mtakatifu, si jambo la akili zake au uwezo wake bali ni la imani . Ni Roho peke yake aliye na uwezo wa kumfunua Mungu, kwa sababu Yeye ni Mungu naye yu ndani ya Mungu, kwa hiyo anamfahamu Mungu kikamilifu 2:10-12. Hakuna mtu awezaye kupenya ndani ya Mungu na „kumgundua". Roho anasoma nia na sababu za mtu, na kumfunulia aliye wa kweli. Kwa njia hiyo mambo ya Mungu hulindwa; ni kondoo zake, wale wa kweli, watakaoisikia sauti yake, na kuitambua, na kumfuata.

Mungu ametupenda upeo kwa kutujalia kumfahamu na kushirikiana naye, ni baraka ya ajabu sana.

Wakristo waliofarakana juu ya wahudumu walikuwa wamesahau kwamba ni Roho wa Mungu aliyewafunulia siri ya Injili walipomuumini Kristo kutokana na imani yao, Iwapo Paulo aliwahubiri na Apolo aliwafundisha, pasipo Roho wasingalielewa na kuitika.

MASWALI

Je! Mhubiri apaswa kuwaza nini na kuandaa mahubiri yake kwa kuangalia mambo yapi kwa kulingana na watu anaowahubiri? Mhubiri ana majaribu gani? Awe na tahadhari gani? Wanaohubiriwa wana majaribu gani? Wawe na tahadhari gani?

3:1-9 Wakristo hawakukua kiroho hivyo hawakuelewa namna ya kuwawaza wahudumu

Tukumbuke kwamba hayo yote Paulo anayoyazungumzia ni katika mazingira ya farakano lao. Ameishasema juu ya ujumbe wa Injili, sasa anaingia eneo lingine kuhusu wahudumu wake. Mkristo mpya ni „mtoto mchanga" ki-imani, ana mengi ya kujifunza, anahitaji maziwa, baadaye chakula, ili akue katika imani, kisha awe mtu mzima ki-imani. Wala si kosa kuwa „mchanga"mwanzoni. Shida ya wakristo wengi wa Korintho, wao wangali wachanga, na kumbe muda umepita tangu walipoamini Iliwapasa wawe wamekua kiroho - k.2 „hata sasa". Ni kitu gani kilichoonyesha uchanga wao? ni tabia ya wivu, fitina, ugomvi n.k. Walijadili ubora wa mhudumu fulani, au kipawa fulani, na kufanya ulinganifu usio na faida, kinyume cha Injili, hayo si dalili ya kuongozwa na Roho na neema ya Injili.

Katika kif.5 Paulo aliuliza swali „Paulo ni nini?" „Apolo ni nini?" (neno la Kiyunani ni „nini" si „nani"). Ndipo Paulo alijibu kwa kusema „ni watumishi" akilichagua neno la Kiyunani lililotumika kwa wale walioleta chakula mezani! Hakuwa na maana kwamba hawakufaa, ila alitaka kukaza kwamba umaana wao hutokana na uhusiano wao na Bwana wao. Bwana wa mavuno. Kila mmoja aliwekwa na Mungu na kutumwa na Mungu, na kupewa vipawa kwa kazi aliyoitiwa na Mungu.

Paulo aliutumia mfano wa ukulima ili waelewe vizuri. Yupo apandaye mbegu, kama Paulo alivyofanya kwao alipowahubiri Injili. Baadaye hufuata atiaye maji, kama Apolo alivyofanya alipowafundisha. Kila mmoja huhitaji mwenzake na kazi yake, kwa hiyo si hekima kumkuza mmoja kinyume cha mwenzake, wote huhitajika.

Zaidi kuna akuzaye na pasipo huyo apandaye na atiaye maji hufanya kazi bure. Akuzaye ni Mungu si wanadamu. Ni Mungu atakayewahukumu wao na kazi zao, si hao Wakorintho, na Mungu huiangalia taabu ya hiyo kazi si mafanikio ya nje.

Katika k.9 Mungu ametajwa mara tatu, kwa kweli watumishi wanayo heshima kubwa ya kufanya kazi pamoja na Mungu, hata hivyo, wasikuzwe kupita kiasi, wauminio ni shamba la Mungu na jengo la Mungu.

3:10-17 Msingi na Jengo

Paulo aliendelea na hoja yake juu ya wahudumu kwa kuutumia mfano wa ujenzi, hapo nyuma ameutumia mfano wa ukulima. Katika ujenzi jambo kuu la kwanza ni msingi. Paulo alijiita „mkuu wa wajenzi" kwa vile alivyolianzisha kanisa pale Korintho, alipouweka msingi wa Kristo kwa kuihubiri Injili na kuvuta watu wamwamini Kristo. Hasemi kwa kiburi, tazama, alitanguliza maneno „kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa". Baada ya msingi kuwekwa ndipo jengo

lajengwa juu yake. Ziko tofauti nyingi za ujenzi kutokana na vifaa vinavyotumiwa na wajenzi wenyewe na hali zao. Paulo alimwonya kila mjenzi awe mwangalifu sana na jinsi ajengavyo, anao wajibu mkubwa.

Ipo siku ya kuipima kazi ya kila mtu na kuona kama itadumu hadi uzima wa milele. Kwa kweli si zote zitakazostahimili hiyo hukumu, nyingine zitadumu na nyingine zitatoweka kama vitu fulani vifanyavyo vinapopimwa na moto. Kitu kikubwa si kiasi cha kazi bali hali yake ni „ya namna gani". Neno linalozungumziwa hapa si wokovu wa mtu binafsi bali utumishi wake, na hasara ni kuikosa thawabu si wokovu, maana wokovu ni kipawa cha neema, thawabu ni ujira wa utumishi.

Ndipo lafuata neno zito sana katika v:16-18. Alifundisha kwamba waumini wote kwa pamoja ni jengo la Mungu, hekalu lake. Mungu akiishi kati yao. Kuleta farakano katika jamii ya wauminio ni dhambi kubwa ya kuliharibu hilo jengo. Wenye kulisababisha watahukumiwa vikali „Mungu atamharibu mtu huyo". Inaonekana kwamba ataukosa wokovu.

3:18-4:13 <u>Wahubiri ni watumishi wadogo</u>

Paulo aliona asili ya shida ni katika wao kujiona kuwa wenye hekima. Lakini hekima yao ilikuwa ya dunia hii ambayo ni upuuzi mbele za Mungu, na kwa kuitumia farakano limetokea. Mtu akitaka hekima ya Mungu ataonekana kama mpumbavu mbele za watu kwa kuwa atajinyenyekea, hatajionyesha, hatajisukuma mbele, hatapenda majadiliano n.k. Wasiwakweze watumishi kadha, na wasiwabague. Yawapasa kuwaheshimu wote na kuwahesabu wote kuwa wao ndipo watapata faida kubwa ya kushirikishwa vipawa vya wote na kutajirika sana kiroho. Baraka zitazidi, na Kristo atakuwa kati yao, na wakiwa na Kristo watakuwa na Mungu pia. Kufarakana ni hasara kubwa.

Basi, wawazaje wahudumu? Taz. 4:1-2 kwa jibu lake. Wawahesabu kuwa „watumishi wa Kristo". Paulo alilichagua neno kwa uangalifu sana ili wafahamu maana yake halisi aliposema ni „watumishi" Alilichagua neno kwa „wavuta makasia wa safu ya chini katika mashua". Ilikuwa kazi ngumu kuvuta makasia na hasa kwa wa safu ya chini- kwa hiyo ni watumishi wafanyao kazi ngumu isiyo na sifa.

Pamoja na kuwa watumishi wao ni „mawakili wa siri za Mungu". Zamani wakili alikuwa mtu aliyekabidhiwa mali ya bwana mkubwa, aliweza kupewa uangalizi mkubwa wa mashamba, nyumba, watumishi, vyakula, n.k. Alikuwa na madaraka juu ya mali aliyoyakabidhiwa. Hata hivyo alikuwa chini ya bwana wake na mali yote ilikuwa ya bwana wake. Kwa hiyo kwa upande mmoja alikuwa na madaraka makubwa na kwa upande wa pili ni mtumwa, chini ya bwana wake. Ilimpasa awa muuminifu na mtu wa kutegemewa, na mambo yake yawe wazi „aonekane kuwa muuminifu".

Kwa hiyo wahudumu kama Paulo na Apolo walimtumikia Kristo wakiwa tayari kufanya kazi ngumu kwa ajili yake. Tena walikuwa mawakili wa siri za Mungu, yaani Injili na ufunuo wa mapenzi ya Mungu. Mali hiyo ni ya thamani sana, kwayo mtu hufunguliwa ufalme wa Mungu, ni „hazina iliyositirika" na "lulu nzuri" Mt 13:44-45.

Paulo hakujali jinsi watu walivyomwona, Bwana wake Yesu Kristo ndiye aliyemweka katika utumishi, naye yu radhi kuisubiri hukumu yake. Alifahamu ni vigumu mtu ajipime vema, maana aweza kuwa kipofu kwa makosa na udhaifu wake, tena aweza kuyapima mengine kwa uzito kuliko mengine. Vilevile wengine hawajui sababu na nia za mtu ili wampime kwa usawa. Ni vema kungoja hadi Bwana Yesu atakaporudi ndipo ataifanya hukumu iliyo haki na ya kudumu, na sifa atakayoipata mtu itakuwa ya kweli na ya thamani.

Paulo na Apolo walijitahidi kuwa vielelezo vyema kwa Wakorintho. Waliishi kwa kanuni ya kuyafuata Maandiko na kwa lengo la kumtukuza Mungu na kufanya yampendezayo. Kati ya Paulo na Apolo hamna shida.

Hata ikiwa hawatamshusha mmoja kwa kusudi, kwa kumkuza mmoja kwa vyo vyote mwingine atakuwa ameshushwa.

Paulo aliliuliza swali gumu - 4:7 „una nini usichokipokea?" Vipawa vyote vyatolewa na Mungu, tena kwa bure, kwa neema, na kwa lengo moja la kumtukuza Yeye na kufanya kazi yake, kwa hiyo budi vitumiwe kwa shabaha hiyo si kwa kukuza watu. Ni vipawa, na kama ni vipawa, yuko Mpaji aliyevitoa. Haviwi malipo au ujira kwa mema au utauwa wetu.

Paulo alitoa picha ya magumu mengi yeye na wenzake waliyoyavumilia, kutokana na mzigo wao juu ya makanisa. Hakunungunika, ila alitaka kuonyesha tofauti kubwa kati yake na wakristo wa Korintho, walioishi maisha ya raha, hawakujali mwenendo wao, hawakuwa na mzigo juu ya ushuhuda wao mbele za wapagani, walizitumia nafasi zao kwa majadiliano na mafarakano, wakitafuta „ukubwa" na „ubwana" Wakati huo huo walipokuwa na raha hiyo Paulo na wenzake wamekosa chakula na nguo na mahali pa kukaa.

4:14-21 <u>Paulo kama baba wa imani yao anawasihi kibinafsi</u>

Paulo alikuwa baba wa imani yao, na kuwaona watoto wake kama walivyo kulimhuzunisha sana. Atawasaidiaje? Aliwasihi waige tabia yake na mwenendo wake. Alikuwa akimtuma Timotheo ili awakumbushe njia zake na aliahidi kwamba atakuja mwenyewe mara apatapo nafasi. Ila wako waliotaka kumtisha wakisema haji, anawaogopa. Yeye aliona ni rahisi wao kuwa wajasiri wa maneno maadamu yeye yu mbali nao. akija Je? Atakapokuja na awe mpole au mkali?

Hapo amemalizia kulizungumzia farakano, ataanza kuyazungumzia matatizo mengine waliyo nayo, hayo pia siyo madogo bali makubwa.

MASWALI

Kama Paulo asingalikuwa macho Kanisa la Korintho lingalizidi kufarakana ndipo kutawanyika. Alikuwa na kundi lake na bila shaka haikuwa rahisi awakemee lakini aliwakemea sawa na wengine.

Mara nyingi katika makanisa yetu viko vikundi vikundi, kuna wa fulani na fulani, na mambo ya chini chini. Je mtumishi wa Mungu na awe na tabia gani na afanye nini kwa hayo?

HASA twatia uzito gani ONYO KALI LA 3:16-18?

5:- 6:20 ULEGEVU MKUBWA KATIKA KANISA

Hao wakristo walitoka katika maisha mabaya, walikuwa wamezoea uasherati na wizi, ulevi na ugomvi - taz. 6:9-11 nao walipoongoka waliishi kati ya watu ambao kawaidi ya maisha yao ilikuwa kufanya dhambi hizo. Si ajabu ilichukua muda kupata ushindi. Hata hivyo Paulo alijua katika Injili ushindi upo, hataki waridhiane na dhambi kati yao.

5:1-8 <u>Uzinifu na waumini hawakujali</u>

Kama tulivyokwisha kuona, wakristo wa Korintho walitoka katika jamii ya watu waliokuwa wameizoea zinaa na kuihesabu ni hali ya kawaida tu. Hata katika dini nyingine ibada zilitoa nafasi kwa tendo kilo la kimwili. Tangu mwanzo na kila mahali Paulo alifundisha kwamba zinaa ni kinyume kabisa cha imani yetu. Wakristo wa Korintho walikuwa na hali ya kutokubali kufuata kanuni za kuishi kama wakristo wengine, walisema Kristo amewaweka huru, hawana haja ya kufungwa na mengine. Hali hii inaonekana kila mara katika waraka huo. Pale Korintho mmoja wao amezini na mke wa babaye, jambo ambalo hata wapagani hawakulifanya. Si hivyo tu, wakristo wenzake hawakumkemea wala kufanya lo lote, licha ya kufanya ilivyowapasa, hata walikuwa walijivunia, hawakulisikitikia, wala kumwita wala kumwonya, nao wako karibu naye. Ilibaki kwa Paulo, aliye mbali, achukue hatua kwa kuwaongoza la kufanya. Kwanza, wakutane katika mkutano wenye hali ya uzito: na pili katika mkutano huo waamue kumtenga, ili asiendelee kushirikiana nao katika ibada na mikutano yao. Aishi kati ya dunia iliyo chini ya uongozi wa Shetani. Atapata hasara ya kukosa baraka zipatikanazo katika jamii ya waumini. Tena atasikia shida anapoishi kati ya wasioamini. Yaonekana Paulo anawaza kwamba huenda ataugua kimwili. Lakini hayo yote ni kwa faida ya roho yake, yatazamiwa atajifunza, atalitambua kosa lake, atajirudi ili asipotee moja kwa moja. Kumrudi kulilenga uponyaji wake si kumpoteza.

Pamoja na hayo waumini watasaidiwa ili wasifuate kielelezo chake ili dhambi isienee kati yao. Ling. na Mdo.5:1-13 na kuona jinsi adhabu iliyowapata Anania na Safira ilivyowaleta waumini wengi kumcha Mungu. Tukumbuke Kanisa bado li changa, na bado Injili haijawafikia wengi mahali pengi. Ni kama mmea dhaifu uliopo mahali pachache tu.

5:9-13 <u>Kuwaelewesha maana ya barua iliyotangulia</u>

Hatunayo hiyo barua iliyotumwa na Paulo kuhusu ushirikiano wao na wazinzi. Waliielewa isivyo, walifikiri amewashauri wasishirikiane hata kidogo na watu wa namna hiyo. Lakini haikuwa na maana hiyo, haitawezekana wajitenge kabisa na watu, kwa sababu katika shughuli za kawaida ya maisha ya kila siku itawabidi washirikiane na watu wa hali zote. Hasa Paulo alitaka kuwaambia kwamba budi wasishirikiane na mzinzi aliye muumini, kwa sababu wakishirikiana na ndugu wa namna hiyo itaonekana kwamba wameunga mkono dhambi yake ndipo watu watachanganyikana wasielewe msimamo wa Kanisa. Kanisa lina wajibu wa kuwatunza watu wake na kuwarudi kwa sababu kwa hiari waumini wameamua kumfuata Kristo, hivyo, hawana budi kuishi kwa kuulingana na ukiri wao. Mkristo hana uhuru wa kuamua mambo yake bila kuwajali wenzake.

Kabla ya kumaliza jambo hilo Paulo alirudia mkazo wake kwa yule mzinzi, lazima aondolewe miongoni mwao k.13

MASWALI

1. *Je! Waonaje? Ni vema Kanisa liwe na marudi kama ya kuwatenga wanaozini n.k.? Je! Tunafanya kwa usawa na bila upendeleo wa watu, na bila kuwa na tofauti kati ya mwanamke na mwanaume? Hayo marudi yawe ya kutengwa tu? Je muda awekwe? Au yawe mpaka toba?*
2. *Pia, tufanye kwa dhambi hiyo tu?*

6:1-11 <u>Kudhulumiana na kushtakiana mbele za wasioamini</u>

Baadhi ya wakristo waliiba na kudhulumu, hata kwa wakristo wenzao. Ndipo walishtakiana mbele ya wasioamini na kwa wale wasio na sifa njema. Hawakuleta mambo hayo mbele ya kanisa au kuutafuta msaada kwa wakristo wenzao. Paulo kwa upande wake aliona ya kuwa afadhali wasimshtaki Mkristo mwenzao, wala kwa kanisa, wala kwa wasioamini, wawe tayari kudhulumiwa na kuachilia. Lakini kama mtu atasukumwa kupata haki basi aipeleke kesi yake kwa kanisa. Paulo alifundisha kwamba wakristo wanapaswa kukata kesi hizo na kuamua mambo kama kayo. Kwa nini washindwe? Je! kati yao hamna watu wa kufaa wenye uwezo kufanya uamuzi? Ndipo Paulo alisema neno la ajabu - ni wakristo ambao watawahukumu malaika !!! na kama ni kweli watafanya hivyo, itakuwa ajabu wasiwe tayari kuamua mambo kati yao.

Kisha Paulo alitoa maonyo makali juu ya maisha yao. Mkristo akiendelea katika dhambi bila kujihoji na bila kujali, hataurithi ufalme wa Mungu. Kwa kweli walitoka katika mabaya mengi lakini baada ya kumuumini Kristo lazima mabadiliko yatokee. Linganisha na Mathayo 18:15-17, 21-22

6:12-20 <u>Zinaa</u>

Tangu zamani hadi leo tamaa za mwili zimewasumbua wanadamu. Katika utangulizi tuliona watu wengi walishindwa na mwili, na hata katika dini mbalimbali nafasi ziliwekwa kuzitimiza tamaa zake. Ni wachache tu walioona njia ni kujitenga kabisa na kuwa kama watawa. Inaonekana wakristo walijaribu kuhalalisha matendo yao kwa kuunga mkono usemi wa wengi waliosema kwamba „kama tumbo ni kwa chakula na chakula kwa tumbo", vivyo hivyo viungo vingine ni kwa zinaa. Mtu asikiapo hamu ya kula hula, kwa hiyo mtu asikiapo hamu ya zinaa basi aitimize tu. Pia walisema mwili ni wa muda tu, kwa hiyo mtu afanye ajisikiavyo, ni roho idumuyo, kwa hiyo roho ndiyo ya maana si mwili ulio wa muda.

Paulo aliyakanusha kwa nguvu mawazo hayo. Alisema kwamba mwili ni kwa Bwana Yesu, ni mali yake, upo kwa ajili yake na shabaha ni mtu amtukuze Mungu katika mwili. Tena mwili ni nyumba au hekalu la Roho Mtakatifu, Roho hakai katika roho zetu tu bali pia hukaa katika miili yetu. Na Yesu alitununua msalabani, mwili, nafsi na roho, na gharama aliyoitoa ni damu yake, akiutoa mwili wake kusulibiwa.

Alilikanusha wazo la kusema mwili ni wa muda tu, kwa sababu ni mwili utakaofufuliwa, nao utabadilika kuwa „mwili wa roho", ni huo huo tulio nao sasa ambao utavikwa uwezo mpya.

Hakukubaliana kwamba „hamu" ya zinaa ni sawa na hamu ya kula. Mpango wa mtu kula ni tofauti na mpango wa mtu kushirikiana kimwili na mwingine. Mpango huo ni katika mtu mmoja kufunga ndoa na mwenzake na kukaa kama „mwili mmoja" daima. Pia „zinaa" hugusa zaidi ya mwili wa mtu, hugusa hata nafsi yake. Mwili ni dhamiri, nafsi, utu, si nyama tu, na katika kuzini twajikosesha utu wetu na kujiharibu. Tulipoamini tuliungamanishwa na Kristo, na mwili umeungana naye. Mwili una nguvu, una hali ya kujiinua na kutaka kuwa bwana, unayo madai makali. Tunahitaji Bwana aliye hodari awezaye kuuongoza na kuutawala ili tusitumikishwe na mwili, na huyo Bwana ni Yesu Kristo. Tusipoutumikisha mwili, mwili utatutumikisha sisi, ndiyo sababu Paulo anafundisha kwamba Kristo ndiye Bwana afaaye mwili.

Paulo anashauri „kimbieni zinaa" kama adui wa hatari sana.

MASWALI

Je! Ni vema Wakristo kamwe wasiende mahakamani au kuna makubwa ambayo yafaa yapelekwe mahakamani? Tena makubwa yapi? Wakristo kwa Wakristo Je! wayaachilie wakati wote? Waonaje?

Je! Waonaje kwamba wakristo wengi hushindwa kuishi maisha safi kwa sababu mkazo katika mahubiri ni juu ya roho zetu kuokolewa na mafundisho ni haba juu ya umaana na thamani ya miili yetu? Tufanyaje?

7:1-40 NDOA

Jambo la ndoa ya Kikristo lilikuwa jipya katika ulimwengu wa siku zile. Bila shaka kila watu walikuwa na mila zao. Ibada ya ndoa ya Kikristo ilikuwa bado haijaandikwa. Jambo kubwa lilikuwa la mume kuwa na mke mmoja maisha yote, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi. Pamoja na hayo maisha ya mke katika ndoa yalipata nafuu kutokana na tabia za Kikristo na usawa wa mume na mke katika neema ya Injili na nafasi walizozipata wanawake katika Kanisa kupita wenzao wengi walio nje ya Kanisa. Hata hivyo wakristo wa Korintho walikuwa na maulizo mengi ya kumwuliza Paulo katika barua yao - k.1.

7:1-7 <u>Mambo ya kuoa/kuolewa na kutokuoa/kutokuolewa</u>

Alianza kwa kukaza ndoa ya mume mmoja na mke mmoja kwa wale waliosikia haja ya kuoa/kuolewa. Kuoa au kutokuoa ni karama ya Mungu k.7. Si wote walioitwa kwa maisha ya ndoa, hali kadhalika si wote walioitwa kwa kutokuoa/kutokuolewa. Kwa hiyo tusifikiri ni kutokuoa tu ambako kwahitaji wito na karama ya Mungu, hali zote mbili ni wito na karama ya Mungu.

Kwa wale waliooa na kuolewa alifundisha kwamba kila mmoja ana haki iliyo sawa kuhusu mwili wake na mwili wa mwenzake k.3 na k.4. Kila mmoja apatane na mwenzake katika kutimiza ndoa kimwili, pia wasinyimane isipokuwa wamepatana, kusudi, mmoja asimwingize mwenzake katika majaribu. Pia shabaha iwe ya kujenga maisha ya kiroho, kama ni kuhusu shughuli za kawaida hiyo siyo shabaha ya kutosha

7:8-9 <u>Wasiooa/wasioolewa na wajane</u>

Inaonekana kwa maneno yake katika k.8 Paulo mwenyewe alikuwa hakuoa, ila hatuna hakika. Alitawaliwa na wito wa kuihubiri Injili ambao utaleta shida kwa mtu aliye na familia. Akiwa na mke uhuru wake wa kwenda hapa na pale na kwenda mbali utapunguzwa. Ila alisema wazi ni afadhali kuoa kuliko kuwaka tamaa na kuanguka dhambini.

7:10-11 <u>Waliooa/walioolewa</u>

Hapo Paulo hakutoa maoni yake bali alikaza agizo la Bwana, ambalo halijadiliwi, ni la kulitii. Waliooana wakae pamoja, nao wakishindwa, basi kila mmoja akae peke yake bila kumchukua mwingine.

7:12-16 Muumini aliyeoa/aliyeolewa na asiyeamini

Bila shaka wengi walijikuta hivyo wakati mmoja alipoongoka na mwenzake hakuongoka. Afanye nini? Paulo alishauri kwamba ni juu ya muumini kujitahidi kukaa na mwenzake, ila kama mwenzake akikazana kumwacha basi amruhusu kwenda. Ila si wazi kwamba Paulo aliona kwamba mwenzake akiondoka yule muumini yu huru kuoa/kuolewa tena au vipi. Sababu ya muumini kujitahidi kukaa na mwenzake ni tumaini la kumvuta na maisha yake mema ya kikristo ili yeye naye apate kuamini. Kuhusu watoto wao Paulo alifundisha kwamba imani ya kikristo ina nguvu ya kuwafunika, wahesabiwe wa yule muumini na baraka za ulinzi wa Mungu zitakuwa pamoja nao kutokana na imani ya mmoja katika ndoa hiyo.

7:17-24 Kuishi maisha kufuatana na jinsi mtu alivyo

Watu walikuwa katika hali mbalimbali walipokata shauri la kuamini, baadhi walikuwa watumwa, wengine wametahiriwa, na hali kadhalika, wafanyeje? Je! waibadili hali yao? Paulo aliwashauri kila mtu akae tu jinsi alivyokutwa, kitu kikubwa ni kumfuata Kristo katika hali aliyoitwa.

7:25-38 Wanawake walio mabikira

Paulo alielekea kupenda watu wasioe/wasiolewe. Hasa sababu yake ilikuwa moja, wawe na uhuru wa kumtumikia Bwana bila masumbufu. Alifikiri mwenye familia hana uhuru kama yule asiye na familia. Asiye na familia aweza kumtumikia Bwana saa zote na habanwi na shughuli nyingine. Katika k.26 na k.29 ametumia maneno „kwa shida iliyopo". Hakusema ni shida gani kwa hiyo sisi hatuwezi kuelewa kwa usahihi ni shida gani aliyoisema, pengine ni mateso, au hatari fulani katika jamii, au wazo la kufikiri Yesu atarudi karibuni.

7:39-40 Wajane

Paulo aliona kwamba mjane aweza kuolewa tena, ila apaswa kuolewa na muumini. Kama hasikii haja ya kuolewa tena afadhali abaki bila kuolewa.

Kwa maneno ya mwisho wa sura hiyo ni dhahiri Paulo aliutafuta uongozi wa Roho kwa mashauri yake.

MASWALI

Je katika mazingira ya siku zetu mashauri ya Paulo bado yanafaa? Matatizo mengi katika ndoa za Kikristo husababishwa na nini? Je! hata katika shughuli za Kanisa ni vema watu watengwe kwa muda mrefu na wake zao kwa sababu ya kufuata masomo ya Biblia na theologia? Kanisa laweza kutoa msaada gani au kuwa na tahadhari gani? Waonaje?

8:1-11:1KANUNI YA KUUTUMIA UHURU KATIKA KRISTO

Tumekwishaona tabia ya wakristo wa Korintho ya kuutumia uhuru wao katika Kristo bila kujali matokeo yake kwa wakristo wenzao waliotofautiana nao, au ushuhuda wao kwa wasioamini.

8:1-6 Ujuzi wa sanamu

Siku zile sehemu kubwa ya maisha ya watu wote isipokuwa Wayahudi ilitawaliwa na miungu na sanamu na kutoa sadaka. Katika familia kila jambo lilikuwa na „mungu" wake, katika kazi kila ufundi ulikuwa na chama chake kilicho chini ya ulinzi wa „mungu" fulani. Vilevile kwa serikali na katika uongozi wa miji na vijiji kila sherehe ya kuadhimisha kitu fulani ilitangulizwa na ibada na kutolea sadaka kwa miungu. Kwa nini ilikuwa hivi? Ni kwa sababu waliamini kwamba miungu ina uwezo wa kuleta madhara mbalimbali, kwa hiyo budi waitulize kwa sadaka ndipo watakuwa salama. Sehemu ya nyama iliyotolewa ilikwenda kwa makuhani na kama ni sherehe ki-familia iliyobaki ililiwa na watu wa familia hiyo. Nyama nyingine ilipelekwa sokoni na kuuzwa. Kwa hiyo Wakristo walibanwa kwelikweli, wafanyaje? wasiposhirikiana katika mengine watahesabiwa wasiopenda wenzao, wakishirikiana ushuhuda wao utapungua. Walio na kazi walikuwa katika hatari ya kuondolewa kazi wakikosa kuhudhuria sherehe za chama.

Wakristo walitofautiana katika mawazo yao na itikio lao. Baadhi waliudai uhuru wao katika Kristo. Walishirikiana katika sherehe hizo hata kiasi cha kuingia mahekaluni mwa miungu na kula chakula kilichotolewa kwa sanamu.

Katika ujuzi wao walisema kwamba sanamu si kitu, haina ukweli wala uhai, tena hakuna miungu ila katika mawazo ya watu tu, na chakula kilichotolewa kwa sanamu, na kwa asili kimetoka kwa Mungu, kwa hiyo hawatadhuriwa. Waliuvunia ujuzi huo na kwa ujasiri walihudhuria sherehe hizo.

8:7-13 Ndugu dhaifu wa imani

Iwapo Paulo aliuunga mkono ujuzi wa wenye nguvu katika kuona sanamu kuwa si kitu na ya kwamba hakuna miungu, hata hivyo hakuwaunga mkono mwenendo wao wa kuwakwaza wakristo walio dhaifu. Shida ya walio dhaifu wa imani ilikuwa kwamba hawakuweza kusahau jinsi walivyowaza mambo hayo kabla ya kuamini. Waliogopa kwamba wakihudhuria sherehe hizo mashetani wataidaka imani yao na dhamiri zao zingali zikiwashtaki, watakosa amani moyoni. Kitu kilichowasumbua kilikuwa dharau ya wakristo wenzao, bila shaka wengine walikubali kwenda kinyume cha kutaka kwenda ili wasidharauliwe. Paulo alikaza sana wajibu wa upendo unaojenga kinyume cha ujuzi unaobomoa. Aliwakemea sana „wenye nguvu" kwa kujivunia ujuzi wao. Kweli ujuzi wao ulikuwa sawa, lakini umewaingiza katika kiburi na dharau kwa wakristo wenzao, na zaidi ya yote wameacha kwenda katika upendo, njia iliyo

bora. Tena aliwafundisha kwamba iwapo ujuzi wao ulikuwa sawa haukuwa kamili na jambo lililo kubwa si mtu kumjua Mungu bali Mungu kumjua mtu. taz.8:1-3 Ling. na 2 Tim-2:19.

Mwishowe Paulo alisema maneno magumu, maana alisema kwamba kumkwaza Mkristo aliye dhaifu wa imani ni dhambi juu ya Kristo mwenyewe, akiwakumbusha kwamba hata walio dhaifu wa imani Kristo amemwaga damu yake kwa ajili yao.

MASWALI

Je! waonaje kuhusu Wakristo wa ki-sasa na uhusiano wao na mila na desturi za zamani? Je? kimawazo wanasumbuliwa nazo? Je! Wafanyaje? hasa wanapotofautiana katika mawazo yao? Je! Ni mila gani ambazo Wakristo wapaswe waziache?

9:1-27 <u>Kielelezo cha Paulo</u>

Paulo alikuwa na haki zote za Mitume kama Petro na wenzake waliowekwa na Yesu Kristo. Alikuwa mtume halisi kwa sababu alikuwa amemwona Yesu na kuwekwa naye wakati alipokwenda Dameski. k.1 ling. na Mdo.1:22 na Mdo.9:lku. Tena Wakorintho wasingaliona shaka juu ya utume wake kwa sababu alipofika kwao na kuihubiri Injili Mungu aliuthibitisha na kuubariki na matokeo yalikuwa Wakorintho walimuumini Kristo na Kanisa lilizaliwa miongoni mwao k.1,2. Kwa nini Paulo anajitetea sana katika sura hiyo? Inaonekana Wakorintho wengine walisema yeye si mtume halisi, maana alipokuja alijitegemea kwa riziki zake, hakukubali wamtunze.

Haki moja ya Mitume ilikuwa watunzwe na wale wa mahali walipofikia, na wakija na wake zao, wote watunzwe. Kwa sababu ya farakano wale ambao si `wa Paulo" walikuwa tayari kukamata neno kama hilo na kulitumia vibaya juu ya Paulo. Kama Mitume walikuwa na haki hiyo, na Paulo hakuidai, ama ana kiburi kingi, au ni dalili ya kuwa hata yeye mwenyewe alijua utume wake sio sawa na wale wengine.

Paulo aliusimamia uhuru wake wa kukubali kutunzwa au kutokukubali. k.1, 12, 18. Baada ya kuuonyesha uhalisi wa utume wake (1-4) aliendelea kwa kuisimamisha haki ya kutunzwa. Alitoa mifano ya kazi mbalimbali; kama askari aendaye vitani si kwa gharama yake bali kwa gharama za wale wanaomtuma. Mkulima hanunui chakula anacholima, na mchungaji hakosi kunywa maziwa. Kwa hiyo mitume wanayo haki kabisa ya kutunzwa na wale wanaoshirikishwa Habari Njema. Pia mafundisho ya Torati yanakubaliana na haki hiyo, „ng"ombe asifungwe kinywa anapopura nafaka" maana yake awe na nafasi ya kula kwa uhuru. Kum.25:4. Hata Bwana Yesu ameamuru vivyo hivyo, k.14 ling. na Luka 10:7. Pia katika dini ya Kiyahudi watumishi wa Mungu walitunzwa k.13, ling. na Hes.18:8, 31 na Kum;18:1-3.

Iwapo Paulo ameisimamia haki hiyo kwa nguvu, yeye mwenyewe aliona vema asiwadai wamtimizie haki hiyo: Kwa nini? Si kwa sababu hakuwa na haki hiyo, wala si kwa sababu yeye hakuwa mtume halisi kama Petro; kama mwanzilishi wa Kanisa kati yao, kwao haki hiyo ilizidi - mbona basi hakuidai?

Ndipo Paulo alieleza sababu kuwa „asiizuie Injili" k.12 na „kuitoa Injili bila gharama" k.18. Alitambua tabia ya wakorintho, hakutaka kuwapa nafasi waseme kwamba aliitafuta faida yake mwenyewe. Yeye alisikia deni la kuhubiri Injili k.16, Ling, na Rumi 1:14, kwa hiyo ataitoa bure hali akijua atapata thawabu ya kiroho k.17.

Paulo ameutumia uhuru wake kwa lengo la kuvuta watu wa hali zote wapate kumjua Kristo k.19. Amekubali kuwa „mtumwa" wao akijihusisha kabisa na watu wa kila kabila na kila hali kwa lengo moja la kuwaleta kwa Kristo, k.22-23 Amekuwa tayari kuutumikisha mwili wake kwa ukali ili aushinde, kisha apate taji isiyoharibika. Aliutumia mfano wa wachezaji hodari, jinsi wanavyojitawala iii wafaulu, (michezo mikubwa ya Isithimia ilifanyika karibu na Korintho kila miaka mitatu)

MASWALI
Fikirini juu ya mtumishi wa Mungu na uvutano uliopo kati ya kutaka kupendwa na watu na kuwapendeza ili awavute kwa Kristo na hatari ya kujipendekeza kwao na kuridhiana nao kinyume cha mapenzi ya Mungu.

10:1-13 <u>Kielelezo cha Waisraeli zamani</u>

Kama tujuavyo Waisraeli walitolewa utumwani na kuletwa jangwani kusudi wajifunze namna ya kumpendeza Mungu.

Lakini hawakuutumia uhuru wao kwa utukufu wa Mungu bali kwa kujipendekeza. Paulo alifikiri wakristo wa Korintho walikuwa katika hatari ya kufanana na hao Waisraeli, akiwaonya juu ya hali zao.

Waisraeli wa zamani walijifariji kwa kufikiri kwamba Mungu hawezi kuleta mabaya juu yao - si amewatoa Misri kwa maajabu mengi na kuwafanyia makubwa! Katika vifungu vinne vya kwanza neno moja limerudiwa mara tano - neno ni „wote" halafu katika k.5. amesema „lakini wengi katika hao" yaani katika wale wote. Wote hao walizishiriki baraka kubwa mno, walivuka Bahari ya Shamu kwa nchi kavu. Jangwani waliongozwa njia kwa mchana na usiku, kwa nguzo ya moto na kwa wingu, kila siku kwa miaka arobaini walilishwa chakula cha „mana" Waliongozwa na kiongozi hodari, Musa. Wakristo wa Korintho wamezishiriki baraka kubwa, wametolewa chini ya utumwa wa dhambi, na kupewa chakula cha uzima, na kupata uongozi na msaada wa Roho Mtakatifu, na kuwa na Yesu Kristo kielelezo chao na kupewa karama nyingi za Roho.

Ilitokeaje kwa Waisraeli waliomwasi Mungu jangwani? Walipotea jangwani, katika wale wote ni wawili tu waliofika nchi ya Kanaani! Itakuwaje kwa wakristo wa Korintho wasipoijali imani hiyo yenye baraka kubwa mno?

Haitoshi wadai „wameokoka" kwa huduma ya Paulo, au Kefa, au Apolo, au nani?

Katika mawazo ya Paulo historia ya Waisraeli haibaki kuwa historia tu, bali ni mafundisho na maonyo kwa watu wa Mungu wa baadaye, kwa Wakorintho, na kwa sisi tunaoishi wakati huo vilevile, „yakaandikwa ili kutuonya sisi" k.11.

Hatari kwa wakristo wale na kwa sisi ni kujidhania kuwa tumesimama; tusijione kuwa tunayo nguvu, wala tusiwe na kiburi cha kiroho. Hata hivyo tunayo ahadi njema sana ya msaada wa Mungu majaribu yanapotujia. Mungu ni muuminifu na wakati wote atatupatia njia ya kuyashinda, hawezi kukubali tujaribiwe kuliko uwezo wetu wa kuyastahimili ila kwa upande wetu tusijiweke katika magumu bila kuutambua udhaifu wetu, tuwe tunamtegemea Mungu na nguvu zake.

10:14-22 Hamna ushirikiano kati ya karama ya Kikristo na ya sanamu

Paulo aliwaita „wapenzi wangu" k.14 akiwasihi kwa upendo waifuate njia njema. Kama alivyowashauri juu ya uasherati 6:18 kwa kusema „kimbieni" vivyo hivyo kwa ibada ya sanamu alisema „ikimbieni" k.14. Waikatae kabisa, na kujitenga mbali nayo. Wasifanane na watu wasogezao kidole kwenye mwali wa moto ili waone ni kwa kiasi gani wawezacho kuukaribia bila kuunguzwa na moto. Kinyume cha kusogea ni kukimbia.

Wakorintho walifikiri wanayo akili nyingi k.16 kwa hiyo Paulo aliwashauri waitumie kwa kutafakari mambo ya ibada ya sanamu. Katika sura ya nane tumeishaona Paulo alikuwa na uhakika kwamba sanamu haina ukweli wala uhai wo wote, na chakula kilichotolewa kwa sanamu hakimdhuru mtu. Hata wakristo wa Korintho waliamini vivyo hivyo. Ubao ni ubao tu na jiwe ni jiwe tu potelea mbali vimechongwa kuwa sanamu. Kama ni hivyo mbona Paulo aliwaambia kuikimbia ibada ya sanamu, hatari ilikuwa ya nini hasa?

Paulo alifundisha kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya sanamu na mashetani, kushirikiana katika ibada ya sanamu ni kushirikiana na mashetani. Mkristo, anapoishiriki meza ya Bwana anashirikiana na Kristo Mwenyewe, kuna uhusiano mkubwa kati ya meza ya Bwana na Bwana Mwenyewe iwapo mkate ni mkate tu na divai ni divai tu, kwa imani ya kuisogea Meza hiyo na kuvishiriki vitu vyake tunashirikiana na Bwana.

Paulo alisema wazi „hamwezi kukinywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. Hamwezi kushiriki katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani!

Bwana Yesu aliyewafia msalabani anawapenda upeo, kwa hiyo kuridhiana na sanamu na kuishiriki ibada ya sanamu ni kumtia wivu. Katika kiburi chao cha kiroho cha kujiona kuwa wenye nguvu walikuwa katika hatari ya kumhuzunisha Bwana Yesu.

10:23-11:1 <u>Matokeo ki-utendaji</u>

Tuliona katika sura ya nane kwamba karibu nyama yote iliyouzwa sokoni ilikuwa imekwisha kutolewa kwa sanamu. Kwa hiyo, wakristo wafanyaje? Je! wahakikishe kwanza kama imekwishatolewa kabla ya kuinunua au vipi? Paulo alisema kwamba hawana haja ya kuuliza maswali. Vilevile wakialikwa kula nyumbani mwa mtu wasifanye utafiti juu ya chakula bali wakile tu. Ila kama aliyewaalika atasema wazi kimetolewa kwa sanamu, basi wasile. Kwa nini? kwa sababu yule mtu amekuwa mhukumu wa uhuru wa yule mkristo, akitaka kumtia utumwani mwa mawazo yake.

Kwa asili vyakula vyote na vitu vyote vimetoka kwa Mungu Mwumbaji. Vyote vimetolewa vitumiwe kwa shukrani. Ling. Mko 7:17-19. Mkristo amewekwa huru na Kristo aweza kula cho chote apendacho. Ila uhuru huo usitumiwe kwa kuwakwaza wasumbuliwao na dhamiri zao wakiwa na miiko juu ya chakula kingine. Shabaha ya mkristo wakati wote ni kuvuta watu wa aina zote ili wapate kuokolewa kwa kutokuwakosesha na kwa kuwapendeza katika yote isipokuwa wasifanye dhambi.

MASWALI

Je! Mpaka leo wako waumini wanaofikiri kwamba potelea mbali waishije Mungu atawakubali? Tuwasaidiaje? Je! Maonyo ni sehemu ya mafundisho inayotakiwa? Na marudi yanatakiwa pia?

11:2-14:40 IBADA ZA KIKRISTO NA WAO KUKOSA UTARATIBU

Baada ya kupata waongofu mahali fulani Paulo aliwapa mwongozo kwa maisha yao mapya katika Kristo na kwa ibada zao.

Katika sehemu hiyo Paulo alianza kwa kuwasifu kwa kufuata mwongozo aliouwapa juu ya ibada k.2. Ila tunapoendelea tunaiona tabia yao ya kufanya walivyotaka kinyume cha uongozi waliopewa, wala hawakuona kuwa tofauti na makanisa mengine kuwa kitu. Walifanya mengine yaliyoupunguza ushuhuda wao na katika mengine walikuwa katika hatari ya kufanya dhambi.

11:2-16 <u>Wanawake kuvaa taji</u>

Katika shirika zao pale Korintho wanawake waliacha kuvaa taji wakidai kwamba Kristo amewaweka huru kwa hiyo hawana haja ya kufungwa na desturi hiyo. Paulo alikataa. Zamani zile ni wanawake wenye maisha mabaya ambao hawakuvaa taji, wakitambulikana kuwa makahaba kwa njia hiyo. Paulo

hakutaka wanawake wa Kikristo wawazwe vibaya na kuleta sifa mbaya kwa kanisa. Si vizuri wautumie uhuru wao kwa jinsi hiyo.

Paulo aliendelea kwa kutoa mafundisho kuhusu mahali pa mwanamke katika uumbaji. Yeye ametoka kwa mwanaume, na ubindamu wake ni sawa na ule wa mwanaume. Ki-mipango yu baada ya mwanaume k.8 ila pia wote wawili hutegemeana kabisa k.11.12. Tena heshima ya mwanamke ni kubwa katika uhusiano wake na mwanaume k.9. Katika ibada za Kikristo wote wawili walipewa nafasi ya kusali na kuhutubu k.4.5 Katika Biblia ya Kiswahili neno moja la Kiyunani halikutafsiriwa vizuri, taz.k.10 linalosema „kumilikiwa" badala ya „kumiliki". Kwa kufunikwa kichwa mwanamke alimiliki, akiwa na mamlaka na heshima. Aliweza kupita po pote bila kuguswa, bila kudharauliwa, na bila kushambuliwa. Kwa kuvaa taji „alimiliki" tena kwa kuvaa taji alikiri ya kuwa anaye „kichwa" yaani mume wake.

Kwa wakati wetu jambo hilo halina nguvu maana hali na mazingira yetu vimebadilika. Kwa hiyo hatufungwi na desturi hiyo ya kuvaa kitu fulani kichwani. Ila bila shaka bado tunapaswa kuangalia kwamba tusifanye lo lote litakalofanya Ukristo uwazwe vibaya na kueleweka usivyo, wala tusiende kinyume cha desturi katika maadili ya wakati wetu.

MASWALI

Makanisa hutofautiana katika kutoa au kutokutoa masharti kwa waumini kuhusu jambo kama hilo la kuvaa kitu kichwani, au nguo za kuvaa na urefu wake, au urembo mbalimbali. Je! Waonaje? twafungwa kabisa na lililoandikwa iwapo mazingira yetu ni tofauti, au tuwe tunaongozwa na misingi idumuyo wakati wote, ya kufanya kwa uzuri na utaratibu na kwa kutoa kielelezo kitakachofanya Ukristo usiwazwe vibaya?

11:17-34 Chakula cha Bwana

Kwa habari hii Paulo hakuwa na neno la kuwasifu bali alitoa maagizo na maonyo kwa uzito. Ilimbidi aitumie mamlaka yake ya ki-mitume kwa sababu ya mambo kuwa mabaya, maana badala ya wakristo kujengwa kiroho na ibada hiyo walikuwa katika hatari ya hukumu ya Mungu. Mpango wa ibada ya Ushirika ulitofautiana na mpango wetu wa sasa. Wao walikutana pamoja kwa kula kwanza, kila mmoja akileta chakula na kushirikishana walicholeta, ndipo baadaye walifanya kumbukumbu ya Kifo cha Bwana Yesu kama alivyoagiza. Karama hiyo waliiita „karama ya upendo" (love-feast,au Agape) Kumbe, pale, haikuonekana ni karama ya upendo, maana walibaguana wao kwa wao na kukaa vikundi vikundi, na wengine kama watumwa wasiokuwa na uwezo wa kuleta chakula waliachwa, walikosa cha kula, huku wengine walikula kupita kiasi. Umoja uko wapi? upendo uko wapi? kujengana ku wapi? Paulo aliwakumbusha asili ya ibada ya Chakula cha Bwana, jinsi Bwana Yesu usiku ule kabla ya kuuawa alivyochukua mkate na kusema „huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu, na vile vile kwa divai" ...

Yawezekana maelezo hayo ni ya kwanza kuandikwa kwa sababu waraka huo ulitangulia kuandikwa kabla ya Injili. Daima ibada hiyo ni kumbukumbu ya Kristo na kifo chake msalabani kwa ajili yetu. Ni Yesu Mwenyewe aliyetuagiza tuifanye akitoa na sababu yake ya Kumkumbuka Yeye. Kwa njia yake kifo chake kinatangazwa, ni mahubiri ya „ki-matendo". Pia ni „mpaka ajapo", kwa hiyo katika ibada hiyo twatazamia kurudi kwake. Twashirikiana naye katika ibada hiyo.

Yatupasa kuja kwenye ibada hiyo kwa heshima, na kwa kuijali, na kwa kujihoji kwanza. Kwa nini? ni kwa sababu baraka ni kubwa sana, ni kushirikiana na Kristo Mwenyewe. Kwa upande wa pili hukumu ni kubwa pia, ni kuwa na hatia ya mwili na damu ya Kristo. Paulo aliona ya kwamba hukumu hiyo huleta watu kuugua, na hata baadhi kufa.k.30.

Aliwasihi wayarekebishe makosa hayo, kila mtu amngojee mwenzake ndipo kwa kukishirikisha kile walicholeta kila mmoja apate kula. Iwe nafasi ya kupendana kwa kweli, wala si ya kula tu.

MASWALI

Je! Siku hizi Wakristo huithamini na kuiheshimu ibada ya Ushirika Mtakatifu au ni wengi ambao huja katika Meza ya Bwana bila kujihoji na bila kujali? Je! wahudumu wachukue hatua zipi za kuwasaidia Wakristo wao?

12:1 - 14:40 <u>Karama za Roho</u>

Katika sura ya kwanza Paulo alidokeza kwamba pale Korintho watu walipoamini Roho aliwapa karama mbalimbali. Baadhi ya karama hizo mojawapo ilikuwa kusema kwa lugha. Baadaye karama hizo zilileta shida kutokana na tabia yao ya kufarakana na kubaguana. Waliikuza karama ya kusema kwa lugha kuliko ilivyowapasa na kuitumia isivyo halali. Fujo ilitokea katika ibada.

Paulo alianza kwa kuisemea hali ya wapagani. Aliwahurumia kwa sababu ni watu „wanaochukuliwa" maana yake waliifuata miungu yao bila kuwa wamewaza na kukata shauri kwanza, walijikuta wameirithi miungu hiyo, „wamechukuliwa". Wamechukuliwa wapi? kwa sanamu zisizonena, miungu yao hawajifunui kwao, wala kuwajibu, wala kuwajulisha habari.

Lakini haiwi hivyo kwa mkristo. Labda katika hali ya msisimko wengine wamesema mambo yasiyo kweli wakidai wamechukuliwa na Roho. Yawezekana mmoja amesema „Yesu amelaaniwa" k.3. akichanganyikiwa katika mawazo yake kuhusu Yesu kuichukua laana ya Torati pale msalabani - Ga1.3:13. Je! ni kitu gani kinachoshuhudia uongozi wa kweli wa Roho, msisimko? au maneno yanayosemwa? Kwa Paulo ni maneno yanayosemwa. Ni mtu yupi aliye na Roho? ni yule anayemtambua Yesu kuwa Bwana na kukiri

hivyo kwa maneno na maisha yake. Hata katika uamsho wa Roho wakristo si watu wa kuchukuliwa, budi wazitumie fahamu zao kuitika itikio lao hasa kutokana na imani yao na ufunuo wa kweli.

Ndipo Paulo aliendelea kuwafundisha juu ya karama za Roho ili ayarekebishe makosa yao ya kubagua kati ya karama na karama na kuzithamini tofauti pia kubagua kati ya waumini kufuatana na karama walizo nazo. Alitaka kufundisha mambo mawili makubwa, umoja na utofauti uliomo katika umoja huo. Neno la Kiyunani kwa „karama" lina maana ya „fungu".

Kila karama ilikuwa na asili moja, ilitoka kwa Roho aliye Mmoja tu. Roho hutoa karama kwa lengo na kusudi fulani, hafitiniki juu ya nafsi yake, naye huelewa kabisa amekusudia nini katika kumpa mtu fulani karama fulani. Karama zote hutolewa kwa shabaha moja tu ya kuhudumiana. Ni Bwana amwezeshaye kila mmoja kuitumia karama yake kwa faida ya wengine. Kila mtu huwa na njia yake ya kufanya kazi na afanyaye kazi ndani yake ni Mungu. Mungu wetu ni Mungu apendaye „utofauti". Katika uumbaji neno hilo ni dhahiri, rangi ni mbalimbali, sauti ni mbalimbali, umbo ni mbalimbali - kila ndege na wimbo wake, kila ua na rangi yake, kila jani na umbo lake. Ila Mwumbaji ni Mmoja. Mtu hupewa karama si kwa faida yake bali kwa faida ya wengine ndipo „utajiri wa kiroho" utazidi kwa wote. Kwa hiyo kumkweza mtu kwa sababu ya karama yake na kumwonea mtu kwa ajili ya karama yake, na kushindana wao kwa wao ni makosa makubwa. Kila mtu amepewa, kila mmoja anayo, na wote walipewa kutokana na ukarimu wa Mungu kwa neema yake, bila kuangalia ubora wa mtu au kustahili kwake.

Paulo aliyaendeleza mafundisho kayo juu ya Umoja na Utofauti uliomo katika umoja, kwa kuutumia mfano wa mwili na viungo. Mfano rahisi wa kueleweka na wa kufaa sana. Mkristo ni mtu aliyewekwa na Roho „katika Kristo" na waumini wote kwa pamoja ni „Mwili wa Kristo".

Tofauti za viungo si bahati nasibu, zimekusudiwa. Kama kiungo fulani chafanya kazi ya maana sana katika mwili, hata hivyo nje ya mwili na bila mwili hakina maana yo yote k.14. Paulo alitaka kuwatia moyo wakristo ambao karama zao hazikusifiwa na kuthaminiwa na wenzao, huenda wengine walifikiri kwamba hawana karama yo vote. k.15,16. Kila Mkristo ni wa pekee, anacho cha kuleta kwa faida ya wenzake ambacho mwingine hanacho. Mungu hupenda wote, si Mungu wa „wenye maana" na „walio nguzo" tu. Wale wenye vipawa vikubwa hawawezi kuishi bila „viungo vingine vinavyodhaniwa kuwa vinyonge, visivyo na heshima" Wenye vipawa visivyosifiwa huhitajika sana, tena wakubaliwe kwa moyo mweupe. Ni Mungu apangaye na kutawala, hapendi farakano katika jamii ya wakristo, anataka watunzane na kusaidiana k.24,25. Kwa mfano nikikata kidole, mwili wangu mzima hujishughulisha kwa ajili yake bila kukilaumu. Mwili mzima huzishiriki shida na baraka zinazoupata, vilevile katika jamii ya Wakristo.

Katika kufunga sehemu hiyo Paulo aliutilia mkazo Mungu kuweka watu katika Kanisa lake, watu hawakujichagulia. Mitume waliwekwa kuwa wa kwanza kwa vile walivyochaguliwa na Yesu Mwenyewe, wakipewa heshima kubwa ya kuwa watangazaji wa kwanza wa Injili na ulinzi wake. Waalimu ni wa tatu kwa sababu ya umuhimu wa mafundisho ya kikristo. Wenye karama ya kusema kwa lugha waliwekwa mwishoni, kinyume cha mawazo ya Wakorintho.

Paulo hakuona ilikuwa vibaya kwa Wakorintho kutafuta karama zilizo kuu, ila walikosa kufahamu ni zipi zilizo kuu hasa. Ila aliwafahamisha kwamba njia ya kuzitumia ni muhimu kuliko karama zenyewe, na njia iliyo bora ni upendo.

MASWALI

Je! Katika makanisa yetu wakristo wanatiwa moyo kumwomba Mungu awape vipawa kwa lengo la kujenga Kanisa mahali walipo? Pia Je! wanapewa nafasi za kutosha kwa kuvitumia?

Ni shida zipi ambazo zimetokea kutokana na uamsho wa matumizi ya vipawa hivi vya Roho? Je! Zatosha kusababisha viongozi wasikubali vitumiwe? Mhudumu aweza kutoa ushauri gani na msaada gani kuhusu neno hilo?

Sura ya 13: Ni sura ijulikanayo sana na wasomaji wa Biblia, inahusu „upendo" ni kama „wimbo wa upendo" ikionyesha upendo wa kweli kuwa na mambo gani na tabia gani. Neno la Kiyunani ni „agape" neno ambalo wakristo walilitumia kama neno jipya, halikutumika sana kabla ya wakristo kulitumia, nao walilichukua na kulitia maana mpya kufuatana na kielelezo cha maisha ya Bwana Yesu. (Katika Kiyunani kuna maneno matatu au manne kwa upendo wa aina mbalimbali). Wakati wo wote sura hii italeta msaada mkubwa katika kuufahamu upendo wa kweli. Katika mazingira ya wakristo wa Korintho na matatizo yao mbalimbali, na hasa kuhusu matumizi ya karama za Roho bila shaka ilisema kwa nguvu sana. Wakiukosa upendo hata wakiwa na kipawa gani au uwezo gani hawana faida.

Walikuza sana mambo ya hotuba, usemi, n.k. na hapo Paulo ametoboa wazi kwamba ipo lugha yenye nguvu kuliko maneno ya lugha walizozisifia, nayo ni lugha ya upendo, upendo unaodhihirika katika matendo. Paulo alizifananisha lugha zao za ajabu ajabu bila upendo kuwa kama debe tupu inayopiga kelele k.l. Hata „unabii" „si kitu" bila upendo k.2. Hata mtu kujitoa kiasi kikubwa asipofanya kwa upendo, hana faida, k.3. Halafu sifa za upendo ziliandikwa, hali hizo zitawasaidia kuishi bila shida ya kufarakana, na zitawajenga waumini wote kwa pamoja. Kisha Paulo alionyesha jinsi ambavyo ni upendo tu utakaodumu na kushinda. Karama nyingine zitapita, hazitahitajika tena. Mtu huhitaji kukua katika imani yake na kuwa „mtu mzima" sawa na anavyokua kimwili.

Kwa mfano, kama mtoto hakui tutamwaza kuwa mgonjwa, vilevile Mkristo asipokua, hasa katika upendo, tumwazaje?. si „mgonjwa" kiroho?

Katika sura ya 14 Paulo alirudia kusema juu ya karama mbalimbali. Alitaka kuwaonyesha jinsi karama nyingine zinafaa kutumika katika mikutano yao na ibada zao kuliko karama ya kusema kwa lugha. Kusema kwa lugha ni karama kweli na ni vizuri waitumie, isipokuwa wafahamu ni kwa mtu kujijenga nafsi yake k.4.5. Isitumiwe katika ibada bila kuwepo kwa mwenye kipawa cha kufasiri, tena kwa kiasi tu, k.28. Maana lugha hizo zisizoeleweka zahusu roho ya mtu si akili k.4.14.19. Paulo mwenyewe alikuwa na kipawa cha kusema kwa lugha lakini hakuitumia kanisani k.18

Ni karama ipi ijengayo sana wakristo katika mikutano yao? Ni karama ya kuhutubu; k.3.4.5. Kwa nini, kwa sababu Paulo alitaka sana watu waelewe vizuri yanayosemwa. Aliutumia mfano wa muziki, tofauti za sauti zawasaidia watu wautambue ni wimbo upi unaopigwa. Vivyo hivyo kwa baragumu, kwa sauti yake watu wataelewa wanaitwa kwa hatari ipi na kuiitikia kulingana na hatari iliyopo. Katika kanisa zikuzwe karama ziletazo uelewano, k.6-9.

Katika ibada mambo yatendeke kwa utaratibu na kwa akili, uvuvio na msisimko wa Roho uandamane na hali hizo. Aliona Wakorintho wangali ni „watoto" wakivutwa na karama ya kusema kwa lugha kuliko karama ya kuhutubu. Ile ya kwanza yaleta mshangao lakini ile ya pili ndiyo itakayowajenga. Kwa wasioamini karama ya kusema kwa lugha ni ushuhuda kwao, itawashtusha, na kuwafanya watambue Uwepo wa Mungu. Karama ya kuhutubu yaleta ujumbe kwa wasioamini ili waguswe mioyoni mwao. Wote wakisema kwa lugha wengine watawadhania kuwa wenda wazima k.22-23.

Tunaposoma sehemu ya k.26-33 twapata picha ya ibada zao. Kila muumini alipata nafasi ya kushiriki katika ibada, kwa kuleta wimbo, au fundisho, kusema kwa lugha na mwingine kufasiri, au kuleta ufunuo. Hawakufuata utaratibu ulioandikwa wala kuwa na mpango maalum. Mwongozo ulikuwa yote yafanyike kwa lengo la kujengana, kwa uzuri, na kwa adabu ya kuachiana nafasi, k.26. Shida moja iliyotokea pale Korintho ilikuwa kuwapa wenye kusema kwa lugha nafasi kubwa. Paulo aliona ni vema wawe wachache tu, na wafanye kwa zamu, na kama hakuna wa kufasiri basi, wanyamaze. Paulo hakukubali kwamba mtu anayesukumwa na Roho anapelekwa tu, hata asiweze kumwachie mwingine nafasi au kuachia kabisa, k.27-28.

Vivyo hivyo kwa upande wa kuutoa unabii, aliona wasichukue nafasi nyingi, pia unabii wao upimwe. Kama mtu atafunuliwa neno wakati ule ule basi apewe nafasi kabla ya yule aliyepangwa. Aliwakumbusha kwamba Mungu wetu si wa machafuko (huenda ibada zao zilikuwa za fujo), kwa hiyo taratibu iwepo pamoja na uhuru wa watu kupata nafasi za kuleta mchango wao kwa uzuri na adabu k.29-31.

Katika sura ya 11 tuliona ya kwamba wanawake walipenda kudai uhuru wao wa kufanya walivyosikia bila kujali ushuhuda wao kwa wasioamini. Katika ibada picha ni kwamba walijionyesha sana na kusema-sema, huenda kuzidi wanaume. Paulo alihofu kwamba Injili itaeleweka vibaya kama wanawake hawatafanya kwa hekima. Walikuwa na nafasi ya kuutoa unabii 11:5 kwa hiyo maana ya Paulo kusema „wanyamaze" si wasiseme lo lote, ila wapunguze hali za kujionyesha na kutaka kuwa mbele katika ibada, na huenda walitatarikana pia, k.34-36. Hawakuona wana haja ya kulingana na makanisa mengine, k.36. Katika hayo yote Paulo alilenga kuwaelekeza kufanya yote kwa kumpendeza Mungu na kumtukuza.

MASWALI

Fikiri juu ya hekima ya Paulo kuweka sura ya 13 juu ya upendo kati ya sura ya 12 na 14 zinazosema juu ya tofauti za vipawa na umoja wa mwili. Ni kitu gain ambacho kitahakikisha kudumu kwa tofauti za vipawa na namna mbalimbali za kuhudumu na njia za kufanya kazi ya Mungu na Umoja wa Waumini? Je! ni kweli ikiwa Upendo utakosekana ama tofauti zitapungua au umoja utapungua? Bila upendo hakuna kuwiana kati yao.

15:1-58 UFUFUO WA MWILI

Inaonekana kwamba wakristo kadha wa Korintho waliukana ufufuo wa mwili kwa sababu walitatizwa na uwezekano wake , hawakuona ni kwa njia gani au kwa jinsi gani mtu aliyekufa atafufuliwa kwa mwili k. 12, 35 .

Paulo alisema kwa kirefu akianzia na uhakika wa Yesu kufufuka kwa mwili na umuhimu wake katika imani ya Kikristo, ndipo baadaye aliwaelezea ni kwa jinsi gani mwili utakavyofufuka.

15:1-11 <u>Ufufuo wa Kristo</u>

Wakorintho walikuwa wameipokea Injili na wamesimama ndani yake. Kwayo wameokolewa kama wataendelea kuishika mpaka mwisho. Waliipata kwa Paulo na Paulo alikuwa ameipata kwa wale waliomtangulia. Mambo makubwa katika Injili ni (i) Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu; (ii) alizikwa; (uhakika wa kufa kwake), (iii) siku ya tatu alifufuka na kuwatokea watu mbalimbali. Kwa hiyo ukweli wa kufufuka kwake ulithibitika kabisa. Jumla ya hayo yote ni Habari Njema.

Ndipo Paulo aliorodhesha baadhi ya wale waliomwona Yesu yu hai baada ya kufa kwake. Kefa ambaye ndiye Petro, Mitume, Ndugu 500 kwa pamoja, ambao baadhi yao walikuwa wangali hai wakati wa Paulo kuwaandikia; (miaka zaidi ya 25 imepita);Yakobo; Mitume tena, na mwishowe Paulo mwenyewe. Ushuhuda wa kiasi hicho unatosha kabisa. Kwa jinsi alivyolitesa Kanisa Paulo aliishangaa neema ya Mungu iliyomjalia kumwona Bwana Yesu na kuzungumza naye, neema ya namna hiyo ilimpa ujasiri na bidii katika kumtangaza Kristo.

15:12-19 Matokeo ya Kuukana ufufuo wa wafu

Paulo alihesabu kwamba neno la ufufuo wa Kristo ni la msingi na bila hilo haupo ufufuo wa wafu. Na zaidi hakuna maana yo yote katika kuwahubiri watu, na hata kuamini ni bure tu. Tena waliotangaza habari hizo ni waongo wakubwa, kwa sababu walisema Mungu amemfufua Kristo, kumbe siyo. Kama Kristo hakufufuka hakuna jambo lililotendeka kuhusu dhambi zetu; tutajuaje kazi yake msalabani ilifaulu bila Yeye kuwa hai baada ya kufa. Tena waumini wote waliomuumini Kristo watakuwa wamepotea baada ya kufa, watu kama Stefano na wengine.

Paulo aliyaunganisha mawili, Kristo alifufuka na kwa sababu hiyo wafu watafufuka; na kama Kristo hakufufuka wala wafu hawatafufuka. Ni shida sana mtu kumuumini Kristo kwa maisha ya sasa tu, bila kutegemea maisha ya uzima wa milele baadaye.

15:20-28 Matokeo ya ufufuo wa Kristo

Iwapo Paulo alionyesha matokeo ya kuukana ufufuo wa Kristo hakuweza kubaki palepale bila kukaza kwa nguvu kwamba „lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala" k.20. Kristo ni limbuko, neno lenyewe „limbuko" laonyesha wengine watafuata. Mauti ililetwa na Adamu wa kwanza, na sote tutakufa kwa sababu tu warithi wake. Kristo ni badala ya Adamu wa kwanza na katika Yeye sote tutafufuliwa. Kristo amelipindua laana yote iliyoletwa na anguko la wanadamu. Mauti ni adui, ambaye itabatilishwa na kutoweka k.26.

Maneno ya k.28 yahusu uhusiano kati ya Baba na Mwana juu ya mpango wa ukombozi si uhusiano wao ki-asili katika Utatu. Kwa ajili ya kazi ya ukombozi Yesu aliwekwa chini ya Baba kwa kuwa ilimbidi afanyike mwili, na afe, na kufufuka, ndipo kurudi kwa Baba. Kisha vitu vyote vitiishwe chini yake kutokana na ushindi alioupata, ndipo mwishoni kabisa atamrudishia Baba kila kitu.

15:27-34 Ushuhuda aina nyingine

Pale Korintho walifanya ubatizo kwa ajili ya mwingine aliyekuwa amekufa. Hatujui zaidi juu ya desturi hiyo, ni hapo tu katika k.29 tuna habari yake. Paulo hasemi desturi hiyo ni nzuri au siyo, ila ameitaja kwa kuonyesha kwamba ni jambo linaloshuhudia uwepo wa ufufuo wa wafu.

Paulo na wenzake walihatarisha maisha yao kwa ajili ya Injili. Je! wafanya hayo kwa ajili ya uongo, kama wafu hawafufuliwi na kama Kristo hakufufuka? Walipatwa na magumu mengi, tena waliwaonya waumini wapya kwamba wataingia Ufalme wa Mungu kwa dhiki nyingi? Je! wangalithubutu kuingiza watu katika kiti kitakachowaletea mateso na dhiki kama hawana uhakika juu yake! Je! wahubiri watadanganya watu huku hawana faida yo yote? Ling. Mdo.14:22. 1 Thes. 3:3.

15:35-49 Uwezekano wa mwili kufufuka ukionyeshwa kwa mfano wa mbegu na mimea na kwa Maandiko

Baadhi ya Wakorintho walipuuza habari ya ufufuo wa mwili kwa sababu walishindwa kuelewa ni kwa jinsi gani mwili uliokufa na kuzikwa na kuozwa utawezaje kufufuliwa? Paulo aliutumia mfano kutoka uumbaji. Mbegu hupandwa ardhini, ni kama „kuzikwa". Kabla ya kupandwa hauonekani kuwa „hai" ila baada ya kupandwa mmea hutokea. Mmea sura yake ni tofauti sana na mbegu iliyopandwa, hata hivyo uhusiano mkubwa upo, kwa sababu mmea hulingana na aina ya mbegu, kila mbegu na mmea wake. Mmea ni kama „mwili" wa ile mbegu. Kama wanadamu wasingaliona jambo hilo likitokea daima wasingaliweza kuamini ni hivyo, maana mbegu ndogo hutokeza mti mrefu sana, miti ya matunda, miti ya ubao n.k. tena mboga za kuliwa zatoka kwa mbegu, hata na maua. Katika mfano huo twapata msaada mkubwa kutuelekeza juu ya uwezekano wa ufufuo wa miili yetu. Lazima tufe, na kuzikwa, ndipo baadaye tutavikwa mwili wa utukufu,. mwili wa roho. Mwili mwenye uwezo mpya. Kama Paulo alivyoeleza mwili huzikwa katika hali ya uharibifu, nao utafufuliwa katika hali ya kutokuharibika, n.k.

Ni uwezo wa Mungu utakaofanya hayo, hata Yesu Mwenyewe alifufuliwa na uwezo wa Mungu. Wala si ajabu. Kama Mungu ameviumba vitu vyote si jambo kubwa Kwake atuhuishe baada ya kufa.

Tutakuwa na mwili gani? ni vigumu kuelewa sana ila tunajua utafaa maisha ya baadaye kama huu wa sasa unafaa maisha ya wakati huo. Tutakuwa na nafsi zetu, ni „mimi" na „wewe" ambao tutafufuliwa. Ni mwili wa roho, huenda maana yake ni kwamba hatutatawaliwa na mambo ya „wakati" na „mahali" kama sasa.

15:50-58 Kushindwa kwa mauti

Wale watakaokuwa hai wakati wa mwisho hawataurithi uzima bila kubadilika „nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu" Hilo badiliko litafanyika kwa haraka mno, kwa uwezo wa Mungu. Uzima wa milele sio kuendelea kuishi tu, bali ni kuishi maisha ya tofauti katika hali tofauti na katika mazingira mapya kabisa. Alipowaza hayo yote Paulo alipaza sauti yake kwa nguvu katika kumshukuru Mungu. Jambo zito si mauti bali ni mauti iliyo mshahara wa dhambi. Kama dhambi imesamehewa ndipo mauti imenyanganywa nguvu yake ya kutisha na kuleta madhara.

Paulo alifunga sehemu hiyo yote kwa kuwasihi wadumu imara na kushika sana uhakika wa ufufuo wa wafu, wawe na moyo na bidii katika kutenda kazi ya Bwana kwa kujua taabu yao haitakuwa bure.

MASWALI

Toa nafasi kwa watu kuzungumzia neno hilo la „ufufuo wa mwili", Pengine walinganishe na jinsi walivyofikiri juu ya maisha baada ya kufa katika imani zao za hapo nyuma na kuona ni nini hasa iliyo tofauti katika Imani ya Kikristo.

16:1-24 MWISHO

16:1-4 Changizo

Paulo alikuwa amelianzisha changizo kwa ajili ya wakristo wa Yerusalemu waliokuwa maskini sana. Pengine, walikuwa wametoa vitu vyao zamani walipoanza kuwa wakristo na sasa hawana akiba - taz., Mdo. 2:43 ku. na 4:32ku. Ki-matendo watasaidiwa sana na changizo hilo litakalotoka kwa makanisa mengi katika Makedonia, Akaya, Asia Ndogo, Galatia n.k. Sehemu kubwa itatoka kwa wakristo wa ki-mataifa. Kwa njia hiyo Paulo alifikiri ni njia ya kuujenga uhusiano kati ya makanisa ya Kiyahudi na makanisa ya ki-Mataifa. Wayahudi wengi walikuwa na mashaka juu ya Paulo na kazi yake katika WaMataifa, kwa hiyo kitu cha upendo cha namna hiyo bila shaka itapunguza mashaka yao.

Inaonekana wakristo walikuwa na desturi ya kutoa mchango wakati wa kukutana siku ya kwanza ya juma, siku yao ya kufanya ibada k.2. Walifuata siku ya kwanza tofauti na Wayahudi walioabudu siku ya saba kwa sababu ya Yesu kufufuka siku hiyo: taz. Yn. 20:19,26 Mdo 20:7 na Uf.1:10.

Utoaji ulifuata uwezekano wa kila mtu binafsi "kama Mungu alivyomfanikisha". Paulo alikuwa mwangalifu sana kuhusu changizo, hakutaka kuwapa watu nafasi yo yote ya kumshtaki kuhusu mambo ya fedha, kwa hiyo alipanga watu kuliangalia katika makanisa yao, na baadaye hao watu watakutana naye mahali fulani na kufunga safari na kulipeleka Yerusalemu.

16:5-9 Mipango ya Paulo

Paulo hakuweza kusema kwa uhakika juu ya mipango yake. Alikuwa na nia sana ya kuwafikia na kukaa nao kwa muda, haidhuru itakuwa kwa muda mfupi tu. Alikuwa Efeso na iwapo vipingamizi vingi vilikuwepo nafasi ilikuwepo kwa kuihubiri Injili. Alikubali mipango yake iongozwe na Bwana.

16:10-12 Timotheo na Apolo

Si wazi kwamba Timotheo amekwisha kwenda Korintho au yu tayari kwenda, Paulo aliwaomba wakristo wampokee bila kumdharau na kumtisha. Timotheo alikuwa kijana aliyefanya kazi ya Injili pamoja na Paulo kama baba na mwana, ila hakuwa mjasiri. Paulo alimuumini sana na kumtuma mara kwa mara kwa makanisa. Paulo alikuwa tayari kumtuma Apolo aende Korintho, ila Apolo hakutaka kwenda wakati ule. Labda aliona italeta shida mpaka watakapokuwa wamelitengeneza farakano. Wako waliompenda sana wakijifanya kundi na kusema „sisi ni wa Apolo".

16:13-14 Kuwasihi

Paulo aliwasihi wasimame imara katika imani na kuwa hodari. Alifahamu wamezungukwa na umati wa watu walioishi maisha yasiyokubaliana na mwenendo wa Kikristo, walijaribiwa sana waridhiane na mambo mbalimbali. Aliwakumbusha wajibu wao wa kufanya yote katika upendo.

16:15 -18 Ombi lake wawajali watu kama Stefana na wenzake

Stefana, Akaiko, na Fortunato walimfikia Paulo pale Efeso wakimletea vipawa, hatujui ni riziki au vipi. Hao ni watu wa Korintho, baadhi ya viongozi wa pale, na Stefana ni mmoja aliyewahi kuongoka pale. Paulo aliburudishwa sana na kuja kwao, bila shaka walimwelezea mengi. Paulo aliwaomba wakristo wa Korintho wawaheshimu na kuwatii, walikuwa wamejitoa kabisa kumtumikia Bwana, huenda walikuwa wamejaribu kuyatatua matatizo yaliyopo, na huenda wengine hawakuwapenda kwa sababu hiyo.

16:19-24 Salaam za mwisho

Aliwapa salaam zake pamoja na salaam za Priska na Akila ambao hapo nyuma waliishi Korintho wakati alipofika Paulo kwa mara ya kwanza. Pia aliwapa salaam za makanisa ya Asia, huenda makanisa mengine yalikuwa mapya kutokana na huduma yake pale Efeso na kandokando yake. Iwapo walikuwa watu wa matatizo mengi, na wengine hawakwenda vizuri katika mwenendo wa Kikristo, hata hivyo Paulo aliwapa wote pendo lake, akiwakumbusha Kuja Kwake Bwana. Hakutaka hata mmoja wao apotee, akijua ni Mungu aliyewaita wamuumini Kristo, ni kusanyiko lake, ni kanisa lake, 1:2.

WARAKA WA PILI KWA WAKORINTHO

YALIYOMO

UTANGULIZI

i. Uhusiano na Waraka wa kwanza
ii. Mwandishi
iii. Tarehe ya Kuandikwa
iv. Sababu za Kuandikwa
v. Mipango ya Paulo itakayotusaidia kuelewa Waraka huu
vi. Umoja wa Waraka

UFAFANUZI

1: 1- 2 Salaam zake
3- 7 Shukrani kwa faraja za Mungu
8-11 Paulo kuokolewa na hatari kubwa katika Asia 12-24 Maelezo ya mabadiliko ya safari ya kufika kwao

2: 1- 4 Barua kali
5-11 Wamsamehe yule mtu aliyemwudhi Paulo
12-17 Ushindi wa Injili

3: 1- 6 Wao ni barua iliyoandikwa na Roho
7-18 Tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya

4: 1- 6 Paulo ni mhudumu wa Agano Jipya
7-18 Unyonge wa Wajumbe na nguvu ya Mungu na Ujumbe wake

5: 1-10 Tumaini la uhakika
11-15 Nia na shabaha za mhubiri
16-17 Upendo wa Kristo na Maisha Mapya katika Kristo
18-21 Ujumbe wa Upatanisho na huduma yake

6: 1-13 Paulo aliwasihi waitike vema na jinsi ilivyompasa aishi
6: 14-7:1 Wito wa kujitenga na wasioamini

7: 2-16 Kurudisha hali ya kuaminiana
8: 1-7 Changizo, kielelezo cha Wakristo wa Makedonia
8-15 Sababu kuu katika Utoaji wa Kikristo
16-24 Tito na wawili wengine kwenda Korintho

9: 1- 5 Sababu za kuwatuma
6-15 Kutoa kwa ukarimu na kuvuna kwa ukarimu

SURA YA 10 HADI 13 - MAMLAKA YA KI-MITUME YA PAULO

10: 1- 6 Silaha za Vita ya Kiroho
7-11 Paulo hakuwa na kigeugeu
12-18 Kazi na eneo la utumishi aliopewa na Mungu

11: 1- 6 Paulo aliwadai Wakorintho utiifu
7-11 Jibu la Paulo kuhusu kijitegemea
12-15 Hali halisi ya wapinzani wake
16-33 Paulo: sifa zake na taabu zake nyingi

12: 1-10 Maono matukufu na mwiba mwilini
11-13 Matokeo ya kufika Korintho hapo nyuma
14-21 Jinsi atakavyofanya atakapokuja tena

13: 1-10 Mpango atakaofuata
11-14 Maneno ya kuagana nao

UTANGULIZI

i. Uhusiano na Waraka wa kwanza

Ni vema kutazama Kitabu cha Ufafanuzi wa Waraka wa kwanza kwa Wakorintho, na hasa katika Utangulizi, habari za Mji wa Korintho, na Uhusiano wa Paulo na Wakorintho, sehemu hizo ni msaada katika kutafakari Waraka huo wa Pili.

ii.Mwandishi

Ni Paulo, kama alivyojitaja katika 1:1 na dalili zote za ndani ni uthibitisho wa Paulo kuwa mwandishi.

iii.Tarehe ya Kuandikwa

Ni kama mwaka mmoja baada ya Waraka wa Kwanza, kwa hiyo, ni kama B.K.55/56.

iv.Sababu za Kuandikwa

Katika Waraka wa kwanza tulipewa picha nzuri ya Kanisa hilo la Korintho. Kanisa hai, lenye mchanganyiko wa watu, waliopewa vipawa vya Roho, ila katika kuvitumia walikosa kuvitumia vizuri, wakishindana juu ya uzuri wa kipawa fulani juu ya kipawa kingine. Pia walikuwa na matatizo katika mambo

ya usafi wa maisha, kushtakiana barazani, kutokujali Ibada ya Chakula cha Bwana, na fujo katika mikutano yao n.k.

Katika Waraka wa Pili twajifunza kwamba Kanisa hilo bado lilikuwa na matatizo mbalimbali na kabla ya kuandikwa kwa Waraka huo uhusiano wao na Paulo ulikuwa mbaya. Ilimbidi aondoke Efeso kwa haraka kwenda kuwaona kwa sababu ya shida zao kuzidi, ila alipofika, hakuweza kufanya lo lote la kuwasaidia, baadhi walimpinga sana na mmoja alimwudhi sana. Kwa hiyo aliondoka halafu akawaandikia barua kali. Katika kuwaandikia Paulo alijifunua wazi moyo wake uliojaa upendo mwingi na masikitiko mengi kwa hali yao, akionyesha mzigo mkubwa aliokuwa nao kwa ajili yao.

v.Mipango ya Paulo itakayotusaidia kuelewa Waraka huu

Katika 1 Kor.4:18-21 Paulo aliwaambia kwamba alitaka kuja kwao mapema, ila baadhi ya Wakorintho waliona mashaka juu ya nia yake ya kuja kwao. Ila alisema atakaa Efeso mpaka Pentekoste ndipo atakuja kwao kwa kupitia Makedonia na kukaa wakati wa baridi 1 Kor.16:5-9. Ndipo baadaye kidogo aliubadili mpango huo, akaamua kuwatembelea mara mbili; mara ya kwanza atakapokwenda Makedonia na mara ya pili atakapoondoka Makedonia. Alitumaini kwamba lile changizo litakuwa tayari (1 Kor.16:4; 2 Kor.1:15ku). Kama ni tayari ataondoka Korintho kwenda Palestina.

Ni nini iliyosababisha aibadili mipango hiyo? Katika 2 Kor.1:8-10 alitaja habari za hatari kubwa iliyompata Asia ila hakueleza hatari hiyo ilikuwa ya namna gani. Pia jambo jingine lilitokea, alisikia habari kwamba shida imezuka tena katika Kanisa la Korintho. Kwa hiyo aliondoka Efeso na kwenda Korintho kwa haraka. Alipofika, baadhi walimpinga na mmoja kama kiongozi wao alimwudhi sana. Basi, aliondoka akisema kwamba hatawafikia tena (2 Kor.1:23-2:2).

Yawezekana Waraka wa kwanza haukufaulu kutatua matatizo yote waliyokuwa nayo. Katikati, Paulo alikuwa amemtuma Timotheo, na huenda Timotheo hakuwa na nguvu za kutosha kushindana nao na kufaulu kuwavuta wayashike maagizo ya Paulo. Twajua Paulo aliwashauri wampokee vema (I Kor.16:10). Pengine ni Timotheo aliyemshauri Paulo aende kuonana nao uso kwa uso.

Safari hiyo ya pili kwenda kwao imetajwa katika 2 Kor.13:2, nayo ni ile iliyotajwa katika 2 Kor.2:1 wakati alipoudhiwa sana na kushushwa sana. Katika safari hiyo upinzani ulifika upeo, walimpinga Paulo na mamlaka yake ya Ki- Mitume na mmoja wao aliyekuwa kama kiongozi wao alizidi hata akamwudhi Paulo sana. Hawakuwa tayari kupokea uongozi na kutii maagizo yake.

Alifanya nini baada ya kuondoka hali ameudhika sana? Aliandika barua kali (2 Kor. 2:4). Katika barua hiyo alifunua mawazo yake ya ndani. Tutachunguza habari hiyo zaidi katika ufafanuzi. Barua hiyo imepotea.

Tito, mjoli wa Paulo, alikwenda na barua hiyo mpaka Korintho na Paulo alipanga kukutana naye Troa. Yeye Paulo ataondoka Efeso kwenda kaskazini na Tito atapitia Makedonia na kufika Troa baada ya kuwashirikisha Wakorintho ile barua. Paulo alionekana kama mtu asiyeweza kutulia mpaka atakapojua hao Wakorintho wameipokeaje hiyo barua na itikio lao limekuwaje. Alipofika Troa hakumkuta Tito na iwapo zilikuwapo nafasi tele za kuihubiri Injili Paulo hakuzitumia. Alitawaliwa na nia ya kuonana na Tito mapema iwezekanavyo. Hivyo alikata shauri kuondoka Troa na kwenda Makedonia na kumwahi huko.

Bila shaka alisumbuliwa na mawazo mbalimbali. Huenda barua yake ilikuwa kali kupita kiasi na pengine imezidisha shida badala ya kuleta nafuu. Labda alifikiri amewatazamia makubwa kuliko uwezekano wao hali wakiwa wangali wachanga ki-imani. Basi alitamani sana sana kuonana na Tito na kujua hali yao halisi.

Walipokutana, Tito alimpasha habari njema. Ile barua kali ilikuwa imefanya kazi njema. Wametii agizo la Paulo na kumwadhibu yule mtu aliyemwudhi Paulo. Ila shida moja iliendelea, hao mitume wa uongo bado wangalipo nao walikuwa wakikazana kuiharibu sifa ya Paulo. Wengine hawakuacha kumnung'unikia juu ya kuibadili mipango. Ila kwa jumla hali yao ilikuwa na nafuu. Kwa hiyo, Waraka huu wa Pili uliandikwa baada ya Paulo kuwa amekutana na Tito huko Makedonia na kupashwa habari zao halisi. Waraka huu wa pili unaonyesha shukrani zake kwa habari hizo na jinsi alivyojisikia kupumua vizuri baada ya wasiwasi wingi.

Katika Waraka huo Paulo alisema mengi kuhusu Huduma ya Injili, utukufu wake pamoja na ugumu wake.

Katika sura za mwisho, kuanzia sura ya 10, kuna mabadiliko katika hali ya barua, Paulo amesema kwa ukali, na amezidi kujitetea juu ya utume wake. Iwapo uhusiano kati yao umetengenezwa, hata hivyo, mitume wa uongo waliendelea kuchochea na kukamata usikivu wa baadhi ya waumini. Paulo alipanga kwenda kuonana nao tena, akiwaonya kwamba hatawahurumia wale wenye kusababisha shida na atawaadhibu wale wasio na utii kwa mamlaka yake (2 Kor.10: lnk: 13: lnk).

Hivyo Waraka huo ni maandalio ya kuwafikia kwa mara ya tatu.

vi.Umoja wa Waraka

Kwa sababu ya tofauti kubwa kati ya Sura 1-9 na sura 10-13; wataalamu wengine wamewaza ya kwamba sura zote hazikuandikwa kwa wakati mmoja. Wengine wamewaza ya kuwa Sura za 10-13 ni sehemu ya ile barua kali iliyotajwa 2 Kor. 2:1 n.k.

Jambo kubwa ni kwamba katika nakala zote za zamani hamna alama yo yote ya Waraka huu kuwa tofauti na unavyoonekana sasa. Pia hamna alama yo yote kwamba sura zake zilipangwa tofauti na mpango tulio nao sasa. Tangu mwanzo Waraka umekuwa kama ulivyo sasa. Wataalamu wa zamani waliochunguza na kusema juu ya vitabu mbalimbali vya Agano Jipya hawakutoa wazo lo lote kwamba Waraka huu ni muungano wa waraka zaidi ya mmoja.

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam zake

Kama ilivyokuwa kawaida ya siku zile mwandishi alijitambulisha ndipo aliwataja wale anaowaandikia, na kutoa salaam zake kwao.

Paulo aliwaandikia kwa mamlaka ya Ki-Mitume ambayo asili yake ilikuwa katika mapenzi ya Mungu, wala haikutoka kwake mwenyewe. Bila shaka alikaza hiyo mamlaka kwa sababu ya wapinzani na jitahada zao kushawishi Wakorintho kwamba Paulo hakuwa Mtume halisi kama wengine, wakijua kwamba wakifaulu kuitikisa mamlaka yake watafaulu kukamata usikivu wa waumini.

Tukilinganisha na salaam zake katika Waraka wa kwanza ziko tofauti ndogondogo. Badala ya kumtaja Sosthene amemtaja Timotheo. Katika Waraka wa kwanza alitaja walioandikiwa kuwa “Kanisa la Mungu lililoko Korintho....” akiwakumbusha kwamba wao ni baadhi ya waumini wote walioko ulimwenguni. Katika Waraka wa Pili alisema “kwa Kanisa la Mungu lililoko Korintho pamoja na watakatifu wote wa Akaya nzima”. Akaya lilikuwa jina la Jimbo lililoundwa na Dola ya Kirumi, na ndani ya mipaka yake miji ya Korintho na Kenkrea ilikuwamo, pamoja na eneo lote la kusini, pamoja na Athene kaskazini yake. Iwapo Paulo alikuwa akiwaandikia watu wa makanisa kadha alijua kwamba ujumbe wake ulifaa Kanisa Zima.

Kila wakati katika barua zake aliwatakia baraka za “neema” na “amani” zilizo msingi kabisa wa Injili, bila hizo mtu hawezi kuwa Mkristo.

1:3-7 Shukrani kwa Faraja za Mungu

Katika sehemu hiyo neno “faraja” limetumika mara kumi. Paulo hakutoa shukrani kwa Mungu kwa ajili yao, kama alivyozoea kufanya katika nyaraka nyingi, ila mara moja alimshukuru Mungu kwa rehemu zake kuu. Karibuni hivi Paulo alikuwa amepitia katika dhiki kubwa naye ameonja kwa upya faraja ya Mungu iliyomtia nguvu na moyo wa kustahimili maudhi na magumu yaliyompata. Kwa hiyo, mara moja, alianza kwa kumsifu Mungu kwa rehema na faraja zake. Alikuwa akiandika kutokana na yale yaliyomgusa sana kibinafsi, na hasa moyoni mwake. Sifa hizo zilijengwa juu ya kweli za Mungu wala si katika hali ya kusikia kwake tu.

k.3 Alimsifu nani? “Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo” yaani Mungu ambaye amejifunua wazi kwa njia ya Mwana wake, kiasi cha sisi kumtambua kuwa Ndiye Mungu na Mungu aliye Baba, na ndivyo alivyo kwetu sisi. Alimtaja Yesu kwa majina yake yote; “Bwana” ufunuo wa uhusiano kati yake na sisi, “Yesu” ufunuo wa Nafsi yake: “Kristo” ufunuo wa Cheo chake.

Huyo Mungu ni “Baba wa rehema” ametuhurumia sana katika umaskini na unyonge wetu, na kwa pendo lake ametukomboa kwa njia ya Yesu Kristo. Pia ni “Mungu wa faraja yote”. Tabia yake ni kuwafariji watu wake, faraja ya kutosha ya kutupitisha salama katika dhiki zetu zote. Yeye aweza kutufariji katika kila aina ya shida, ugumu, na dhiki. Paulo alisema hivyo, si kama sharti moja la imani alilojifunza kwa kichwa, la! bali kutokana na ujuzi alioupata katika maisha yake. Kila mara alipopatwa na dhiki au shida fulani, alionja rehema na faraja za Mungu. Kwake, daima Mungu alikuwa Baba wa Rehema na Mungu wa Faraja yote. Hivyo, aliwezeshwa kuendelea na huduma yake, wala si kwa kustahimili tu, bali pia kwa kusikia baraka.

Kwa hali hiyo Paulo aliweza kuwafariji wengine wakati wa dhiki zao, akiwa na uhakika watafarijiwa na Mungu, akiwatia moyo wa kutazamia ndivyo itakavyokuwa.

k.5 Alisema mateso aliyoyapata, yaliyowazidi wenzake wote, ni “mateso ya Kristo”. Kwa imani alikuwa ameunganika na Kristo sana, kiasi cha kusababisha ateswe sana kama Bwana wake. Hata Wakristo wote watateswa kwa vile hao nao wameunganika na Kristo. Yesu Mwenyewe alisema vivyo hivyo alipotaja habari za “kubeba msalaba kila siku” “kuushiriki ubatizo wake” n.k. (Mt.16:24; 20:23; Flp.3:10) Mara nyingi Paulo aliwaonya waumini juu ya dhiki na mateso (Mdo.14:22; Rm.8:17; 1 The.3:3). Mateso na dhiki zikizidi, ndipo faraja ya Mungu itazidi.

k.6 Paulo alitaka kuwafariji waumini wa Kanisa la Korintho. Wokovu wao ulikuwa hatarini, lakini watasalimika ikiwa Paulo atafaulu kuwaelekeza kutazamia na kupokeai faraja ya Mungu. Yeye alikuwa tayari kutoa maisha yake kwa ajili yao. Kielelezo chake kitawasaidia, nao watatambua ya kuwa wako katika njia iliyo sawa, maana kuteswa siyo kusema wamekosa njia bali ni thibitisho la kuwa katika njia ya kweli ya Mungu, na hata ikiwa kwa muda hawapati mateso, kwa vyo vyote, kwa wakati wake watateswa. Mateso hutofautiana, ila jambo lenyewe la kuteswa ladumu. Uhusiano kati yao na Paulo ulipoharibika ilimbidi Paulo abebe sehemu kubwa ya maudhi ili wao wasilemewe kupita walivyoweza kustahimili. Utayari huo ulisaidia kuleta upatanisho na hali ya kuaminiana kati yao ikakua.

1:8-11 Paulo kuokolewa na hatari kubwa katika Asia

Paulo hakueleza hatari hiyo ilikuwa nini hasa, isipokuwa kusema ilikuwa kubwa kiasi cha kuwalemea mno kuliko nguvu zao hata wakadhani watakufa.

Inaonekana hatari ilitoka kwa nje, na ya kuwa hawakuona njia ya kujisalimisha. Ila Mungu alijiingiza kwa nguvu, na kwa kipekee, akawaokoa. Paulo alieleza tendo hilo la Mungu kwa maneno “Mungu afufuaye wafu”.

Yaonekana Wakorintho hawakuwa na habari juu yake, huenda ilikuwa imetokea hivi karibuni. Baadhi ya watu hufikiri Paulo alisemea habari ya ile fujo iliyotokea Efeso (Mdo.19:23-41) wakati aliposhauriwa asifike kiwanjani. Twajua alikuwa na maadui wengi kwa sababu alisema hivyo katika 1 Kor.16:9. Pengine hao maadui walizidi kufanya mipango ya kuhatarisha maisha ya Paulo na wenzake..

Potelea mbali hatari hiyo ilikuwa nini, twajua Paulo aliona maisha yao yalikuwa hatarini sana, kiasi cha kuuawa, nao hawakuona njia yo yote ya kuondoka katika hatari hiyo, bali ni Mungu peke yake aliyeweza kuwaokoa, na ndivyo Alivyofanya. Jambo hilo lilimfanya azidi kuacha hali zote za kujitegemea na kuzidi kumtegemea Mungu. Pengine alipokuwa akiwaandikia hiyo hatari ilikuwa bado haijaondoka kabisa.

Paulo alitaka waumini wa Korintho wafahamu kabisa kwamba Mungu yu tayari kujiingiza kwa nguvu wakiwa na shida kubwa, nao wapaswa kumwamini kufanya hivyo. Wajue uwezo wa maombi, pia wamwombee yeye na wafanya kazi walio pamoja naye, ili waendelee kuuona uwezo mkuu wa Mungu ukitenda kazi pamoja nao na kwa ajili yao. Mungu hudumu kuwa mwenye rehema, kama tukiomba, au kama tukikosa kuomba. Hata hivyo tuna hakika kwamba Mungu hupendezwa na watu wake wanapomwomba na kumsifu, na kumshukuru, hasa kwa kuyajibu maombi yao. Paulo alitamani sana watu wengi zaidi wamsifu na kumshukuru Mungu. Tusifikiri kwamba maombi yetu yanastahili thawabu, au ni njia ya kumlazimisha Mungu afanye kazi, la, sivyo. Twamwomba Mungu kwa sababu ya tabia yake ya upendo na rehema. Majibu ni zawadi yake, na zawadi hiyo twaipokea na kumshukuru.

Jambo la hatari yao na kuponyeka kwao lilimgusa Paulo sana na kuweka alama katika maisha na huduma yake.

1: 12-24 Maelezo ya mabadiliko ya safari ya kuwafika kwao

k. 12-14 Paulo alitaka wajue kwa uhakika kwamba yeye ni mtu wa kweli kabisa katika yote atendayo hana hila wala unafiki. Wao hawakupendezwa naye alipoubadili mpango wa kuja kuwaona, na baadhi yao walimshtaki kuwa yeye si mtu wa kweli. Yeye aliwathibitishia kwamba dhamiri yake ilimshuhudia ukweli wake iwapo ni Mungu tu ambaye anaona kwa ndani.

Aliubadili mpango kwa sababu aliamini ni mapenzi ya Mungu kufanya hivyo, pia kwa ajili yao aliwaza ni vema asije kwao wakati ule. Hakupanga mambo yake kwa kutegemea akili zake na kwa busara ya kibinadamu. Wakati wote alitegemea neema na uongozi wa Mungu, akihakikisha mipango yake yote mbele zake. Alijivuna kwamba mambo yake na ya Timotheo yaliweza kuustahimili upelelezi wa Mungu, kwa kuwa walifanya yote kwa neema ya Mungu na kwa nia ya kutaka kumpendeza.

Wakorintho walikuwa wamekwisha kuona jinsi Paulo alivyoishi alipokaa nao kwa muda mrefu na kumtazama kwa ukaribu. Pamoja na hayo, bila shaka Timotheo na Tito waliotumwa kwao waliwaelezea vizuri juu ya sababu zilizomwongoza Paulo kuivunja mipango ya kuwafikia. Hata hivyo, baadhi yao hawakuwa tayari kuyapokea maelezo hayo wakisema kwamba barua zake si za kweli, ni mtu asiyeaminika ambaye ameficha maana na nia yake ya kweli. Paulo alitaka wayaamini maneno yake kama yalivyo, wala wasisome maandishi yake kwa hali ya kutafuta maana iliyofichwa huku yeye hakuficha maana.

Ni dhahiri Paulo alitaka wamwelewe vizuri (1 Kor.5:9-11). Walipokosa kumwelewa vizuri alichukua nafasi ya kusahihisha kuelewa kwao. Pia, kwa msaada wa mafundisho ambayo amekwisha kuwapa waliweza kuelewa maana yake, kwa kuwa hakubadili mafundisho yake, yalidumu kama mapokeo katika makanisa. (2 The.2:15). Ndipo aliongeza jambo jingine kuhusu uthabiti wa dhamiri yake. Aliwakumbusha juu ya siku ya mwisho, siku ya Hukumu. Siku ambayo ukweli wote utadhihirika, na hapo kati, kabla ya siku hiyo, walihitaji kukua katika ufahamu wao.

Alitaka wamwonee fahari, kama yeye naye alivyowaonea fahari hata kiasi cha kuwasifu sana mbele za wengine (2 Kor.7:14; 9:2). Katika Siku ya Hukumu atafurahi sana kuwakiri kuwa waongofu wake, naye alitumaini kwamba katika Siku hiyo wao nao watakuwa na shauku juu yake kama Mtume wao aliyewajulisha Habari Njema za Kristo. Iko sababu moja tu ya kujivuna, nayo ni Injili. Wao ni thibitisho la kazi yake jinsi alivyoutimiza wajibu wake kuwa Mhubiri wa Injili.

Katika sehemu hiyo Paulo aliyajibu mashtaka ya kigeugeu. Wapinzani wa Paulo walidaka jambo dogo na kulikuza kupita kiasi kwa lengo la kuupunguza uzuri wake machoni mwa waumini wa Korintho. Kusudi lao lilikuwa kuutikisa utume wa Paulo na mamlaka yake. Hivyo walionyesha tabia ya kuwa mitume wa uongo. Paulo alikabili jambo hilo kwa upole na hekima. Hakuwanyosha mara moja bali aliwazungumzia kwa kirefu utukufu pamoja na taabu za Huduma ya Kikristo.

Walimshtaki kuwa mtu wa kigeugeu, eti, amebadili mipango yake ya safari, asiwafikie kama alivyoahidi, kwa hiyo ni nani awezaye kutegemea kwamba

hata ule Ujumbe wa Injili hakuubadili. Alikuwa amepanga kuwafikia baada ya kupitia Makedonia na kukaa nao muda wote wa baridi (1 Kor. 16:5-7), halafu kuondoka Korintho na kwenda moja kwa moja mpaka Yerusalemu. Alibadili akikusudia kuwafikia kwa muda mfupi, ndipo aende Makedonia, halafu arudi kwao. Kwa hiyo alitazamia kuwafikia mara mbili - labda ndiyo maana ya “baraka mbili” za k.15.

Lakini ilimbidi hata mpango huo aubadili akiwaza kutoka Efeso moja kwa moja mpaka Korontho ndipo aende Makedonia, Twajua ilimpasa kuonana na WaMakedonia, ila hakusema sababu yake 2 Kor.7 na Mdo.20:2. Kwa kufanya hivyo ataweza kupima maendeleo ya lile changizo kwa makanisa maskini ya Uyahudi na Yerusalemu. Atakapofahamu kwa usahihi maendeleo hayo ataweza kufanya mpango halisi wa kulipeleka changizo. Alishtakiwa kuwa anapanga mipango kwa urahisi bila kuwaza kwa kina. Alikataa mashtaka hayo akionyesha kwamba hata mipango yake yote hupangwa kwa uangalifu sana, hata ile iliyombidi aibadili ilipangwa kwa uangalifu, na wakati wote alitafuta kufanya mapenzi ya Mungu kwa kila jambo. Kama ni hivyo, na amepanga kwa uangalifu sana, kwa nini imetokea kwamba imempasa aibadili? Paulo aliona ya kuwa kama atashindwa kuibadili mipango yake atakuwa mtu wa shingo ngumu. Kwa vyovyote budi awe tayari kufanya mabadiliko kama hali zikitokea zitakapohitaji afanye hivyo. Hata Injili iliwafikia mwanzoni kwa sababu ya utayari wa kubadili mpango wake alipoongozwa kufanya hivyo (Mdo.16:6,7; 1 The.2:18).

k.18 Lakini huo utayari wa Paulo kuibadili mipango ya safari Je! ni dalili ya kuwa hata Ujumbe wa Injili aweza kuubadili? La! hata kidogo! Mipango ni ya Paulo, ni ya ki-binadamu, ambayo yaweza kubadilishwa. Injili ni tofauti, ni Injili ya Mungu, na Mungu hawezi kuibadili: Neno Lake ladumu milele. Tena, ujumbe wa Injili ni Habari Njema za Matendo makuu ambayo Mungu amefanya kwa njia ya Yesu Kristo, na matendo hayo yamekwisha kutendeka ki-historia, hayana mabadiliko, yaliyotendeka yametendeka, basi.

k.19 Ujumbe wa Injili umekazwa katika Kristo, hautikisiki, na Kristo ni Njia, na Kweli, na Uzima (Yn.14:6). Paulo alipofika Korintho alikuja ili amhubiri Kristo (1 Kor.2:2) na wale waliokuja pamoja naye, pia walimhubiri Kristo. Hakuna uwezekano wa kuubadili Ujumbe wa Injili.

k.20 Mungu alitoa ahadi nyingi kumhusu Kristo, na zote zimetimizwa na Kristo. Hizo ahadi zilipata ukweli wao katika Kristo, nazo zatufikia kwa njia ya Kristo. Inayotubakia ni kuzipokea kwa kumwamini Kristo. Kwa kuwako kwa ahadi ni wazi kwamba ni Mungu atakayetuwezesha kuzikubali, bila msaada wa Mungu hatuwezi kuzipokea, ila kwa sababu ni ahadi za Mungu zina nguvu za kutuvuta kuzipokea. “Amina” ni itikio letu la kuziamini, imani hiyo inazalishwa na Kristo aliye ndani yetu. Kwa hiyo utukufu wote una Mungu.

“kwa njia yetu”. Mungu aliwateua Paulo na wenzake wawaletee Wakorintho ujumbe wa Injili. Hawakupanga kufanya hivyo, ila ni Mungu aliyewaongoza, na kwa kuufuata uongozi wa Mungu ilimbidi Paulo aibadili mipango yake. Tena alikuwa amekazana sana katika kuwaletea Injili, alifanya bila kujali wale waliomshtaki kuwa na kigeugeu.

Alimpa Mungu utukufu na sifa kwa jambo hilo, maana ni Mungu aliyemwimarisha, yeye mwenyewe asingaliweza kuwa imara bila msaada wa Mungu. Kipawa hicho si chake tu, hata wao pia wanacho, maana wote wamo ndani ya Kristo na wote wameungana na Kristo. Wamepewa Roho Mtakatifu, yule yule ambaye Kristo alikuwa naye. Mungu ametutia muhuri na kututia alama ya kuwa Wake. Kutiwa muhuri ni ishara ya tabia ya Mungu ya kutuangalia kwa hali ya kibinafsi na nia yake ni kutusaidia katika kila jambo la maisha yetu.

Waumini wa Korintho walipaswa wasiwasikilize wale wenye kusudi la kuwadanganya. Afadhali wamsikilize Mungu pamoja na wale walio Wake waliotiwa muhuri yake. Mungu ametupa arabuni, yaani, kipawa cha Roho ili aishi mioyoni mwetu. Ni kazi ya Roho kututia nguvu, na kutuimarisha, na kutufanya tuzae matunda, na kukua mpaka tumekamilika.

Ikiwa Paulo alimhubiri Mungu kuwa yule awezaye kutegemewa kabisa, ilimpasa na yeye mtumishi wake kufanana na Mungu huyo na kuwa mtu wa kutegemewa.

k. 23-24 Paulo alionyesha kwamba aliipanga mipango yake kwa kuwaza manufaa ya wengine, na ikiwa ilimbidi aibadili, lazima iwepo sababu ya kutosha. Kwa hiyo, ni kwa sababu gani alikuwa ameibadili safari ya kuja kwao? Sababu kubwa ilikuwa mzigo alio nao kwa ajili yao. Hakutaka kuongeza huzuni yao na aibu yao. Kwanza wayatengeneze mambo kadha, na kwa kuahirisha safari, alikuwa akiwapa nafasi ya kuyatengeneza makosa yao. Kwa njia hiyo watakua kiroho na furaha yao itazidi, na imani yao itatiwa nguvu. Yafaa zaidi wao wenyewe kuwarudi wenye makosa, hali wakijua Paulo na wenzake wanawaunga mkono kwa njia ya maombi na mashauri, kwa sababu hakuwa na shabaha ya kuitawala imani yao ila alitaka kuwasaidia waishi kama ilivyowapasa.

2: 1-4 <u>Barua kali</u>

Katika kifungu cha kwanza Paulo alitaja safari ambayo imekwisha kufanyika. Wengine huwaza safari hiyo ilitokea hata kabla ya kuandikwa kwa Waraka wa kwanza, nayo ililihusu changizo (2 Kor.8:10; 9:2). Ila wengi huwaza kwamba alikuwa amewafikia hivi karibuni. Alipata shida kubwa ya kuaibishwa na kuumizwa sana. Ndipo mbele za Mungu alikata shauri kwamba hatawarudia. Hakuwa na maana kwamba hatawarudia kamwe ila hatawafikia tena kwa hali

ya yeye kuumizwa sana na wao kuhuzunishwa. Katika 1 Kor.4:21 Paulo alitambua kwamba itambidi kuwa mkali atakapowafikia kwa sababu wengine wangali wakiridhiana na mabaya bila kuwa na nia ya kuyatengeneza. Akienda atawaamuru kwa nguvu, ila zaidi alipenda kuwasubiri na kuwapa nafasi ya kujirekebisha. Akifika kwao na kukuta mambo hayawi sawa atakuwa hana njia isipokuwa kuwakemea kwa wazi na kuwalazimisha kusawazisha mambo, nao watasikia aibu na huzuni. Paulo amefungamana nao sana na ni wao walioweza kuamsha furaha ndani yake, ile furaha inayosababishwa na itikio lao kwa Injili maishani mwao. Twaona Paulo alitawaliwa na kitu kimoja, itikio lao kwa Kristo (1 Kor.2:2). Kama watakosa kuitika vema na kuyatengeneza mambo, hakuna kitu kingine kitakachomfanya afurahi. Kwa hiyo, badala ya kwenda kwao tena alikuwa amewaandikia barua kali kwa shabaha ya kuwasaidia na kuwahimiza kutengeneza hayo mambo. Baadhi ya watalaamu huwaza barua kali ni Waraka wa kwanza lakini ni vigumu kufikiri hivyo, kwa jinsi inavyotajwa na Paulo katika sura ya pili, tena Waraka wa kwanza hauwi mkali. Hivyo imewazwa kuwa barua iliyokwenda hivi karibuni kwa mkono wa Tito.

k.4 Paulo aliiandika barua hiyo kali akiwa na hali nzito, alisema aliandika kwa machozi na masumbufu ya rohoni. Hakuwa na shabaha ya kuwaumiza. Aliwapenda sana na kutokana na upendo wake alisikia mzigo sana juu yao. Alitaka kuwajenga katika imani yao hali akifahamu kabisa kwamba uheri wao wote kiroho huutegemea utii wao kwa Kristo. Upendo wa namna hiyo unasumbua wale ambao hawawi tayari kuupokea. Upendo wa kweli ni tayari kukemea kwa kusudi la kupona, tena upendo wa kweli huwa tayari kuvumilia kutoelewekwa vizuri. Mara hao Wakorintho watakapotambua ni upendo unaomsukuma asiwafikie mara, ndipo wataweza kutokujali mashtaka ya wateta wake.

2:5-11 <u>Wamsamehe yule mtu aliyemwudhi Paulo</u>

Kutokana na sehemu hiyo twajifunza ni mtu mmoja aliyeongoza na kuchochea jambo la kumpinga Paulo. Wengine wamewaza ya kuwa ni yule aliyetajwa katika 1 Kor.5:1. Huyo mtu alikuwa amefanya uasherati wa hali ya juu, hata kuzidi wapagani. Lakini huenda si huyo. Iliyo wazi ni kwamba kosa la huyo mtu hasa ni katika kuongoza upinzani wa kumpinga Paulo alipokuwa kwao (k.5, 10) na zaidi ya kumpinga akaruka mpaka akimwaibisha na kumshusha, asimpe heshima akiidharau mamlaka yake, tena, mbele za waumini, hata Paulo akaumizwa sana moyoni mwake.

Pamoja na kumwumiza Paulo, tendo hilo liliwagusa waumini wa Korintho. Katika barua kali alikuwa amewaomba wamwadhibu huyo mtu ili apate kuupima utii wao kwa mamlaka yake ya Ki-Mitume. Mara alipofahamu wamemtii na yule mtu kweli ameadhibiwa, basi, shabaha yake ilitimizwa.

Baada ya kushauriwa na Paulo wakamwadhibu huyo mtu, hata wengine walizidi mpaka. Paulo hakutaka waendelee kumkemea, iliyohitajika ni kumtia moyo na kumfariji. maana alikuwa ametubu na adhabu aliyopewa ilitosha. Ahakikishiwe msamaha na kuonja neema ya Mungu na faraja ya Injili kusudi asimezwe na huzuni na kukata tamaa hata kiasi cha kufikiri hawezi kusamehewa na kurudishwa kwenye jamii ya waumini na kupokelewa nao kwa moyo. Ni wajibu wa jamii ya Wakristo wa pale kumwonyesha upendo, na kwa njia hiyo wataudhihirisha utii wao kwa Injili, si utii kwa Paulo tu. Katika 1:24 alisema kwamba hakutaka kutawala imani yao. Pasipo kukubaliana juu ya jambo hilo walikuwa katika hatari ya kufarakana, wengine kuwa wakali, wengine kuwa walegevu.

k.10 Paulo mwenyewe alijiunga nao katika kumsamehe, iwapo alikuwa ameumizwa sana. Hakutaka kuendelea kumwaza vibaya. Neno la kutengwa na jamii ya waumini au kurudishwa katika jamii ya waumini, yapaswa lifanywe katika “undugu” kama wajumbe wa Kristo na katika Jina lake.

k.11 Shetani hujishughulisha sana ili apate njia ya kupenya shirika za Kikristo. Tunapoacha kukemea makosa Shetani hupata nafasi. Vilevile tunapokemea kwa ukali na kwa hali ya sheria Shetani hufaidi; na tunapokataa kutoa msamaha kwa mkosaji hali ametubu kosa lake basi Shetani hushangilia sana.

Paulo alishauri: “Shetani asipate nafasi juu yetu”. Sote tumepokea msamaha kutoka kwa Kristo, na twapaswa kutoa msamaha kwa wengine. Shetani hutafuta njia ya kuwafanya wakosaji wakate tamaa na kuhuzunika kupita kiasi. Pia tusipotahadhari ni rahisi kwa Wakristo kugombana juu ya namna ya adhabu ya kutolewa.

2:12-17 <u>Ushindi wa Injili</u>

Twautambua mzigo wa Paulo kwa hao Wakorintho tunapotazama hali yake alipomsubiri Tito pale Troa. Nafasi tele za kuhubiri Injili zilikuwepo. Bwana alikuwa amemtangulia na kumfungulia mlango wazi kwa Injili.

Lakini Paulo alifanyaje? Je! alizitumia nafasi hizo? La! Badala ya kutulia na kuihubiri Injili hadi atakapofika Tito, maana mpango wao ulikuwa wakutane pale; Paulo aliamua kuvuka mpaka Makedonia na kumwahi huko. Ni dhahiri mambo ya Wakorintho yalitawala mawazo yake. Alihofu sana huenda hali ya Wakorintho si nzuri, na Tito ameshindwa kuwasaidia.

Kama Kanisa la Korintho likirudi nyuma, je! itakuwaje katika makanisa mengine walio na wapinzani mbalimbali? Tena, itakuwaje mipango ya kupeleka Injili mahali papya, hata mpaka Rumi? Kwa hiyo katika mawazo yake jambo la maana ni maendeleo mazuri ya Kanisa la Korintho.

Hivyo, Paulo aliondoka Troa, akaenda mpaka Makedonia, akiwa na shauku kubwa ya kumwona Tito na kupata habari za Wakristo wa Korintho. Ni kweli kabisa Paulo alikuwa na mzigo juu yao. Kwa upande wao, itikio lao kwa mzigo na upendo huo, ni katika wao kuwa tayari kumtetea ili wamtie nguvu na moyo wa kuendelea katika uenezi wa Injili badala ya kunyonya nguvu zake kwa mateta. Pia, watambue ya kuwa yanayotokea kwao hugusa hata na makanisa mengine na ndugu zao katika Kristo mahali pengi, na kwa jumla kazi zote za Injili.

Bila shaka haikuwa rahisi kwa Paulo kuondoka Troa, huenda alifikiri ni Shetani aliyesababisha afanye hivyo, maana amemtaja hapo juu. Ila si udhaifu, wala si kwa kushindwa, kwa sababu alipotaja mambo hayo aliingia hali ya kumsifu sana Mungu, na aliona jinsi Kristo anavyoongoza watumishi wake katika ushindi wa Injili kotekote ulimwenguni. Tito alileta habari njema kutoka Korintho, na Paulo alijifananisha na jemadari aliyeshinda vitani. Siku zile baada ya jeshi kushinda vitani na maaskari kurudi Jemadari Mkuu hali amevaa taji ya maua na kushangiliwa na watu, aliongoza maandamano makubwa wakipitia mjini na viunga vyake. Watu waliotekwa walitembezwa mjini ili watu wawatazame. Lakini ushindi wa Paulo na wenzake si ushindi wao bali ni Ushindi wa Kristo na Injili, ambao wao wameshirikishwa hali wakiwa wahudumu na watumishi wake. Iwapo vilikuwako vipingamizi vingi, hata hivyo, kazi ya Injili iliendelea. Katika kazi hiyo Mungu aliwatumia. Alifananisha ujuzi wa kumjua Kristo kuwa harufu nzuri, mfano wa manukato.

k.15 Ila ujuzi huo wa kumjua Kristo baadhi ya watu waliukataa na kwao harufu haikuwa ya manukato bali ya mauti. Injili yasema juu ya Uzima, ni mwongozo kwa watu ili waupate. Uzima kwa njia ya kumwamini Kristo, ila kwa wale wanaokataa kuamini ni sababu ya Mauti. Kristo ndiye manukato, na wahubiri wa Injili yake ni manukato ya Kristo. Mungu hupendezwa nao, potelea mbali watu wakiipokea au wakiikataa Injili yenyewe. Injili hushinda sikuzote, maana nje yake hamna wokovu, na wote ambao huzitegemea juhudi zao kwa kupata wokovu hupotea, na kushindwa kwao ni dhihirisho wazi kwamba ni Injili tu, peke yake, iliyo na nguvu ya kuokoa na ushindi wa ki-maisha.

Kwa sababu ya matokeo makuu yanayosababishwa na Injili, makubwa ambayo ni Uzima na Mauti, basi ni wazi ya kuwa anayeihubiri Injili hawezi kazi hiyo bila neema ya Mungu. Injili si kitu kama vitu ambavyo mtu hufanya biashara navyo. Wajumbe wa Injili hawawezi kutumia hila au ujanja, wala ushawishi na mbinu za ki-dunia. Hawawezi kujitafutia faida, imewapasa uaminifu wa hali ya juu na kujitoa kwa kweli.

Katika siku za Paulo wengine walipunguza sehemu sehemu za ujumbe, wakiacha kutaja au kueleza magumu yaliyomo katika kumfuata Kristo. Wengine walichanganya habari za Injili na mawazo yao ya kibinadamu,

wakitegemea hekima za kibinadamu. Hata baadhi ya waumini wa Korintho walikuwa wa aina hiyo. Na mpaka leo wako wa hali hiyo.

Baada ya kuzungumzia hayo Paulo aliuliza swali gumu “ni nani atoshaye mambo hayo?” Alitaka wawaze kwa kina juu ya Huduma na Utumishi wa Kristo. Ni hali zipi zilizotakiwa kwa kazi hiyo? Ni kwa njia gani watumishi wanyonge, wenye kutetwa vibaya na kwa uongo, wawezao kusababisha matokeo makubwa ya makanisa kupandwa na waumini kupatikana, na Wakristo kuishi maisha mazuri kuliko wenzao?

Paulo alitoa jibu kwa swali lake. Kwanza watumishi wa Kristo wakwepa kosa la kulitumia Neno la Mungu kwa ujanja na hila. Waseme kweli tupu, kweli iliyo wazi, kusudi watu waifahamu vizuri na kujua ni kweli hasa. Kweli itakavyoweza kupimwa na kudhihirika kuwa kweli.

Pili, waseme kama wako “mbele za Mungu” waseme yale ambayo Mungu hupenda wayaseme. Tatu, waseme hali wakitambua “Kuwako kwa Mungu” na kwa kumtegemea. Nne, waseme “katika Kristo” yaani yote wasemayo yamhusu Kristo.

Wakati wote Paulo alikuwa na dhamiri safi juu ya nia na sababu zake za ndani. Hakuogopa kumwita Mungu awe shahidi.

3:1-6 <u>Wao ni barua iliyoandikwa na Roho</u>

Bila shaka wengine walifikiri kwamba Paulo alikuwa akijisifu, ni kama aliandika barua ya sifa zake, hasa kwa jinsi alivyosema katika sehemu ya mwisho ya sura ya pili kuhusu kuongozwa katika ushindi.

Wakristo waliosafiri huko na huko walikwenda na barua za sifa ili shirika za Kikristo zilindwe na mitume na manabii wa uongo. Paulo hakuwa na maana ya kuwa barua hizo ni mbaya au ya kuwa hazikutakiwa (Mdo.18:27; Ru.16:1).

Paulo na wenzake hawakuzihitaji barua za namna hiyo, maana wao hawakuwa wageni kwa Wakorintho. Kutokana na kazi walizofanya na matokeo yake, Wakorintho walipata kuwafahamu vizuri. Kwa njia yao walikuwa wameletwa katika shirika la Kikristo na katika Kristo wameungana nao. Kwa hiyo, Je! kweli walihitaji barua? Eti! wamesahau jinsi Paulo na wenzake walivyo? Kweli kabisa, hawana haja ya barua ya kuwaelezea! Hata watu wa mbali walimfahamu Paulo na hali yake, maana habari za kazi yake zilikuwa zimefika mbali.

k.2 Katika kifungu hicho Paulo amekaza sana kwamba Wakristo wa Korintho ndio hasa barua yake. Daima, wamo moyoni mwake na mawazoni mwake, na matendo yake yaliudhihirisha mzigo alio nao hata ukawa wazi kwa kila mtu.

Halafu alisema kwamba wao ni “barua ya Kristo” iliyoandikwa na Roho Mtakatifu. Walikuwa wamejaliwa kupata uhai mpya katika Kristo, walizaliwa upya na Roho na maisha yao yote yaliguswa na kubadilika. Iwapo walikuwa na udhaifu mwingi na makosa mengi hata hivyo, hakika walikuwa na “uhai mpya”. Na chanzo cha hayo yote ni katika Paulo kufika kwao na kuhubiri Injili. Hahitaji barua ya kwenda kwao au ya kutoka kwao. Anapozungumzia matokeo ya Huduma yake hakutafuta asifiwe na watu, bali alikuwa akiwakumbusha hali ya huduma aliyo nayo.

Maneno ya “wino” na “Roho” na “vibao vya mawe” na “vibao vya moyo” ni ukumbusho wa tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Ni ukumbusho wa maneno ya Yeremia 31:33 aliyetoa unabii juu ya Agano Jipya, pia maneno ya Ezekieli 11:19; 36:26 kuhusu ahadi ya moyo mpya badala ya moyo wa jiwe. Ndipo alirudia swali kuhusu “utoshelevu” kwa huduma ya aina hiyo. Paulo alijua hakika kabisa kwamba yeye hakuwa na cho chote cha kuchangia kwa utoshelevu huo. Kweli alikuwa na akili kali, na nia iliyokazwa kwa nguvu; ila huo utoshelevu hautokani na vitu hivi. Yote hutoka kwa Mungu. Wao ni wahudumu wa “Agano Jipya”; Agano lenye upande mmoja hasa; Agano lililoanzishwa na upande mmoja; na kutekelezwa na huo upande mmoja; yaani upande wa Mungu. Agano Jipya ni Agano la Roho wa Uzima. Wakristo wa Korintho ni ushuhuda kwa Huduma ya Roho na kwa Agano Jipya lililoletwa na Mungu. Kristo ni kiini chake, akiwa Mwanzilizi na Mtekelezaji wake. Ni Kristo aliyekufa ili awe Mpatanishi, kusudi Agano lisimamishwe. Paulo na wenzake walikuwa waleta habari tu, nao waliwezeshwa na Mungu aliyewaita na kuwafanya kuwa wahudumu wa Agano Jipya. Agano hilo la Roho linahitaji watu waliojaa Roho kulihudumia maana ni hao tu watakaoweza kulihudumia vema.

3:7-18 <u>Tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya</u>

Paulo aliendelea kwa kulinganisha Agano la Kale na Agano Jipya. Maagano yote mawili yalikuwa matukufu, hata hivyo, utukufu wao ulitofautiana sana. Agano la Kale lilikuwa Agano la sheria na kwa sababu hiyo lilikuwa huduma ya mauti. Agano Jipya ni Agano la uzima kwa hiyo ni huduma ya Roho. Hasa Paulo alitumia maneno “mauti” na “uzima” kueleza uhusiano kati ya Mungu na wanadamu. Kuwa na “uzima” ni kuwa katika uhusiano mwema na Mungu; kuwa na “mauti” ni kukosa uhusiano mwema na Mungu na kuwa mbali na chemchemi ya uzima.

Tena, Agano la Kale lilikuwa huduma ya adhabu, kwa sababu Sheria humwachilia mtu tu maadamu ameitimiza. Lakini wote ni wenye dhambi, wala hakuna awezaye kuitimiza Sheria kwa ukamilifu. Ila Agano Jipya ni Huduma ya kuleta haki, yaani, kumleta mtu katika uhusiano mwema wa Mungu, iwapo ni mwenye dhambi. Hilo lawezekana kwa sababu madai ya sheria yametimizwa na Kristo ambaye hakuwa na dhambi, hata hivyo alikubali kutwishwa dhambi za wote na kuchukua katika mwili wake adhabu yake (1 Pet.2:24; 3:18).

Agano la Kale lilikuwa na utukufu, na huo utukufu ulikuwa wa kweli. Ulionekana wakati Agano lilipotolewa katika Mlima Sinai, hata Musa alifunikwa huo utukufu, uso wake uling"aa kiasi cha kumpasa avae taji. Lakini hakuwa na huo utukufu kwa asili nao ukatoweka baadaye. Kwa nini utukufu huo ulionekana kwa muda? Ni kwa sababu Agano hilo lilitolewa na Mungu, nalo lilionyesha tabia ya Mungu ya kuwa mwenye haki na mtakatifu, na mapenzi yake ya kutaka watu wafanane naye. Halikuwa la kudumu, kwa sababu, mara lilipotimiza shabaha iliyokusudiwa na Mungu likaondolewa.

Halikuwa neno kamili na la mwisho kutoka kwa Mungu. Liliwatazamisha watu kwa lile litakalolifuata baadaye, lile bora, yaani, Agano Jipya na Huduma ya Roho. Roho hufanya kazi iliyo bora zaidi, Roho huleta mtu kwenye uhusiano mwema na Mungu, mtu huhesabiwa haki kwa kazi ya upatanisho wa Kristo uliofanyika Msalabani. Mtu hupewa haki bure, kwa neema, kwa njia ya kumwamini Kristo, ndipo mtu aweza kuishi katika hali ya kuwa amekubalika na Mungu (Rm.3:22; 1 Kor. 1: 30, 2 Kor.5:21). Hayo ndiyo tofauti kubwa kati ya Maagano hayo mawili, na tofauti hiyo kubwa hufanya lile Agano la Kale kuwa kama halina utukufu.

Utukufu wa Agano Jipya ni katika asili yake na mfumo wake; nao utadumu kwa sababu matokeo ya Agano hilo katika maisha ya watu ni ya kudumu.

k.12 Paulo alikuwa akiishi chini ya hilo Agano Jipya, pia alikuwa Mhudumu wake, naye alikiri ya kuwa yote yaliyomo katika Agano hilo hayajadhihirika bado, yamebaki matimizo ya mwisho. Alitumia neno “faraja”, faraja yenye uhakika. Hakuwa na wasiwasi wala hakusitasita juu yake. Kazi yake ilikuwa kuhubiri Injili kwa ujasiri, na kwa wazi, bila hofu.

k.13 Alitofautiana sana na Musa, aliyekuwa Mhudumu wa Agano la Kale. Musa alishughulikia vivuli na mifano, ukweli uliofichwafichwa na kufunikwakufunikwa. Kwa nini Musa alijivika taji usoni? Yawezekana alijivika taji usoni ili watu wasione ya kuwa ule utukufu aliokuwa nao ulikuwa ukipungua. Au, pengine taji lilifundisha kwamba ule utukufu hautaendelea utakapofika wakati wa kazi ya Torati kutimizwa. Kwa hiyo, huduma ya Musa na Paulo ilitofautiana sana. Paulo hakuwa na haja ya kuvaa taji, yeye aliweza kusema waziwazi na kwa uhuru wakati wote. Huduma la Musa la Agano la Kale lilikuwa la matayarisho, la kuwatazamisha watu kwa Agano Jipya litakaloingizwa baadaye, Agano bora lenye ahadi bora na uwezo bora. Katika Agano Jipya Mungu ametoa Neno lake la mwisho, nalo hilo Agano Jipya litadumu.

k.14-15 Hata Wayahudi katika siku za Paulo walikuwa vipofu, walishindwa kumtambua Kristo na kukubali kwambe Yeye ndiye Timizo la Agano la Kale. Waliendelea kusoma Agano la Kale katika hali ya kufikiri kwamba Torati ilikuwa neno la mwisho kutoka kwa Mungu. Ila kweli ni kwamba Kristo

aliliondoa lile taji kwa kuitimiza Torati kwa ukamilifu. Wao waliendelea kuvaa taji, taji ambalo wamelifuma wenyewe, taji lililowazuia wasiutambue ukweli, kwa kuwa akili zao zilitiwa giza.

k.16 Musa alipofika “mbele za Bwana” aliliondoa taji, kielelezo cha kuonyesha kwamba alipoacha kuitegemea Torati kwa kupata haki, aliweza kushirikiana na Mungu kwa ukaribu kuliko Waisraeli wenzake. Vilevile, Myahudi ye yote atakapoacha kuitegemea Torati kuwa njia ya kupata haki, na kumgeukia Bwana Yesu na kuutegemea upatanisho uliofanyika na Yesu Msalabani, basi huyo pia ataondelewa taji. Ki-binafsi atakutana na Yesu, na hii ni ishara kwamba yote yaliyokuwa kati yake na Mungu yameondolewa.
Bwana Yesu ni Masihi aliyeahidiwa, na katika Yeye, vivuli vyote na mifano yote ya Agano la Kale vimetimizwa. Ni Yeye Aliye na Roho Mtakatifu, na kwa njia ya Roho mtu ye yote, wa mahali po pote, na wa wakati wo wote, aweza kumpokea Kristo na kuzifaidi kazi za ukombozi na upatanisho alizozifanya. Yesu hakuwa mtu tu, aliyekufa, bali pia alikuwa Mungu Mwana. Yesu na Roho ni wamoja kwa maana ile ile ya Baba na Mwana kuwa ni wamoja (Yn.10:30; 16:14). Roho ni “Roho wa Kristo”. Alipo Kristo kuna uhuru wa kila aina. Uhuru mbali na Torati Gal.5:18; uhuru mbali na hofu Rum.8:15; uhuru mbali na dhambi Rum.7:6; Uhuru mbali na uharibifu Rumi 8:21, 23. Hata mtumwa anayeokolewa na Kristo huufurahia kabisa uhuru wa kuwa mtoto wa Mungu, uhuru mtukufu.

k.18 Ni Wakristo wote, si mitume tu, walio na “nyuso zisizotiwa taji”. Waweza kumkaribia Mungu kwa ujasiri bila kizuizi, na siku kwa siku wabadilishwa na Roho anayewahuisha. Kwa kumtazama Kristo, Mkristo hugeuzwa afanane zaidi na zaidi na Kristo Mwenyewe. Utukufu wa Agano Jipya ni utukufu unaotuhuisha, twaukolea huo utukufu na tokeo lake ni kwamba sisi pia twakutukuzwa.

MASWALI:

1:1-11Kwa nini Paulo alianza Waraka kwa kusema mengi kuhusu “faraja ya Mungu”?
Paulo alipata msaada gani kutokana na faraja hiyo?
Tunajuaje kwa hakika kwamba Mungu ni Baba wa rehema?
Mateso, dhiki, shida n.k. vina sehemu gani katika maisha ya Mkristo na ni dalili ya nini?
Siku hizo Wakristo hupatwa na mashinikizo na mashurutisho gani yanayowapasa kuwa na tahadhari nayo? Eleza

1:12-24Ni neno gani lililowasumbua Wakorintho na kuleta shida katika uhusiano wao na Paulo?
Ni watu gani waliodaka neno hilo na kulikuza, na kwa nini walifanya hivyo?

Ni nini dalili za uaminifu wa kutegemewa na msimamo mzuri kwa waumini?
Kwa mfano, Wakristo wafanye nini mahali ambapo ni kawaida kwa watu kutoa au kupokea rushwa?

2:1-11 Kwa nini Paulo aliwaandikia barua kali?
Katika barua hiyo aliwaagiza kufanya nini? Je! walimtii?
Shetani hujitahidi kufanya nini kuhusu sharika za Kikristo?
Atafaulu kwa njia gani? atashindwa kwa njia gani?

3:1-6 Kwa nini Wakorintho hawakuhitaji barua ya sifa juu ya Paulo?
Paulo alipotumia maneno "barua ya Kristo" na "iliyoandikwa na Roho" alikuwa akisema kuwahusu watu gani, na alikuwa na maana gani?

3:7-18 Eleza tofauti kubwa kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Musa na Paulo walitofautiana katika mambo gani na kwa njia zipi?

SURA YA 4:1 - 5:10 UTUKUFU NA UGUMU WA UTUMISHI WA INJILI

4: 1-6 <u>Paulo ni mhudumu wa Agano Jipya</u>

Paulo na wenzake walifanywa kuwa wahudumu wa Agano Jipya kwa huruma za Mungu tu. Hawakustahili kuwa wahudumu wala hawakufanya lo lote lililowastahilisha. Walizipokea "rehema" za Mungu. Mungu alikuwa amewahurumia katika unyonge wao.

Huduma hiyo ni ya ajabu sana, na uzuri wake ulizidi zaidi sana shida zote na ugumu wote waliopata katika utumishi huo. Kwa hiyo hawakuweza kuruhusu jinsi walivyojisikia pamoja na ukosefu katika maitikio ya watu, wala upinzani wa adui zao kubadili mawazo yao juu ya huduma hiyo. Wataendelea kwa bidii, bila kukata tamaa, na bila kulegea. Watakubali wajibu zake zote kwa ushujaa na kufanya yote kwa wazi. Wamekaza nia zao kufanya hivyo. Wameacha njia zote za hila na ujanja katika kuitangaza Injili; hawatatumia maneno ya mapambo, wala maneno ya juujuu; wala mbinu zozote zisizofaa katika kuwavuta watu. Hawatachanganya kweli na uongo wala hawataongeza wala kupunguza neno lolote la kweli. Hawatatumia lugha isiyoeleweka itakayowapatia watu nafasi ya kujificha au kuwa na udhuru au kukawia kuipokea Injili. Hivyo, walikata shauri kuihubiri kweli ya Injili kwa wazi na bila maficho, kusudi Injili ipate kuzigusa dhamiri za watu, na wale wenye kushtakiwa na dhamiri zao watatubu kweli na kupata amani rohoni. Alisema kwamba wanafanya yote "mbele za Mungu"; hawakuogopa kumwita Mungu awe shahidi wa mambo yao.

k.3 Kama ni hivyo, walikuwa na haki kutazamia kwamba watu wataitika vema wito wa kumwamini Kristo. Kumbe! sivyo. Badala ya maitikio mazuri wengi hawakujali hata na wengine waliupinga vikali.

k.4: Lakini hitilafu si katika Injili wala katika wahudumu. Iliyopo ni kwamba watu walichagua kubaki katika njia ya upotevu. Walimkubali Shetani, adui wa Yesu, badala ya Yesu mwenye uwezo wa kuwaokoa na kuwaweka huru mbali na utawala wa Shetani.

Paulo alimtaja Shetani kwa kumwita “mungu wa ulimwengu huu”. Lugha hiyo hutuelekeza kuwaza juu ya nguvu na utawala wa Shetani, na kuonyesha kwamba wako watu walio tayari kujitia chini yake. Ila kweli ni kwamba hana nguvu juu yao wala hawezi kuwatawala kinyume cha wao kutaka. Hali hiyo imetokea kwa sababu watu wamedanganywa na Shetani, wameziamini uongo zake, naye amewapofusha macho ili wasiutambue ukweli, hata mwanga wa Injili usiwatie nuru mioyoni mwao. Ila si wote waliodanganywa na kupofushwa macho.

k.5 Kama Paulo na wenzake walikuwa wangali wakitafuta faida zao wenyewe katika kazi hiyo wangalikata tamaa zamani. Kazi yao ilikuwa kumtangaza Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha. Walimtangaza Kristo kuwa Mleta Amani na Mleta Matumaini. Waliwahakikishia watu hali yao halisi mbele za Mungu. Hawakufanana na wanafalsafa waliotoa hekima yao na majibu yao. Walikuwa radhi kumtangaza Kristo kuwa Bwana. Hawakuwa na uchaguzi katika jambo hilo, maana ni Kristo aliyewaongoza na kuwaagiza, na wao kwa upande wao walikuwa tayari kufanya mapenzi ya Kristo kwa moyo na kwa uwezo wao wote. Walikuwa “watumwa” wa Wakorintho, si katika maana ya kuwa “mali” yao, ila katika maana ya kuwa walifanya kazi kwa ajili yao wakitafuta ote yatakayowafaidia kiroho. Walifanya kwa ajili ya Kristo, na hasa kwa sababu ya tendo kuu la Yesu kuwafia wao wote Msalabani.

k.6 Katika kifungu hiki Paulo alitaja kazi ya Mungu katika uumbaji. Kwa agizo la Mungu, nuru, ambayo haikuwepo, ilitokea na kumulika ulimwenguni. Ila sasa, Mungu hufanya kazi ya ajabu zaidi, anaondoa giza la rohoni, na kuwamulikia watu ndani ya mioyo yao kwa Kristo kuishi ndani yao, kwa njia ya Roho Mtakatifu. Mungu ni Mungu wa Nuru, na nuru hiyo, yaani, ujuzi wa Injili, si habari kadha za kushikwa kichwani bali ni ujuzi wa kibinafsi.

Katika huduma ya aina hiyo Je! watachoka? Hata ikiwa watu watakosa kuitikia vema? Je! watumie ujanja ili wavute watu? La, hata kidogo, wala hawatalegea, wala kukata tamaa, kwa sababu huduma hiyo ni ya maana sana, nayo ina utukufu mwingi.

4:7-18 <u>Unyonge wa Wajumbe na Nguvu ya Mungu na Ujumbe wake</u>

Katika sehemu hiyo Paulo alilinganisha “hazina” yaani Ujumbe wa Injili na udhaifu wa Wajumbe wake. Alipima dhiki na mateso waliyokuwa wakiyapata katika maisha ya kuwa wahudumu wa Injili katika maana ya huduma hiyo. Kuujua Utukufu wa Mungu katika Uso wa Yesu Kristo na kuitwa kuueneza ujuzi huo walihesabu ni hazina ipitayo hazina zote. Lakini hiyo “hazina” huhitaji chombo cha kuitunzia, na bila shaka kwa sababu ya uzuri wa hazina ingefikiriwa kwamba vyombo vyake pia vingekuwa vizuri kusudi hazina yenyewe iheshimiwe vema. Lakini ajabu ni kwamba Mungu amefanya kinyume cha mawazo hayo. Amewachagua wajumbe ambao ni vyombo dhaifu, visivyo na uzuri na ametia ndani yao ujumbe wa Injili, ambayo ni hazina kuu. Injili imekabidhiwa mikononi mwa watu wanyonge, wenye udhaifu mbalimbali, watu wa dunia hii, wenye mipaka katika uwezo wao. Ni kama kuweka lulu au mito ya ghali sana katika bahasha ya karatasi tu!!

Kwa nini Mungu amefanya hivyo? Ili idhihirike wazi kwamba Injii haikubunwa na mwanadamu awaye yote, wala haikuundwa hapa duniani, bali ni Ufunuo wa Mungu. Kama hazina hiyo ingewekwa katika vyombo vizuri na vya nguvu, basi ingekuwa rahisi kwa sehemu ya sifa iende kwa vile vyombo na sehemu iende kwa hazina, badala ya sifa zote ziende kwa hazina tu. Lakini kwa sababu ni wazi kwamba vyombo ni dhaifu na vinakosa uzuri, basi “hazina” huonekana wazi kuwa nzuri sana yenye nguvu. Paulo alijifunza neno hilo kwa njia ngumu kwa kupewa “mwiba” mwilini mwake. Aliomba mara tatu kwa mwiba huo kuondolewa, na bila shaka alifikiri kwamba mwiba ukiondolewa atakuwa na nguvu zaidi kuitangaza Injili ila Mungu akamjibu kwamba nguvu ya Mungu itakamilika katika udhaifu wake si katika nguvu zake na Mungu alimwambia “neema yangu itatosha” (2 Kor.12:9).

Kwa hiyo Paulo alianza kuwa hodari katika udhaifu wake akiukubali na kuufurahia, kusudi, uwezo mkuu wa Mungu uwe juu yake. Mungu atamshika na kumwongoza, atamtawala na kumwezesha, Mungu atakuwa pamoja naye, pamoja na mwiba wake! Nguvu hiyo ni ya namna gani? Ni nguvu ya upendo, ya neema, nguvu ya rehema, na nguvu ya kweli. Nguvu ya namna hiyo haitoki kwetu, yatoka kwa Mungu. Kwa hiyo, hatuwezi kudai sifa wakati wa matokeo mazuri katika utumishi wala hatuna haja ya kukata tamaa wakati matokeo hayaonekani.

Kwa kuwa vyombo vinyonge na dhaifu huendelea katika utumishi wao ni thibitisho la nguvu ya ajabu ya Mungu, nao wavutwa kuendelea na utumishi kwa furaha. Hivyo, Mungu aweza kuchagua watu walioelimika au watu wasioelimika, watu walio na nguvu kimwili au walio dhaifu kimwili; wao wote huwa vyombo vya udongo, ambao ndani yao Nuru na Uwezo wa Mungu hufanya kazi. “Vyombo vya udongo” vinavyokosa thamani ni ushuhuda thabiti wa uwezo upitao kiasi ambao unaandamana na mjumbe anapohubiri Injili.

k.8-11 Watu hawajali wala hawatumii kwa uangalifu vyombo vya udongo. Udhaifu na unyonge wa mitume ulionekana kwa jinsi walivyotendewa vibaya, hata hivyo Mungu aliwalinda. Machoni pa ulimwengu walipata shida nyingi, ila walishinda kutokana na rehemu za Mungu zilizowaokoa daima. Ndipo Paulo alilinganisha mambo manne: La kwanza: Iwapo walisumbuliwa sana, hawakuzuiliwa kabisa hata vizuizi vilitokeza nafasi zingine. La pili: Mara kwa mara walibanwa wasijue la kufanya, hata hivyo, mwishowe wakatoka kwa usalama. La tatu: Walipofukuzwa mahali fulani waliacha kundi la waumini pale. Pia, mafundisho yalitolewa ambayo kwayo waumini walisaidiwa. Na mafundisho hayo yamewasaidia Wakristo kizazi baada ya kizazi. La nne: Wakati fulani Paulo alipigwa mawe na kuachwa hali akidhaniwa kuwa amekufa, ila Mungu akamwinua na kumtia nguvu, akaendelea na huduma yake.

Kwa kweli walikuwa kama “vyombo vya udongo”, wakati mwingine walikuwa na njaa, mara nyingi walisikia uchovu mwingi, walipigwa, walizama majini, walikuwa katika hatari mbalimbali, hata hivyo Mungu aliwapitisha salama akiwajalia neema yake na nguvu za ajabu, hata Paulo alishuhudia kwamba “ninapokuwa dhaifu ndipo nina nguvu” (2 Kor.12:10).

k.10-11 Katika hayo yote walifanana na Yesu Kristo. Bila shaka Paulo daima alikumbuka jinsi Bwana Yesu Mwenyewe alivyoishi kwa shida sana. Alimtaja Yesu mara nne katika vifungo hivi viwili. Daima Yesu alikuwa kama “anakufa” katika kuwatumikia watu mpaka upeo wa nguvu zake, aliwahudumia watu mchana kutwa akiwaponya, akiwafundisha, hakupata nafasi ya kupumzika ya kutosha, aliamka mapema sana ili apate nafasi ya kuomba, mara kwa mara hata nafasi ya kula aliikosa. Alishambuliwa na kuviziwa na adui zake hasa Mafarisayo na Waandishi na wapinzani wengine. Kuuawa Kwake kulikuwa hatua ya mwisho katika mwenendo wa “kufa”. Vivyo hivyo Paulo pia aliitwa kwa huduma iliyofanana na ile ya Yesu, huduma ya kujitoa bila kujihurumia, huduma ya kujihesabu kuuawa kila siku. Pia aliushiriki Uzima wa Yesu aliyefufuka, alijua kuokolewa kwa ajabu katika hatari mbalimbali, na kwa njia hiyo alitazamia “Ufufuo wa baadaye”. Kila siku Paulo aliamka hali asijue kama itakuwa siku yake ya mwisho. Alichukiwa sana sana, aliwindwawindwa daima, akawa tayari wakati wo wote kwa kuuawa. Hayo yote hayakumshinda, maana adui zake walishindwa kummaliza kabisa, ishara ya kuwa Yesu alikuwa akiishi ndani yake.

k.12 Taabu zake zilisababisha wale walioipokea huduma yake wapate “uzima” kwa kuwa Mwenye Uzima, Yesu Kristo, aliletwa kwao. Iwapo Wakristo wote huitwa kushiriki mateso inaonekana Paulo alipewa fungu kubwa zaidi. Baadhi hawakumwelewa na wengine walimshtaki isiyo kweli, hivyo alionja “mauti”. Hata hivyo, hakulegea wala kuchoka wala kukata tamaa, wala hakuwaacha kuzibeba shida zao peke yao.

k.13-14 Ni imani na hasa imani katika Ufufuo iliyomsukuma aendelee katika utumishi huo mgumu. Alijua kwamba siku moja atakufa, naye alikuwa na uhakika kwamba atafufuliwa kwa uwezo wa Mungu kwa sababu ameungana na Kristo Aliyefufuka. Iwapo ufufuo wetu umetengwa na ule wa Kristo kwa miaka mingi, hata hivyo, ufufuo wetu umefungamana na wake. Macho ya Paulo yalikazwa kutazama "Siku ya Ufufuo" na kwa njia hiyo alisaidiwa kuvumilia mateso na dhiki.

Yesu atamleta mbele za Babaye pamoja na waumini wa Korintho, na wote pamoja watakaribishwa na Baba, si Paulo peke yake, maana maisha yake yalifungamana na maisha yao kwa sababu ya huduma ya Injili. Lo lote atendalo alifanya kwa kuwaza faida ya roho zao, haidhuru ateswe kwa sababu hiyo.

k.l5 Shabaha yake hasa ilikuwa kumtukuza Mungu aliyejaa neema tele, naye alitaka wengi zaidi waonje neema hiyo kwa njia ya kushirikiana na Yesu, ndipo watazidi kumshukuru Mungu, na Mungu atazidi kutukuzwa. Lengo lake ni kwa watu wengi kumtukuza Mungu.

k.16-17 Maumivu ya ki-mwili ni kwa muda mfupi bali Utukufu ni wa milele. Atawezaje kuchoka katika huduma hiyo? Hawezi! Mwili ulizidi kudhoofika ila alisikia kufanywa upya rohoni kila wakati. Alitiwa nguvu ya ndani kwa sababu ya ushirika wake na Yesu. Dhiki na mateso vilimlazimisha amtegemee Mungu zaidi na zaidi, na kwa sababu ya shida zilizompata Mungu alikuwa akimtayarisha kwa "utukufu wa milele".

Katika mwanga wa tumaini la "utukufu wa milele" alihesabu mateso yake kuwa "mepesi" na pia "ya muda mfupi" (tazama orodha ya mateso na dhiki katika 2 Kor.11:23-27). Utukufu wa baadaye ni mazao ya dhiki zake kwa nazo zilizidisha uzuri wa utukufu ule. Bila shaka kama angaliwaza dhiki zake tofauti angalitishwa sana nazo, maana kwa kawaida dhiki au hatari moja ilipopita, nyingine ilitokea. Ndio mwenendo wa kawaida wa maisha yake.

k.18 Alizidi kutokutazama yaliyopo na hali zilizopo na kutazama yajayo. Tokeo la kufanya hivyo lilikuwa hakujali sana yaliyopo, wala kuangalia hali zilizopo. Alizidi kuwaza na kutazama mbele kwa maisha ya baadaye.

5: 1-10 <u>Tumaini la uhakika</u>

Katika sehemu hii Paulo aliendeleza wazo juu ya hali ya kudumu na hali ya kutokubadilika kuhusu maisha ya baadaye.

k.1 Alisema "twajua". Alijuaje? Alijua kwa sababu Mungu alimfunulia iwapo bado hajayaonja hayo. Ni ya hakika kabisa hata mtu aweza kujenga maisha

yake yote juu ya tumaini hilo. Paulo alidharau magumu yote ya wakati huo na kuyahesabu kuwa si kitu.

“nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii” ni nini? na “jengo litokalo kwa Mungu” ni nini? Pengine maana yake ni maisha yetu ya sasa na maisha ya baadaye. Wengine huwaza “nyumba ya maskani yetu” ni miili yetu tuliyo nayo; na “jengo litokalo kwa Mungu” ni mwili wa roho yaani mwili wa ufufuo. Neno “jengo” latuelekeza kufikiri juu ya hali ya kudumu; tena “kutoka kwa Mungu” na “isiyofanywa kwa mikono” huleta wazo la “kitu cha kiroho”.

Maisha yetu ya hapa duniani si ya raha wala ya pumziko. Ni maisha ya kubadilikabadilika, mfano wa mtu anayeishi katika hema na kuhamahama. “Hapo hatuna mji udumuo”. (Ebr.13:14). Tena maisha yetu ya sasa ni ya muda, yatakoma wakati wa kufa. Neno hilo halimsumbui Mkristo kwa sababu mbele yake ni maisha ya raha na pumziko jema, na starehe huko mbinguni. “Tunao” katika maisha yetu ya Kikristo ya wakati huo twaonja kwa kiasi “limbuko” la maisha ya baadaye (Kol.3:1-3).

(Ikiwa Paulo alikuwa akiyasemea maisha baada ya kufa na kabla ya kufufuka, ni wazi kwamba hakutaka kuishi bila kuwa na “mwili” wa aina fulani. Alitaka kutoka katika mwili huu wa sasa kwa kuubadili na kupata mwingine, usiopatikana na kufa).

k.2-3 Hapo Paulo alisema juu ya “kuvikwa kao letu”. Maana yake, alitaka kuvikwa kwa maisha ya baadaye, maisha kamili na ya kudumu. Lakini, hali ya kuwaza mambo kama hayo haina maana kwamba hatufai kazi hapa duniani, si kana kwamba yeye (na sisi) twataka kuondoka haraka katika dunia hii, la, sivyo, ila ni dhiki zake zilizomfanya atazame kwa yale ya mbele, yatakayofuata baada ya dhiki hizo.

k.4 “twaugua” kama watu waliolemewa na mzigo (Flp.1:22-24). Si kwa sababu twataka kuvuliwa bali kwa sababu twataka kuvikwa, yaani kuingia kwenye hali ya kushirikiana na Kristo kwa ukaribu zaidi na kuwa pamoja naye moja kwa moja (1 Kor. 15:24). Katika maisha ya muumini hakuna muda kati ya kuvuliwa na kuvikwa, iwapo katika kalenda muda unaweza kuwa mrefu. Pengine liko wazo la kuvikwa vazi la Haki ya Kristo.

k.5 Kwa nje inaonekana kama mambo yote huelekea kumezwa na mauti. Twawezaje kuishi maisha yetu juu ya msingi wa kujua tunayo maisha ya kudumu pamoja na Yesu. Ni Mungu anayetuweka tayari kwa kutupa Roho Wake. Ni Yeye, peke yake, awezaye kusifiwa, Roho ni kipawa chake kwetu. Kwa wakati huo Roho ni dhamana, twaonja uwezo wa Kuwako Kwake maishani mwetu, kama limbuko. Kwa njia yake Mungu ametuumbia upya, tendo limetendeka ndani yetu, haibaki kama wazo au dhana tu. Makusudi yake ni kuleta wana wengi kwa utukufu.

k.6 Kwa hiyo, katika dhiki na mateso, Paulo alikuwa mjasiri na mchangamfu, hakukata tamaa, wala hakuchoka. Aliendelea kufanya kazi kwa moyo mkuu. Maisha yetu ya sasa ni mfano wa maisha ya kuishi katika hema, tunaishi mbali na Bwana, hatumwoni, hata hivyo, tunashirikiana naye, ila si uso kwa uso. Kukata tamaa ni kukana Kuwako Kwa Roho maishani mwetu.

k.8 Paulo alikataa kuwazawaza dhiki na taabu zake. Hakutafuta kuziepuka au kuzitoroka, maana alifahamu alikuwa akikanyaga nyayo za Bwana Yesu. Kama angaliruhusu mawazo ya kujihurumia, angalishindwa kuendelea. Kweli, alitamani sana sana kuwa na Yesu na kumwona "uso kwa uso" ila kwa wakati huo budi aendelee na huduma.

k.9 Tumaini hilo lilizidisha ndani yake nia ya kumpendeza Bwana. Alimpenda Yesu sana na alitaka Ufalme wake usimamishwe katika ulimwengu huu, kwa hiyo, haidhuru awe wapi, alilenga kumpendeza. Hata sisi twapaswa kuwa na nia hiyo ya kumpendeza.

k.10 Ndipo, kutokana na mawazo hayo, Paulo aliingia kuwaza juu ya Hukumu ya Mwisho. Jinsi wanadamu walivyomwona si kitu kwa sababu yupo Mmoja atakayemhukumu yeye na wale pia. Tena alifahamu kwamba aliyepewa vingi, atadaiwa vingi.

Hakuna mwanadamu awaye yote atakayeweza kukwepa Hukumu hiyo. Mungu ameiweka tayari Siku yake na dhamiri zetu zaishuhudia. Hukumu hiyo itawapata "watu wote", hata tukiita milima ituangukie, haitabadili lo lote.

Atakayetuhukumu ni Kristo, Yule aliyekufa kwa ajili yetu, yule ambaye kwa kazi zake Msalabani, kila mtu amkubaliye apewa uamuzi wa "huna hatia"!! Ndipo itadhihirika kama imani iliongoza maisha yetu au siyo. Hukumu itakuwa juu ya maisha yetu jinsi tulivyoishi na kutenda, ili tuupate ujira. "Jinsi alivyotenda kwa mwili" iwapo mwili huu wa sasa ni wa hapa duniani, wa wakati huu, hata hivyo ni maisha yetu tunayoishi katika mwili huo ambayo itahukumiwa na Mungu.

5:11-15 <u>Nia na shabaha za Mhubiri</u>

Yeye Paulo alifanya huduma yake katika "hofu ya Bwana". Mambo mawili yalimvuta kufanya kwa kanuni hii. Jambo moja lilikuwa "utukufu" wa Agano Jipya; na la pili lilikuwa Hukumu ya Siku ya Mwisho. Kazi yake ya kila siku ilikuwa kuwavuta na kuwashawishi watu waiamini kweli ya Injili ili watubu dhambi zao na kumwamini Kristo. Bila shaka alijaribiwa kukaza upande mmoja wa maisha ya Kikristo, yaani uzuri wake, bila kutaja mateso au dhiki zitakazoweza kumpata Mkristo katika kumfuata Yesu kwa uaminifu. Pengine alijaribiwa kuuonyesha ujuzi wake mwingi. Alipopingwa ingalikuwa rahisi kuridhiana na watu na kuwapaka mafuta na kupunguza madai ya Injili au kutokutaja mambo fulani ili asiwakwaze. Lakini alitiwa nguvu asifanye hivyo.

Alifahamu kwamba ni Mungu aliyemwita na ya kuwa Mungu alifahamu nia na sababu zake katika kazi hiyo, na kwa sababu hiyo aliweza kukabili hukumu zisizo haki za watu.

Pale Korintho Wakristo kadha walikuwa wakishawishiwa na mitume wa uongo waliomdharau Paulo, hata utiifu wao kwa Paulo ulipungua. Hao mitume wa uongo walipata nguvu ya kumshtaki Paulo kwa jinsi alivyobadili mipango yake ya kuja kwao. Paulo hakujitetea kwa kutoa maelezo marefu, Wakorintho walimfahamu ya kutosha kwa sababu alikuwa amekaa nao kwa muda mrefu, alijua dhamiri zao zitawathibitishia ukweli wa kujitoa kwake. Wale mitume wa uongo walitegemea hali zao za nje, hawakuwa na mzigo juu ya mambo ya ndani kama imani na upendo. Paulo alikaza kwamba kazi yake hasa ilikuwa kuvuta watu kwa Kristo, hakutaka fedha wala cheo, wala sifa zao.

Wale waliomkubali Kristo walipata amani ya rohoni, walisamehewa dhambi zao, dhamiri zao zilitulizwa, nao walionja nguvu ya Injili, na waliweza kutambua uzito wa mzigo ambao Paulo alikuwa nao kwa ajili yao. Uaminifu wake na bidii zake zilizidi zile za wanadamu wenye kazi zingine, maana alifanya kazi yake katika "hofu ya Bwana" Alikaa nao kwa muda mrefu kwa kufunuliwa na Mungu katika maono (Mdo. 18: 10). Alijua kwamba dhamiri zao zitawashuhudia (k.11b).

k.12 Kwa nini Paulo alichukua nafasi ya kukaza jinsi alivyoishi kwao na mzigo aliokuwa nao? Kwa nini alitaka waipime vizuri kazi yake? Je! alikuwa na wivu? la. Sababu ilikuwa katika wao kusitasita na kuvutwa na mitume wa uongo. Hao wakifaulu kuitilia mashaka mamlaka ya Paulo ndipo watafaulu kuutilia mashaka ujumbe wa Injili aliowaletea. Inaonekana kwamba waumini hawakujua njia ya kupambana na hao mitume wa uongo. Pamoja na hayo watapata msaada kwa kukumbuka jinsi maisha yao yalivyobadilika na kutiwa nguvu kwa kuupokea ule ujumbe wa Injili ulioletwa na Paulo. Badala ya kuyajali mashtaka ya mitume wa uongo walipaswa kumtetea Paulo, maana yalikuwepo mengi katika kielelezo chake ambayo yalitosha wajisifu kwa ajili yake. Hakutaka wamsifu ila alitaka watambue jinsi mambo yalivyo hasa ili wawapinge adui zake waliowaza mambo ya nje tofauti na Paulo aliyewaza mambo makuu ya ndani kuhusu uhusiano wao na Mungu.

k.13 Pengine baadhi ya watu walisema kwamba amerukwa na akili. Labda kwa sababu ya maono aliyoyapata, labda kwa sababu ya ile barua kali. Ila kwake yote aliyoyafanya yalikuwa kwa ajili ya Mungu na kwa ajili yao. Aliwezaje kuwa mpole huku chachu ya uovu imeanza kuenea kati yao?

k.14 Hasa alitawaliwa na upendo, kama ule wa Kristo. Kristo aliwaita Mafarisayo "wanafiki" kusudi awashtushe ili watambue hatari waliyo nayo kwa sababu ya kiburi chao cha kiroho. Walijiona kuwa sawa, wakaridhika na hali yao. Ni kwa sababu ya kuwapenda Kristo alisema hivyo, kusudi wasipotee.

Vivyo hivyo Paulo alisukumwa na upendo wa Kristo uliomshika ili asiwapendeze watu wala kujipendekeza kwao. Atawatumikia katika upendo kama wakimwelewa au siyo (Lk.12:50).

k.15 Aliwajibika hivyo kutokana na mambo mawili kuhusu Kifo cha Yesu. Kifo hicho kiliwagusa watu wote, maana Alikufa mahali pao na badala yao. Alikufa kifo ambacho si chake, ni kifo cha mwenye dhambi. Mungu aliweka juu ya Mwana Wake dhambi za watu wote na kuzihukumu katika Yeye, na Yeye amelipa deni lao. Halafu Kristo aliachiliwa, Akafufuka kutoka kwa wafu; vivyo hivyo sisi twaachiliwa na tumefufuliwa ndani yake. Basi, tu wake, kwa imani twaunganika naye na kuushiriki Uzima wake wa Ufufuo. Hatuwi kama tulivyokuwa.

Neno la pili ni kwamba tusiishi maisha yetu kwa faida yetu wenyewe tu, bali kwa ajili ya Yesu, aliyetufia. Yeye awe kiini cha maisha yetu.

k.16-17 Upendo wa Kristo na Maisha mapya katika Kristo. Hali moja mpya ya maisha mapya inahusu namna ya kupima na kuthamini mambo, nayo itakuwa kinyume kabisa cha hapo nyuma. Umaana wa mtu na thamani yake hautokani na mambo ya nje kama ni mtu wa watu au ametoka mahali fulani; wala haihusu kiasi cha mali aliyo nayo; wala elimu yake, wala uzuri wa umbo lake, wala rangi yake. Hayo yote si kitu. Kitu kikubwa ni uhusiano wa mtu na Yesu Kristo aliyemfia. Hata katika kumwaza Kristo. Alionekana kama hakufaa kuwa Masihi kwa sababu alizaliwa kwa wazazi maskini, akalelewa katika mji usiokuwa na sifa yo yote katika historia ya Wayahudi, ndipo mwishowe aliuawa kwa ukatili sana kama mhalifu wa hali ya juu. Yesu Mwenyewe aliwaambia watu kwamba “ninyi mnahukumu kwa kufuata mambo ya mwili”, na mitume wa uongo walifanya vivyo hivyo. Bila shaka Paulo mwenyewe alimwaza Yesu hivyo kabla ya kuokolewa kwake.

k.17 Matokeo ya Ukombozi uliofanywa na Kristo alipokufa Msalabani ni kuuleta uwezekano wa mabadiliko makubwa katika uhusiano wa mtu na Mungu. Ulimwengu wote umetangazwa kuwa una haki katika Kristo, na kwa sababu hiyo, mtu ye yote atahesabiwa haki mara atakapompokea Kristo. Mabadiliko hayo hasa yahusu uhusiano kati ya watu na Mungu. Mwenye dhambi na mwenye hatia huhesabiwa kuwa Mtakatifu na mwenye haki, asiye na hatia. Katika msingi wa kazi ya Kristo Paulo aliwasihi wenye dhambi waupokee huo upatanisho.

5:18-2l Ujumbe wa Upatanisho na Huduma yake

Mungu ndiye mwanzilizi wa hayo yote mapya kama alivyokuwa mwanzilizi wa mpango wa uumbaji wa kwanza. Mungu alitangulia na katika kumtuma Kristo na kwa njia ya Upatanisho Yesu alioufanya alipokufa Msalabani, ametutoa chini ya taratibu na hali za zamani na kutuweka “katika Kristo”. Twapataje

kushiriki baraka hizo? Ni lazima Ujumbe wa Upatanisho utangazwe kwa watu na watu waitike kwa kumpokea Kristo. Mungu aiweka “Huduma ya Upatanisho” mikononi mwa watumishi wake, ambaye Paulo alikuwa mmojawapo. Paulo aliitwa na kuwezeshwa kuwa Mjumbe wa Upatanisho, Mungu akiwa pamoja naye na kwa njia yake Mungu alikuwa akiwasihi watu waupokee huo upatanisho.

k.19 Mungu aliupatanisha “ulimwengu” na Nafsi Yake, kwa hiyo upatanisho ni kwa kila mwanadamu wa mahali pote na wa wakati wote. Iwapo upatanisho ulifanyika mara moja tu pale Msalabani, hata hivyo, baraka zake zaendelee na kuwafikia wote watakaoitika wanapotangaziwa habari njema ya Injili.

k.21 Hicho kifungu hutoboa kabisa jambo lililotendeka katika upatanisho huo. Ni jambo la ajabu sana sana. Kristo, ambaye hakuwa na dhambi, wala hakujua dhambi, wala hakufanya dhambi, alifanywa kuwa “dhambi” kwa mapenzi ya Mungu, ili sisi tupate kufanywa “kuwa haki”, sisi ambao tu wenye dhambi, tusio na haki. Ni kama pale Msalabani Kristo na sisi tulibadilishana hali, Yeye alibandikwa hali yetu ya dhambi, na sisi tunaomkubali twavikwa haki yake. Neno hilo ni la kushangaza sana sana.

6:1-13 Paulo aliwasihi waitike vema akionyesha jinsi ilivyompasa aishi

Paulo ~~alifurahia sana Huduma ya Upatanisho aliyopewa na Mungu (1 The~~ 2:4) ila, kwa upande wa pili, alitetemeka sana kwa kuwa alipewa wajibu mzito (Mdo.20:28).

Je! Wakorintho wataonaje watakapotambua hiyo huduma na kazi ambayo Mungu amemkabidhi Paulo, na jinsi alivyoitimiza kwa uaminifu.

k.1 Paulo aliwasihi Wokorintho waupokee upatanisho wa Kristo. Mungu huwaita na kuwasihi watu kwa njia ya kuvitumia vinywa vya wahudumu na wainjilisti (1 Kor.3:9).

Pia, Paulo alikuwa akiwasaidia Wokorintho ili waupokee huo upatanisho. Mungu aliidhihirisha neema yake katika ukombozi huo (Rum.11:16). “Neema” ni nini hasa? Neema ni kipawa na baraka, nao Wakorintho wapaswa kuipokea kwa faida yao. Isiwe bure kwao. Itakuwa bure yaani itakuwa haina kazi ikiwa hawataijali, wala kuiruhusu ibadili nia na mawazo yao. Wasiwaze uzuri wao na kujisifu, bali waitegemee na kuisifu neema tu. Kutokana na maneno ya Paulo katika 6:13 na 7:2 labda baadhi yao walikuwa hawajampokea Yesu kibinafsi

k.2 Paulo aliwasihi waiitike mara, maana wakati ni huu na nafasi yao ni sasa, kwa hiyo wasiipoteze nafasi hiyo ya ajabu iliyo mbele yao. Yapasa ujumbe wa Injili utangazwe bila kukawia na itikio litafutwe mara, maana wakati wapita na nafasi pia zapita.

k.3 Kwa sababu hiyo, Paulo aliwajibika kuangalia sana maisha yake mwenyewe kusudi asilete kikwazo cha aina yo yote. Kwa vyo vyote Huduma yake isilaumiwe, ili watu wasiupate udhuru wa kuikataa Injili kwa kuona hitilafu fulani katika yeye. Mara nyingi watu hutumia jambo fulani katika maisha ya mhudumu kuwa udhuru wa kutokuitika vema na kumkubali Kristo. Kweli iliyopo ni kwamba ujumbe wa Injili husimama jinsi ulivyo, wala hauwezi kubadilishwa kutokana na maisha au tabia za wahubiri wake. Hata hivyo, kazi za Kanisa hufanikiwa kutokana na uaminifu wa watumishi wake, na kinyume chake hupata shida kwa watumishi wasio waaminifu.

Paulo na wajoli wake hawakuweza kamwe kushtakiwa kwamba wao wameipokea neema ya Mungu bure. (mtu mmoja alifananisha wahubiri wasioishi kulingana na Injili kama kinyozi mwenye upara anayejaribu kumwuzia mwingine dawa ya kurudisha au kuotesha nywele).

k.4-5 Uvumilivu na mateso yake viliushuhudia ukweli wa Utume wake pamoja na kuwa kielelezo chema kwa waumini. Halafu Paulo alitaja aina mbalimbali za mateso akitanguliza subira, ndipo shida za kawaida, ndipo shida zilizosababishwa na wengine, kisha shida kutokana na kujinyima kwake.

k.6-7 Halafu aliorodhesha tabia njema zilizojitokeza wakati wa dhiki mbalimbali. Injili ya kweli ilihubiriwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kusudi wote watambue ya kuwa Mungu alikuwa akifanya kazi kwa nguvu ndani yake. Kazi ya kuhubiri Injili haifanani na kazi za kawaida za kibinadamu (1 Kor.2:1-5).

k.8 Kifungu hicho chaonyesha kwamba Injili ilipokelewa na wengine na kukataliwa na wengine na ilimbidi yeye apitie katika hali mbalimbali na hali hizo zote zilihitaji hekima.

k.9 Wengi walimkataa yeye pamoja na Injili aliyoihubiri wakiwaza kwamba yeye na Injili yake, si kitu. Alionekana kama mtu wa kufa, daima alikuwa hatarini, hata hivyo, ajabu ni kwamba, ilipofikiriwa mwisho wake umefika, kumbe, sivyo ilivyo, akatoka tena yu hai. Mara nyingi alipingwa, na watu walimaanisha kwamba Mungu hakupendezwa naye, lakini yeye alijua kwa hakika kwamba Mungu alikuwa pamoja naye, akimsaidia na kumwokoa katika hatari zake zote.

k.10 Watu walipenda mambo ya kuwafurahisha lakini Paulo alionekana kama mtu aliyekosa furaha. Hakukosa furaha, ila furaha zake zilikuwa za ndani kabisa kutokana na imani na tumaini lake na kwa kuonja uzuri wa Mungu binafsi. Furaha yake haikutegemea mambo ya nje. Mara nyingine alikosa mahitaji ya lazima, na mara nyingine alikuwa na vyote alivyohitaji (Flp.4:12). Potelea mbali alikuwa na vingi au alikuwa na vichache, kiroho alijisikia kuwa tajiri sana, naye aliwatajirisha wengine katika kuwaletea habari ya utajiri wa

kweli. Alikuwa mrithi pamoja na Kristo na wa baraka zote za mbinguni na za uzima wa milele (1 Kor.3:21-22).

k.11 Kwa Wakorintho alikuwa amesema nao waziwazi akiufunua moyo wake, wala hakuzuia kuwaambia jambo lo lote kwa sababu aliwapenda na kusikia mzigo mkubwa juu yao. Alitia maanani shtaka lao la kuwa na kigeugeu katika kubadili mipango yake, akawaeleza sababu zake.

k.12 Kwa wakati huo alitaka waitike vema, aliwaomba wamwekee nafsi mioyoni mwao. Pengine walifikiri kwamba Paulo hakuwa na mzigo juu yao na ya kuwa aliyashughulikia makanisa mengine kuliko lao. Lakini hii haikuwa kweli. Hasa shida ilikuwa upande wao kwa sababu waliruhusu mambo mengine yaukamate usikivu wao kuliko Injili.

k.12 Wao ni watoto wake kiroho. Alipowasihi wamwitikie vema na kufuata kielelezo chake ni kwa sababu wao ni watoto wake kiroho.

MASWALI:

4:1-6Katika kuwa mhudumu wa Agano Jipya ilimbidi Paulo awe na tabia gani? Je! tabia hizo bado zinatakiwa katika wahudumu wa siku hizi? Eleza.

4:7-18 Je! Siku hizi wahudumu wa Injili wanazifuata nyayo za Paulo na kuwa tayari kuvumilia shida na kudhiliwa, au ni watu wapendao cheo na heshima? Toa mawazo yako.

Hazina ni nini na chombo ni nini? Eleza maana yake. Kwa nini Mungu ameweka „hazina" katika „chombo cha udongo"? Mara nyingi twafikiri kwamba udhaifu wetu unazuia maendeleo ya Injili ila maneno ya Paulo katika sehemu hiyo yanatusaidia kuwaza kwamba sivyo ilivyo. Eleza.

4:18Paulo alisisitiza jambo la mbinguni na mambo ya baadaye. Je! Ni neno linalotawala maisho yako? Eleza.

5:1-10 Kwa nini Paulo alikubali kuwa „chombo cha udongo". Aliishi katika matazamio gani alipopatwa na dhiki na mateso?

5:10Katika maisha yako wazo la hukumu linagusaje kazi yako na mwenendo wako?

5:11-15Kwa nini Paulo alifanya huduma katika "hofu ya Bwana"? Waonaje? Siku hizi neno hilo linawaongoza watumishi wa Kristo?

5:16-21 Andika kwa kifupi jinsi ambavyo ungemwambia rafiki yako asiye Mkristo habari za Upatanisho aliofanya Yesu Msalabani ukitumia maneno ya kawaida ya kila siku badala ya lugha ya Kibiblia.

Tunawezaje kutangaza Injili kwa mamlaka na kwa moyo bila kutisha watu? Eleza.

6:11-13 Wahudumu wa Injili wanao wajibu gani kufuatana na Upatanisho uliofanywa na Kristo? Waishi maisha gani?

6:14-7:1 <u>Wito wa kujitenga na wasioamini</u>

Iwapo Paulo alikuwa ameukunjua moyo wake kwao siyo kusema hawezi kuwaonya juu ya makosa kama yakiwapo. Wakristo walioishi katika miji mikubwa na kati ya wapagani wengi walitatizwa na swala la kujitenga nao kwa kiasi gani na kwa mambo gani. Katika Waraka wa Kwanza Paulo alisema kwamba hawana haja ya kujitenga nao kabisa. Yawezekana baadhi yao walifikiri kwamba hawana haja ya kuwa na tahadhari katika mambo kadha wa kadha. Huenda baadhi yao walishindwa kuwa wazi kwa Paulo nao hawakuikunjua mioyo yao kwake kwa sababu walijua hawajajitenga vizuri na mengine, kama kuabudu sanamu n.k. Paulo alijua walikuwa na haja ya kuyarekebisha mengine ili Injili ipenye maishani mwao na kufanya kazi ndani yao. Huenda mitume wa uongo waliwashauri kwamba hawakuwa na haja ya kujitenga na desturi kadha wa kadha. Hasa Paulo alikuwa akisemea uhusiano wao na wasioamini, si uhusiano wao na waumini wenzao waliokuwa dhaifu.

k.14 Iliyopo ni kwamba wasifanye uhusiano wa karibu na wa kudumu, kama kufunga ndoa na wasioamini. Wakifanya muungano wa namna hiyo watasikia ni vigumu kushika kweli na watavutwa kuridhiana katika mambo mbalimbali.

Kisha Paulo aliwaulizia maswali matano yenye shabaha ya kutoboa wazi tofauti kubwa iliyopo kati ya muumini na asiyeamini. Majibu ya maswali hayo matano ni mamoja nayo yanaonyesha kwamba haiwezekani uwepo muungano wa kudumu kati yao. Muumini huwa ni kinyume cha asiyeamini, wala hamna kuwapatanisha. Mwenye imani hukubali kile ambacho asiyeamini hukataa, maana haki haikubaliani na uasi; na nuru hufukuza giza, na kamwe hamna ushirikiano kati yao.

k.16b Ndipo Paulo alitangaza kwamba “sisi tu hekalu la Mungu aliye Hai”, maneno hayo ni lugha kuhusu Agano, yaani kugusa uhusiano kati ya Mungu na watu wake. Alipotumia neno “sisi” hakusema kwa kiburi bali alisema kwa unyenyekevu na shukrani. Mungu alikuwa akiishi ndani yao na kati yao, kwa hiyo wapaswa kujitenga na yote yasiyopatana na Mungu Aliye Mtakatifu. Ni juu yao kuacha mengine ili waufurahie urafiki wao na Mungu. Mungu yu Hai, kinyume cha sanamu zisizosema wala kusikia. Ni tendo la Mungu kukaa ndani

yao, Mungu amenia hivyo na ni Yeye aliyetangulia kuweka makao yake ndani yao. Ameahidi kuwakaribisha kama watoto wake, na itaonekana kuwa Mungu anakaa ndani yao kwa maisha wanayoishi.

k.17 Kwa sababu hiyo wajibu wao ni kujitenga na uchafu na uovu unaofanyika katika jamii ya wapagani; taz. Isa.52:11 Neno la kujitenga, ambalo Paulo alitumia hapa ni neno la nguvu sana, sawa na neno la Mt.13:49; 25:32. Lakini jambo la kujitenga haina maana ya kujitenga tu, bali shabaha yake ni kuwa muumini afurahie urafiki wake na Mungu pamoja na waumini wenzake.

k.18 Pamoja na kuwa hekalu la Mungu, Kanisa la Kristo ni familia ya Mungu. Mungu, zaidi ya yote, ni Baba wa watu wake, wao ni wana na binti zake (Yer.31:9; Isa.43:6; 2 Sam.7:14). Kwa sababu hiyo, likitokea jambo fulani katika familia ya Mkristo ambalo ni kinyume cha imani yake itampasa aweke nyuma madai ya ki-familia na kumtanguliza Mungu na mapenzi yake.

7:1 Wakristo wa Korintho walikuwa na haja ya kuzingatia sana ahadi za Mungu katika 2 Kor.6:16b; 17b; 18, na kuishi kufuatana nazo katika maisha matakatifu ya kila siku. Waukuze utakatifu katika maisha yao na wakamilike katika kila jambo, hali wakimcha Mungu, wala wasinaswe na mtego wa kuwapendeza wanadamu au kujipendekeza kwao. Miili yao na roho zao zilihitaji kutakaswa. Jambo la kutakaswa ni jambo linaloendeleaendelea katika maisha ya Mkristo mpaka kufa kwake, nalo lahitaji bidii nyingi (1 Pet.1:17).

7:2-16 <u>Kurudisha hali ya kuaminiana</u>

Paulo alilirudia ombi lake la 6:13. Wao walikuwa na nafasi kubwa katika moyo wa Paulo. Aliwapenda sana, aliwathamini sana, alikuwa na mzigo juu ya hali yao ya kiroho. Aliwaomba wampe nafasi katika mioyo yao. Hakuona sababu yoyote ya wao kuwa na mioyo “baridi” kwake. Ni adui zake waliojitahidi kuupunguza uzuri wake machoni mwao kwa kumsingizia vibaya. Alitamani wampende kwa uhuru. Alikuwa amejitetea kuhusu mambo mbalimbali kusudi awasaidie kutambua hila za adui zake. Hakutaka wafikiri kwamba yeye anawawaza vibaya na kuwashtaki, la, hata kidogo, yeye yu tayari kufa na kuishi pamoja nao. Hata ombi hilo hakulitoa kwa ajili yake mwenyewe bali kwa ajili ya Kristo na Injili. Alikuwa amefundisha Injili, na pia ameishi kwa kanuni ya Injili. Yote hayo yalidhihirika wazi kwa jinsi alivyoishi kati yao na kwa sababu hiyo alikuwa na ujasiri wa kusema “tupokeeni sisi” au “mpokeeni Kristo” maana mawili hayo ni mamoja kutokana na jinsi alivyoishi kwa kufuata kielelezo cha Kristo. Aliwakumbusha jinsi alivyoishi kati yao; hakuwadhulumu, hakujitafutia faida yake mwenyewe, hakumfanyia mwingine ubaya, la.

k.3 Hakutaka wafikiri kwamba alikuwa na neno juu yao, la, hata kidogo, ila ni adui zake waliomsingizia ili watu wawaze hivyo. Ni wazi kwamba Paulo hakuwaweka pembeni, maana wakati fulani hakuweza kuendelea na kazi

nyingine mpaka alipoonana na Tito na kujua hali zao. Alifungamana nao, alikufa pamoja na Kristo sawa na wao walipomwamini Kristo, na sasa amefufuka na Kristo pamoja nao. Ni jambo la kweli lenye nguvu, yeye na wao wameushiriki umoja wa maisha katika Kristo.

k.4 Kinyume cha kuwa na malaumu alikuwa na tumaini kubwa juu yao na kuwaonea fahari alipozungumzia habari zao katika makanisa mengine. Kwa hiyo hakuwa na haja ya kuficha mambo, aliweza kusema waziwazi jinsi alivyoona na kujisikia, na hali hii inatakiwa katika jumuiya ya Kikristo. Alikuwa mjasiri alipoona matunda ya Injili katika maisha yao, naye alijaa furaha alipojulishwa na Tito habari ya maendeleo yao. Iwapo alikuwa katika dhiki nyingi ripoti ya Tito ilimfariji sana.

k.5 Aliwaelezea wazi yaliyotokea na jinsi alivyosikia. Alikumbuka jinsi ambavyo hakuweza kutulia, akaondoka Troa na kufika Makedonia ili akutane na Tito. Hata katika Makedonia, mahali ambapo waumini walimkaribisha vema wakati wote, hata pale, alikuta shida. Hakusema ni shida gani. Kwa ndani alizidi kuhofu Tito alipochelewa kufika, akaanza kuwa na wasiwasi juu ya hali zao.

k.6 Baada ya kuonana na Tito hofu zake zilitoweka, Mungu alimpatia faraja (tabia ya Mungu ni kuwafariji wanyonge). Alisikia kufarijika kwa mambo mawili: moja ni la kufika kwa Tito, potelea mbali awe ameleta habari gani, kule kumngojea kulikwisha. Pili, habari aliyoileta Tito ilikuwa njema.

k.7 Hao waumini wa Korintho walikuwa wameyatubu makosa yao na kuyabadili mawazo yao juu ya Paulo, hata waliiombolezea hali yao ya hapo nyuma ya kumwudhi, nao walionyesha bidii nyingi za kumpenda na kutaka kuwa na uhusiano mwema naye, hata walitamani sana kumwona uso kwa uso. Tito aliendelea kumwambia Paulo mengi na kadiri alivyomwambia ndivyo Paulo alivyozidi kufurahi.

k.8 n.k Huzuni iliyoumiza ikatokeza furaha iliyoburudisha. Hapo nyuma Paulo alikuwa amewakemea Wokorintho vikali nao hawakupenda kukemewa hivyo. Paulo alifahamu kwamba hawatapenda kukemewa kwa ukali ila shabaha yake haikuwa kuwachukiza bali alikuwa akilenga neno moja tu, awasaidie kuzingatia juu ya hali yao mbaya ya kiroho. Alipokwisha kuiandika ile barua kali alisikia wasiwasi na kufikiri kwamba pengine amepita mpaka katika ukali wake. Alihofu kwamba watazidi kuwa na mioyo migumu, ndipo kazi alizozifanya kati yao zitakuwa bure. Hakutaka kuleta farakano wala kufanya huzuni yao isipoe, la, ila ilimbidi awashtushe kusudi watambue hatari waliyo nayo na kujirekebisha. Kwa hiyo, wakiijali ile barua baraka itapatikana.

k.9 Sasa kwa sababu ya matokeo mazuri yaliyotokea alifurahi kwa kuwa walikuwa wameshtushwa kiasi cha kujirekebisha. Njia ya Paulo ilikuwa kama njia ya Mungu, kwa sababu Mungu hafanyi lolote kwa kusudi la kusababisha

hasara na maudhi tu, bali lengo lake ni kuokoa. Huzuni yote inayoleta mtu kutubu ni huzuni ya Ki-Mungu. Huzuni yote inayomwacha Mungu nje humwingiza mtu katika uchungu na masikitiko na mwisho mtu hubaki katika hali ya kujidharau na kujihurumia. Barua ya Paulo iliwahuzunisha, lakini kwa muda tu, tena huzuni yao ilikuwa ya namna ya Ki-Mungu, iliyoleta toba la kweli, kwa hiyo, badala ya hasara walipata baraka.

k.10 Paulo aliendelea kusema juu ya huzuni, akifundisha kwamba kule kukemea kwa maneno au barua au tendo fulani yapasa kuwa na lengo la kuleta watu kwenye toba la kweli, liletalo wokovu, ndipo hakuna majuto. Neno ambalo Paulo alihofu lilikuwa kuwahuzunisha ndipo wao kukosa kutubu kweli. Wakihuzunishwa kwa namna ya dunia, watabaki katika huzuni, au watajuta tu, bila kutubu toba la kweli.

k.11 Ndipo Paulo alitaja baraka mbalimbali zilizopatikana kufuatana na huzuni yao ya jinsi ya ki-Mungu. Badala ya kuwa walegevu walikuwa na moyo wa kujirekebisha kufanya lililo jema badala ya kuridhiana na uovu kati yao. (Ling. na 1 Kor. 5:1n.k). Walikuwa tayari kujitetea na kuwa na msimamo. Walisikia aibu juu ya hali zao za hapo nyuma. Walitaka kumwona Paulo na walikuwa tayari kumtetea. Maneno kama bidii, kukasirika, hofu, shauku, kujitahidi, kisasi, ni dalili za kuonyesha kwamba wameamka baada ya kupoa na kuridhika na hali zao. Paulo alijumlisha mabadiliko hayo kwa maneno “kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo” kama wafuasi wa kweli wa Kristo.

k.12 Katika mambo hayo shabaha yake hasa haikuwa mkosaji aadhibiwe tu, wala aliyekosewa apate haki yake tu, la! jambo kubwa zaidi lilikuwa kwamba bidii yao idhihirike wazi, kusudi ionekane. Bidii ya nini hasa? bidii yao kwa Paulo na wenzake? Ni nani atakayefaidi kwa kuonekana wazi bidii hiyo? Je! Ni kwa Paulo kuiona? La! Jibu la kushangaza ni ili wao wenyewe waione!! Katika ugomvi na matatizo na mashindano yaliyotokea ilikuwa rahisi jambo moja kubwa lisionekane, na jambo hilo ni bidii yao kwa Paulo na wenzake waliowaletea Injili. Tena walipaswa watambue neno hilo “mbele za Mungu” kuwa neno la maana sana.

k.13 Iliyopo ni kwamba hayo yametokea, na Paulo amesikia kufarijika sana. Tunakumbuka kwamba jambo la faraja lilisisitizwa mwanzoni wa waraka huo.

Tito pia alifurahishwa sana na hali ya Wakorintho akiwa na matumaini makubwa kwamba wamerudi katika njia nzuri. Bila shaka alipokwenda kwao alisikia uzito na kuwa na mashaka akitamani kuona nguvu ya Injili iwashindie matatizo yao. Aliwaacha katika hali ya wao kutengeneza mambo, hivyo alipata kupumua vizuri na kuwa na raha. Paulo alikuwa amemhakikisha kwamba, ki- msingi Wakorintho walikuwa waumini wa kweli wa Kristo. Kuwavunia hivyo kumeonekana kuwa sawa na Tito ametiwa moyo.

k.15 Wakorintho wamepata rafiki mpya katika Tito na bila shaka uhusiano wao utaendelezwa atakapozidi kwenda kwao na kuonana nao. Wakorintho walimtii Paulo na Tito kama wajumbe wa Injili, kwa hiyo utii wao hasa ulikuwa utii kwa Injili si utii kwa watu kibinafsi. Walimkaribisha Tito kwa moyo na kwa kweli, si kwa sababu ya kutishwa naye, bali katika hali ya dhamiri zao kuwa hai na tayari kuujali ujumbe wake. Paulo alikuwa amemtia moyo Tito kutazamia mazuri iwapo bila shaka mwenyewe alikuwa na hofu kiasi fulani. Paulo alizidi kufurahi alipoona furaha ya Tito na matumaini yake kuzidi.

k.16 Paulo alizidi kuwa na moyo mkuu juu yao na moyo huo ulifanya ushirikiano kati yao kuwa wa ukaribu zaidi. Lakini moyo huo haukujengwa katika uzuri au uaminifu wa kibinadamu bali zaidi ulikuwa wa kiroho, ukiwa na msingi katika Injili na uwezo wake. Moyo wa namna hiyo ni kipawa cha Roho, na bila msaada huu huduma na kazi ya Injili ni nzito sana, ila kwa msaada wa Roho huduma hiyo huleta furaha ya ajabu.

Hali amemaliza maelezo hayo yote ndipo Paulo alileta mbele za waumini wa Korintho mambo mengine, ambalo mojawapo lilikuwa changizo, na sura za 8 na 9 zahusu hilo changizo kwa ajili ya Wakristo maskini wa Yerusalemu.

Wakati fulani Paulo alipokuwapo Yerusalemu shauri lilikatwa kwa yeye na wenzake kwenda kuhubiri Injili kwa WaMataifa na Petro na wenzake wahubiri Injili kwa Wayahudi (Gal.2:9). Si kwa lengo la kuanzisha makanisa mawili, la! Kanisa ni moja tu, na wahudumu wake wana wajibu juu ya Kanisa zima, ila kwa upande wa uenezi wa Injili Paulo ataelekea sehemu zilizo na WaMataifa wengi na Petro sehemu zilizo na Wayahudi hasa. Wakati huo, viongozi wa Kanisa walimwomba Paulo awakumbuke maskini katika huduma yake (Gal. 2:10). Paulo hakuwa na haja ya kuambiwa, maana tayari alikuwa na bidii hiyo.

Katika Kanisa walikuwepo watu walioitwa Mayahudishaji, watu waliosababisha shida nyingi kwa waumini wa Ki-Mataifa, wakisema kwamba imewapasa waumini wa Ki-Mataifa watahiriwe na kushika Torati wakitaka kuwa Wakristo kamili. Twakumbuka Baraza la Yerusalemu lilikutanishwa kwa kusudi la kukata shauri hilo (Matendo 15). Hao watu walimfuatafuata Paulo na kuleta fujo wakijaribu kuwazuia WaMataifa wasiamini. Pia katika makanisa walijaribu kuleta matengano kati ya waumini, na kueneza habari zisizo kweli. Hata changizo lilipoletwa Yerusalemu na wajumbe waliotoka makanisa mbalimbali ya Ki-Mataifa, Paulo alishtakiwa kwa uongo kwamba amemwingiza Mkristo wa Ki-Mataifa ndani ya Hekalu (Mdo.21:20, 21).

Paulo alipotafakari juu ya hali ya umaskini wa waumini wengi huko Yerusalemu, aliamua kufanya mpango wa makanisa ya Ki-Mataifa kuchanga msaada, halafu changizo hilo lipelekwe Yerusalemu na wajumbe kutoka makanisa hayo. Kwa njia hii alitaka kuukuza upendano na kujenga ushirikiano kati ya waumini wa pande zote mbili.

Sura za 8 na 9 zinaonyesha jinsi Paulo alivyokuwa na moyo mkuu juu ya changizo hilo akipenda sana waumini walioko Yerusalemu wapate nafuu katika hali yao ya kimwili, pamoja na ya kuuendeleza uhusiano mzuri kati ya makanisa yote.

Hivyo, makanisa walipewa habari za changizo na kuambiwa waliandae kwa muda ili baadaye likusanywe na mpango halisi wa kulipeleka litengenezwe. Mara kwa mara habari hiyo iliguswa katika barua za Paulo. Tukitazama 1 Kor.16: 1-3 Wakorintho walishauriwa kuwa na taratibu katika kutoa na Paulo aliwaambia ya kwamba amekwisha kuyaamuru makanisa ya Galatia kufanya vivyo hivyo.

Katika Waraka huo wa pili aliwaeleza juu ya maendeleo ya changizo katika makanisa ya Makedonia. Tunapotazama majina ya wajumbe wa kwenda Yerusalemu (Mdo.20:4) twakuta watu wa makanisa ya Asia wametajwa.

Pale Korintho changizo lilikubalika ndipo likasimama wakati wa matatizo yao mengi. Paulo hakuona vema kuwasukuma kwa sababu ya uhusiano mbaya uliotokea kati yao, kwa hiyo, iwapo walikuwa tayari kwa muda mrefu, sasa walihitaji kuhimiza jambo hilo au watakosa kufaulu kupata changizo zuri.

Polepole katika sura zilizotangulia Paulo alizidi kujenga uhusiano kati yake na wao mpaka tayari uhusiano ulikuwa mwema. Sasa yu tayari kusema juu ya changizo. Ilimbidi aseme kwa busara, maana alitaka wawe wakarimu, ila pia alitaka watoe kwa hiari na kwa kupenda.

8:1-7 <u>Changizo, kielelezo cha Wakristo wa Makedonia</u>

Paulo alianza kwa kuwaita “ndugu” na kuwapasha habari njema kuhusu Wakristo wenzao katika makanisa ya Makedonia waliounga mkono mpango wa changizo. Paulo alitaka Wakisto wa kila mahali waone kwamba wajibu wao ni kuishi kama familia moja wa Mungu Baba.

Katika k.1 Paulo aliita jambo hilo la changizo kuwa “neema ya Mungu”; baadaye katika k.4. alilliita “huduma”. Kwa nini ni neema? Ni kwa sababu ni sehemu ya neema ya Mungu ambayo Wakristo hushiriki na kuonja maishani mwao. Kwa neema changizo hilo litafanikiwa, si kwa bidii za kibinadamu tu, na wapokeaji watakuwa wapokeaji wa neema. Ni Roho Mtakatifu anayetia moyo wa kutoa kwa ukarimu na kwa kutaka, kwa sababu watakuwa wanatoa kwa watu ambao hawajawaona bado (Flp.4:13). Wale wenye kushiriki katika changizo hilo hupewa kipawa kutoka kwa Mungu; watakuwa wapokezi, si watoaji tu. Iwapo walipata hasara ya kiasi kile walichotoa, Paulo alifundisha kwamba watakapokuwa wameionja neema ya kutoa watataka neema zaidi ili watoe zaidi na zaidi. Ni tabia ya Mungu kutoa, na watoto wake, kwa neema yake hushiriki tabia hiyo.

k.2 Ndipo Paulo aliwaeleza juu ya makanisa ya Makedonia na jinsi ambavyo hayo makanisa kwa neema ya Mungu walitoa kwa ukarimu wa ajabu iwapo watu walikuwa maskini sana, tena walifurahi sana kufanya hivyo, hawakusikia shida yoyote. Neno “ukarimu” kwa asili lina maana ya “urahisi” unaosababisha unyofu wa moyo. Maana yake hao Wakristo walilenga kitu kimoja katika maisha yao na hali hiyo ya kukaza kitu kimoja ilitokeza ukarimu huo.

Kwa kuipenda sana Injili na kuikubali kwa moyo waliyashinda majaribu makali ambayo yangaliweza kuwapata kutokana na umaskini wao, majaribu ya kunung'unika na kukata tamaa, kuwa na mashaka juu ya wema wa Mungu, kuwaonea wivu wengine, na kufikiri hawana la kufanya. Waliona kwamba wakaze jambo moja tu, kutupilia mbali hali zote za kujihurumia na kujifikiria tu. Ni neema ya Mungu ndani yao iliyokuza hali hiyo ya kulenga kitu kimoja tu (Rum.12:8). Walijaribiwa vikali kwa sababu ya dhiki nyingi. Paulo hakusema hizo dhiki zilikuwa za namna gani ila alisema mambo mawili yalidhihirika kwa njia ya dhiki hizo, moja lilikuwa furaha yao nyingi na la pili, umaskini wao mwingi. Mambo hayo mawili yaliongeza ukarimu wao kuwa mwingi sana.

k.3-5 Hali yao iligusaje hilo changizo. Kweli, walitoa kwa changizo, ila kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana, neno la maana sana na pamoja na kujitoa kwa Bwana walijitoa pia kwa watumishi wake akina Paulo na wenzake (k.5). Hapo twaona jinsi ambavyo watumishi wa Bwana wamefungamana na Bwana wao. Hawakuweza kujitoa kwa Mungu na kutokumjali Paulo, wala hawakuweza kujitoa kwa Paulo kama mhudumu wa Injili bila kujitoa kwa Bwana kwanza.

Jambo lingine ni kwamba walitoa kupita uwezo wao kwa hiari yao na kwa kutaka. Pengine Paulo alijaribu kuwashauri wasipite mpaka, akijua hali yao mbaya, lakini wao walimwomba waruhusiwe kufanya kwa ukarimu kama walivyokusudia. Tukisoma k.4 twapata maneno “wakituomba sana” “na kutusihi”, kwa kweli walitamani sana kushiriki katika hilo changizo, wala hawakutaka umaskini wao kuwa sababu ya kuwazuia.

Walihesabu hilo changizo si mzigo waliotwishwa, ila ni njia ya kutajirika kiroho, wakipewa neema, na neema ilizidi kwa kadiri walivyoendelea kutoa. Ni ujuzi mpya wa kiroho, na hali mpya ya kuionja “neema” kwa namna hiyo. Bila shaka walijisikia wako karibu zaidi na ndugu zao wa Yerusalemu. Wameingizwa ndani zaidi katika shirika la watakatifu. Changizo ni dhihirisho la “shirika”, ndugu wengine wakitoa na ndugu wengine wakipokea kufuatana na hali zao. Kupokea na kutoa kuwe katika msingi wa kuwaza “shirika”.

Ni wazi kabisa kwamba hao Wakristo wa makanisa ya Makedonia walizidi matazamio ya Paulo. Katika Makedonia yalikuwepo makanisa ya Filipi, Thesalonike na Beroya. Makanisa hayo yalionekana kuwa makanisa imara, na bila shaka Paulo alijua wataitika vizuri wito wa kufanya changizo, hata hivyo waliitika kuliko alivyotazamia.

k.6 Kwa nini Paulo alitaja hayo yote kwa Kanisa la Korintho? Alitaka Wakorintho pia waionje “neema hiyo”, watajirike kiroho kwa njia ya kutoa kwa ukarimu. Alitaka wathibitishe nia yao kwa kutekeleza mipango waliyokuwa wameandaa kama mwaka mmoja uliotangulia, mipango iliyosimama kwa sababu ya matatizo yao. Kwa hiyo, Paulo alimwomba Tito aende tena kuonana nao. Yeye Tito, daima alikuwa akiwakumbuka, na ni yeye aliyewasaidia wakati wa shida zao. Sasa atakwenda kuwasaidia kuhusu changizo ili walikusanye haraka, kwa vile wako nyuma ya makanisa mengine. Si kwamba hawakutaka kuchanga au kwamba walikosa uwezo, la. Paulo aliona kwamba wamekuwa na imani, usemi, elimu, bidii, na upendo kwa wingi, naye alitaka wawe na “neema” hii ya utoaji kwa wingi ili waionje baraka za kiroho zaidi na zaidi.

8:8-15 <u>Sababu kuu katika Utoaji wa Kikristo</u>

Paulo hakutoa amri, ila iliyopo ni kwamba kwa njia hii ataweza kuupima upendo wao na kuulinganisha na makanisa mengine. Ni nafasi njema kwao kuuhakikisha ukweli wa upendo wao.

k.9 Aliwakumbusha kielelezo cha Bwana Yesu ambaye kwa ajili yetu, alikubali kuondoka mbinguni penye utajiri wa ajabu, na kuja duniani na kuishi kama maskini. Kwa njia hiyo, sisi tumepewa ahadi za kuushiriki utajiri wa mbinguni, na kwa umaskini wake sisi tumetajirika. Kila Mkristo ameionja neema hii ya Bwana Yesu.

k.10-12 Aliwashauri kutimiliza neno hilo la changizo kama neno linalofaa. Watoe kulingana na uwezo wao, mtu alicho nacho kingi na atoe kingi, aliye nacho kidogo, na atoe kidogo, maana Mungu ajua hali na uwezo wa kila mtu, kiasi si kitu. Mbele za Mungu neno la maana ni unyofu wa moyo wa kutoa kwa furaha. Hakuwashauri watoe kupita uwezo wao kama ndugu wa Makedonia walivyofanya. Ni hiari ya mtu si sheria.

k.13-15 “Usawa” ni katika watu wa hali zote kushiriki, na kwa kanuni ya kadiri ya alivyo navyo mtu. Usawa si wa kipimo ila ni katika wote kujiunga. Kwa wakati huu Wakorintho hawakuwa na shida, na huko Yerusalemu ndugu zao walikuwa na dhiki ya kukosa riziki. Kwa hiyo Wakorintho watoe, na watu wa Yerusalemu wapokee, ndipo hali zao zitasawazishwa. Wale wa Yerusalemu watapata faida ya kimwili, na Wakorintho faida ya kiroho, na wote watasikia kuwa na ushirikiano mwema. Tukumbuke mkazo wa Paulo juu ya changizo kuwa neno la neema ya Mungu. Katika dunia watu husaidiana (Lk.6:34) lakini Wakristo hawafanyi kwa lengo la kurudishiwa kitu.

Katika k.15 Paulo aligusa habari ya zamani wakati wa watu wa Mungu kulishwa jangwani. Hata zamani “usawa” ulionekana katika kutolewa kwa chakula cha pekee, cha mana (Kut.16:18).

8:16-24 Tito na wawili wengine kwenda Korintho

Tito alikuwa amekolea sana mawazo ya Paulo juu ya changizo kuhusu neema ya Mungu na baraka zitakazofuata utoaji wa kweli. Kwa kuwatembelea wakati wa shida zao amesikia mzigo sana juu yao, na uhusiano mzuri umejengwa nao. Lakini hali hiyo imeanza kwa Mungu, ni Mungu aliyemtia bidii ya kuwapenda Wakorintho na kuwashughulikia na Paulo alimshukuru Mungu kwa jambo hilo. Tito alikuwa tayari kuwaendea tena, alikuwa na shauku juu yao akitumaini atafaulu kuwasaidia katika neno la changizo, kama alivyowasaidia hapo nyuma katika matatizo yao.

k.18 Wawili watakwenda pamoja naye. Paulo aliona vema awaeleze sifa za hao wawili, kusudi wasimwelewe vibaya juu ya kuwatuma. Kwa hiyo, ni nani na nani wa kwenda? Mmoja ni ndugu aliyejulikana sana katika makanisa, ndugu mwaminifu, mwenye uwezo na sifa nzuri, na Paulo aliona ya kuwa hata Wakorintho watafurahi kumpata.

k.19 Paulo aliendelea kutoboa habari za huyo ndugu. Yeye si mgeni kwa kazi ya Mungu, naye alichaguliwa na makanisa kusafiri pamoja na akina Paulo kuhusu jambo la neema hii, yaani changizo. Bila shaka ni mjumbe mmojawapo atakayepeleka changizo mpaka Yerusalemu. Nani huyo? Pengine ni Mkristo wa Makedonia.Katika Matendo 20:4 tumepewa majina kadha; Soprato wa Beroya; Aristarko na Sekundo wa Thesalonike, (Mdo.19:29). Aristarko alikuwa na Paulo mara nyingi labda ni huyo. Twajua kwamba Luka pia alikuwa pamoja nao. Katika 1 Kor.4:4 ni wazi kwamba changizo limeendelea sana ila Paulo alikuwa bado hajakata shauri la kwenda Yerusalemu pamoja na wajumbe. Sasa twaona kwamba Paulo amekata shauri la kwenda, na makanisa mengi wamekwisha kuwachagua wajumbe wao, hivyo Wakorintho wapaswa wafanye haraka.

k.20 Lengo ni kumtukuza Mungu na mambo yote yawe nuruni ili wasishtakiwe kwa uongo kuhusu changizo ili wajiepushe na lawama. Tukiuliza “ni lawama gani?” iwapo kwa sehemu itakuwa lawama la kula fedha za changizo, ndiyo sababu litapelekwa na wajumbe wa makanisa mbalimbali. Ila, pia, lengo la changizo lionekane wazi, ambalo ni kuujenga ushirikiano kati ya waumini wa Kiyahudi na waumini ya Ki-Mataifa. Paulo hakutaka wale wa Yerusalemu wawaza neno hilo kuwa la Paulo binafsi, bali alitaka watambue kwamba ndugu zao, Wakristo wa Ki-Mataifa wamekubali kabisa kwa moyo kujiunga katika changizo. Yote yawe sawa na wazi mbele za Bwana na watu pia.

k.22 Mwingine atakwenda na Tito pamoja na yule mwingine aliyetajwa hapo juu. Mtu aliye na sifa zilezile, mtu aliyeaminika sana na Paulo, mtu mwenye bidii na mzigo, mtu mwenye upendo mwingi kwa hao Wakorintho akiwatumaini watajiunga naye kuhusu neno la changizo. Paulo hakutaja jina lake.

k.23 Ndipo Paulo alisisitiza sifa za Tito na wale wawili watakaokwenda. Tito ni mjoli wake kikazi, mmoja aliyekuwa karibu naye katika huduma ya Injili. Wale wengine wameitwa “mitume wa makanisa na utukufu wa Kristo”. Paulo alitaka wakaribishwe kwa upendo ili makanisa yote yafahamu kwamba kanisa la Korintho halitaki kujiongoza, bali ni tayari kufuata desturi na mapokeo yanayofuatwa katika makanisa mengine (1 Kor.4:17; 7:17; 11:16; 10:32; 14:36). Hapo nyuma hali hiyo haikuonekana. Tito atakuwa badala ya Paulo na kiongozi. Wale wawili ni wajumbe wa makanisa yao na kwa sababu ya maisha yao na utumishi wao mzuri, Kristo ametukuzwa.

k.24 Paulo hakutaka zile sifa ambazo amewasifia Wakorintho mbele za makanisa ziwe bure au zionekane kuwa si kweli. Bila shaka waumini katika makanisa mengine wamehuzunishwa na hali ya Wakorintho hapo nyuma. Sifa zake juu yao zikithibitishwa kuwa za kweli basi, makanisa mengine yatatiwa moyo, na mitume wa uongo watapunguzwa nguvu.

9:1-5 <u>Sababu ya kuwatuma</u>

Paulo alikuwa na moyo mkuu juu ya Wakorintho kwa sababu kama mwaka uliopita walionyesha utayari wao wa kujiunga na makanisa mengine katika changizo. Utayari wao uliwatia Wakristo katika makanisa mengine kuwa na moyo wa kuchanga. Alikuwa amefundisha kwamba hilo changizo si changizo tu, bali ni njia ya kuujenga uhusiano mwema kati ya makanisa, pia ni kupimo cha kupimia jinsi waumini wanavyothamini jambo la ushirkiano. Tena ni njia ya kuleta “usawa” katika hali zao.

Kwa nini hao watatu waende Korintho ikiwa Wakorintho walikuwa na moyo mkuu hapo nyuma? Ni kwa sababu ya matatizo makubwa yaliyotokea. Matatizo hayo yalisababisha neno la changizo kuachwa kwa muda, pia uhusiano wao na Paulo ulikuwa mbaya. Kwa hiyo baada ya kuzitengeneza shida zao, na baada ya uhusiano wao na Paulo kuwa mzuri, basi wamejikuta wako nyuma ya makanisa mengine kuhusu hilo changizo. Bidii nyingi ilihitajika na kwa msaada wa hao watatu Paulo alitumaini kwamba watafaulu kuchanga tena watachanga vizuri.

k.4-5 Paulo mwenyewe atakuja kwao, pamoja na wajumbe wa makanisa ya Makedonia, kwa hiyo, kwa busara aliwatuma hao watatu, kusudi atakapokuja pamoja na wale wajumbe, watakuta changizo ni tayari, hivyo, wao wenyewe hawataaibika, wala Paulo na wenzake. Hao watatu watawasaidia waumini kutimiza ahadi waliyoahidi mwanzoni, tena watawasaidia kuwaza changizo kuwa kipawa na karamu ili wasiwe wanyimavu.

9:6-15 <u>Kutoa kwa ukarimu na kuvuna kwa ukarimu</u>

Paulo aliendelea kuzungumzia changizo kwa kuutumia mfano wa ulimaji. Alifananisha kutoa kwa changizo ni kama kupanda mbegu, na kwa vyovyote mpandaji wa mbegu hufanya katika tumaini la kuvuna mbeleni.

Upo uhusiano mkubwa kati ya kupanda na kuvuna, na kwa sababu hiyo mpandaji huangalia sana kupanda kwake. Anafahamu kabisa kwamba akipanda kwa haba hawezi kuvuna kwa wingi. Lakini kwa upande wa changizo kiasi ni jambo moja tu katika habari nzima ya utoaji, maana kiasi chafuatana na uwezo wa mtu. Mtu atapanda kwa haba kama atasitasita katika kutoa kwake, au kama atatoa kwa moyo mzito au kwa lazima. Kupanda kwa ukarimu ni kutoa kwa ukunjufu wa moyo na kwa hiari. Hivyo ni juu ya mpandaji kuchagua kupanda kwa haba au kwa ukarimu.

Lakini katika jambo la changizo kwa sababu ni jambo la kiroho mavuno hutegemea Bwana na baraka zake. Mpandaji huutumainia wema wa Bwana. Paulo alitaka kuamsha hali hiyo ya kumtumaini Bwana. Mbegu hazipotei zinapotupwa ardhini, la, ni njia ya kuzihuisha. Changizo si njia ya kupotewa na fedha, la. Si hesabu inayowekwa katika upande wa “kutoka” kwa fedha, la. Ni mfano wa fedha zilizowekwa kwa riba, ili faida ipatikane (Gal.6:7). Hata hivyo, mtoaji atoe tu bila kuwaza thawabu au kustahili kwake, bali awaze kuwa njia ya kuionja neema ya Mungu kwa wingi. Wakumbuke ya kuwa wamejaliwa kupata Injili, na katika mwaka uliopita Mungu amewapitisha katika shida nyingi na kuwapa ushindi wa kiroho.

k.7 Kumlazimisha mtu au kumshawishi ni vibaya. Budi wafanye kwa hiari, kila mtu aamue mapema kulingana na imani aliyo nayo. Wenzake waweza kushauri, kuonya, kusihi, na kutia moyo ila mwishowe ni kati ya muumini na Bwana Yesu. Waepukane na hatari mbili; hatari ya kufanya kwa huzuni, na hatari ya kufanya kwa lazima. Je! yupo mpandaji ye yote anayesikitika kwamba amepoteza mbegu zake ardhini? La! yeye hufurahi kwamba alikuwa na mbegu za kupanda. Tunafahamu kwamba katika nchi nyingi watu hutegemea kilimo sana, na kama mtu atakosa mbegu za kupanda kwa vyovyote atazitafuta kwa bidii, hali akiwa tayari kuzikopa kwa ndugu zake, au hata kukopa fedha za kuzinunua. Vivyo hivyo Mkristo apaswa kuuwaza utoaji.

Akitoa kwa huzuni kipawa chake kimeguswa, ni kama hakutambua neema ya Mungu iliyomwezesha kutoa, na nia yake haikuwa safi, huenda amenyang"anyia mali ya hapa duniani. Pengine ni kwa sababu hakutia maanani ushirikiano wake na wengine na kuona ushirikiano huo si kitu. Akiwa na mawazo hayo kweli atatoa kwa huzuni.
Kwa njia gani atatoa kwa lazima? Kama akiwekewa kima fulani na ndugu zake; au pengine kwa kumwogopa Mungu, (kuogopa si sawa na kumcha), akifikiri kwamba asipotoa vizuri Mungu atamkasirikia; au pengine atasikia

kulazimika kwa sababu, eti! fulani ametoa kiasi fulani. Hali hizo zote ni kama vibano vya kumfanya atoe kwa “lazima” kumbe! kipawa chake kimeguswa.

Mungu hupenda mtu atoe kwa moyo mkunjufu, moyo wa kutoa ni muhimu kuliko kiasi kinachotolewa. Ni vema kukumbuka kwamba Mungu hahitaji vipawa vyetu (Zab.50:12). Mungu hana haja ya kuomba kitu chochote. Anao uwezo wa kuwahifadhi wote, ila apenda kuwapa watu nafasi ya kushirikiana naye katika kuwapatia watu mahitaji yao. Kwa njia hiyo wamepata nafasi ya kuonyesha maisha yao mapya katika Kristo, na upendo wao kwa ndugu zao, na shukrani zao kwa Mungu. Nafasi za utoaji zatokana na neema ya Mungu, kwa hiyo, wazitumie kwa ukunjufu wa moyo (Mit.22:8). Mungu Mwenyewe hutoa kwa moyo mkunjufu (Yak.1:5,17). Tukumbuke ya kwamba kile tunachotoa ni kile ambacho Mungu ametujalia kupata (Mdo.20:35).

k.8 Mungu humpenda sana na kumbariki sana mtoaji mkarimu. Je! Mungu anao uwezo wa kutupa neema ya kutoa kwa ukarimu? Jibu ni ndiyo. Ikiwa Yeye amewahi kutuokoa, na kugeuza mioyo yetu, si neno gumu atujaze neema ya kuzidi kutoa. Paulo alisema kwa uhakika “Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna sikuzote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema” (1 Kor.14:7- 2 Kor.8:7).

k.9 Paulo alitumia kifungu cha Agano la Kale kuonyesha kwamba hata tangu zamani neno hilo limekuwapo (Zab.111 na 112; Mit.11:24). “Kutapanya” ni kutoa kwa maskini, na mavuno yake ni kuhesabiwa haki kwa imani.

k.10 Ni Mungu anayetoa mbegu, na ni Mungu anayezibariki. Vilevile kwa changizo, Mungu atalitokeza, na Mungu atalibariki. Mungu ni Mpataji wetu anayetupatia. Kwa hiyo atawapatia ya kutosha kuwafanya wawe watoaji wakarimu. Wale wa kutoa ni wenye dhambi waliohesabiwa haki bure kwa neema, na matunda ya haki hiyo ni moyo mkarimu.

k.11 Watatajirika hali wakilenga kitu kimoja tu; wasikubali kuvutwa upande na mambo mengine, ndipo Mungu atashukuriwa.

k.12 Kilicho mbele yao ni kuchanga msaada kwa Wakristo wenzao walio maskini huko Yerusalemu. Lakini, kama ambavyo tumekwisha kuona si hivyo tu. Paulo alikuza jambo lenyewe kuwa jambo la kiroho, ni “huduma”. Kwa ndani kabisa jambo linalotafutwa ni Mungu apewe shukrani nyingi na watu wengi. Sifa za Mungu zikuzwe.

k.13 Paulo aliona hilo changizo ni kama mtihani wa kupima nia zao, lengo lao, na jinsi wanavyothamini ushirika wa watakatifu. Wakiufaulu huo mtihani wataonekana kuwa waumini wa kweli. Itajulikana kwamba wameikiri Injili ya Kristo na kujiweka chini ya nguvu zake, wakiishi maisha mapya na kufuata ile

njia mpya ya kuishi kwa upendano katika ulimwengu wa sasa. Mtu hawezi kuikiri Injili huku anakana ushirikiano wa watakatifu. Ni ushirikiano wa Ki-Injili usiojali rangi na kabila za watu, ni ushirikiano unaoruka viambaza vyote vinavyowekwa na wanadamu.

Wakorintho hawatakuwa watoaji tu. Kwa sababu ni jambo la kiroho, hao Wakristo wa Kiyahudi wataziitikia fadhili za watoaji kwa kuwaombea Wakorintho kwa moyo na kuwa na mzigo juu yao, mioyo ya wote itakaribiana, wakitaka sana hao Wakorintho wapate baraka za Mungu (Yak.5:16 Mt.18:19- 20). Kwa njia hiyo Mungu atazidi kushukuriwa maana itatambulikana na wote kwamba asili ya yote ni katika Mungu na neema yake. Kipawa hicho hakina mfano wake hapa duniani wala hakielezeki nje ya Mungu na neema yake. Atakayeshukuriwa ni Mungu peke yake.

MASWALI:

6:14-7:1 Kwa nini Wakristo wajitenge na wasioamini?
Wajitenge katika mambo gani?
Katika mawazo yako kuna desturi gani ambazo Wakristo hupaswa kuziacha?
Je! Kanisa la leo linakaza utakatifu wa maisha au vipi? Zungumza habari hiyo.

7: 2-16 Pasipo kuaminiana Je! kazi za Injili zitafanikiwa?
Kwa njia gani uhusiano mwema unajengwa?

Sura ya 8 na 9: Jumlisha mambo makubwa katika Utoaji wa Kikristo. Toa mawazo kuhusu hali hiyo katika makanisa yetu.

SURA YA 10 HADI 13 - MAMLAKA YA KI-MITUME YA PAULO

Katika sura hizo za mwisho hewa na lugha ni tofauti na sura zilizotangulia. Katika sura hizo Paulo amejieleza na kujitetea kwa kirefu juu ya mabadiliko ya mipango yake ya safari na kukaza kwamba iwapo alikuwa amebadili mipango hiyo siyo kusema kwamba amezibadili kweli za Injilii anayohubiri.

Kwa nini aliiahirisha safari? Ni kwa sababu ya kuwahurumia Wakorintho. Katika kujitetea, kwa nini aliukaza uzuri wa Agano Jipya kuliko Agano la Kale na kuwashtaki kwamba wanaposoma Agano la Kale ni kama wamevaa taji? Kwa nini changizo limechelewa? Kwa nini Paulo aliwaelezea kwa uangalifu sana juu mpango wa wazee kulibeba changizo mpaka Yerusalemu?

Sehemu hiyo ni kama utetezi, akijitetea na kuandika kama imemlazimu afanye hivyo kwa ajili ya Injili. Si kwamba alipenda kufanya hivyo, ila kwa usalama wa kiroho wa Wakorintho aliona ni lazima (5:12).

10:1-6 <u>Silaha ya Vita ya Kiroho</u>

Alianza kwa maneno „mimi Paulo" hapo nyuma ameandika kama ni yeye na Timotheo, hivyo inaonekana kwamba sehemu hiyo yamhusu yeye hasa iwapo hata wasaidizi wake hawakuachwa kulaumiwa, ndiyo sababu neno "sisi" imetumiwa pia (k.2).

Ameanza na ombi kwao, na kuliweka katika msingi wa "upole na utaratibu wa Kristo". Hali hizo si kigeni kwao, maana wamezijua katika kuongoka kwao na pia katika kujirekebisha kwao na katika kurudia hali njema baada ya matatizo yao. Neno la maana ni kwamba wanaye Kristo. Mayahudishaji waliowasumbua walishambulia maisha yao ya Kikristo (Gal.5:4). Hasa walimshambulia Paulo, huenda maneno ambayo yametumika hapo ni mfano wa maneno waliyotumia, na Wakorintho walikuwa tayari kuyasikiliza na kuyakubali.

Paulo alikuwa mnyenyekevu, alinyenyekezwa sana sana Yesu alipokutana naye njiani kwenda Dameski. Ni Yesu mpole aliyemshinda, kwa hiyo maishani mwake alikubali kuwa mpole na kuishi kwa utaratibu wa Kristo. Iwapo alijitahidi na kutumika zaidi ya Mitume wote, alijihesabu ni mdogo kupita wote hata alisikia shida ya kujiita Mtume. Alijaribu kujiweka mahali pa watu, kwa wanyonge alikuwa kama mnyonge. Kwa Wakristo wapya alionyesha tabia ya ki-mama, kama mlezi mpole na kuwa „baba wa kiroho" kwa waumini wengi (1 Thes. 2: 7, 11). Haikuwa rahisi kuwa hivyo kwa sababu kwa tabia ya asili alikuwa mtu wa haraka, mkakamavu, na hodari. Hakuwa mjanja. Alifanya yote kwa ajili ya Injili. Hata kwa Wakorintho wenye matatizo mengi alikuwa mpole, na washtaki wake waligeuza upole huo na kusema ni woga. Walisema kwamba, anapokuwa mbali, Paulo huwa mjasiri, ila akiwa karibu anaogopaogopa. Alijibuje hayo mashtaka? Aliwaambia kwamba washtaki wake wataona ujasiri wake, ila hakutaka wote waingizwe, ila wale tu waliohusika.

k.2 Inaonekana hao watu waliowasumbua waumini walikuwa wangaliko huko Korintho, na Paulo alisema kwamba itambidi awakabili pamoja na wale Wakorintho waliojiunga nao. Hatamhurumia yeyote aliyesababisha shida, haidhuru ni mtu wa nje au mtu wa ndani. Aliamini kabisa kwamba katika uwezo wa Injili hakuna atakayeshindana naye na kumshinda. Hatua atakazozichukua zitapatana na Injili na uwezo uliomo katika Injili utamaliza upinzani wote. Iwapo katika huduma ya Injili mateso ni sehemu mojawapo, hata hivyo yu katika maandamano ya ushindi na Kristo ndiye kiongozi wake (2:14).

Kwa vyovyote Paulo atawashambulia hao waliokuja Korintho kutoka nje wakiwa na lengo la kutikisa imani ya kweli ya waumini wa pale, lakini hapendi hata muumini mmoja awemo pamoja na hao wengine. Adui zake walisema kwa uongo kwamba Paulo alikuwa akitafuta faida yake, na ya kuwa alitumia hekima

za dunia, na ni mtu dhaifu. Kumbe! hawana habari ya tabia za Kristo, ya upole na utaratibu, tabia zilizomtawala Paulo.

k.3 Hata hivyo Paulo angali katika mwili (4:7) hazina ya Injili imo katika chombo cha udongo.Vita ya kupigania Injili haifuati kanuni za hapo duniani. Vita hiyo imo mikononi mwa Mungu. Kama angalitegemea ujanja na nguvu zake asingaliweza vita hiyo.

Katika vita ya Injili silaha zatoka kwa Mungu. Silaha za kujilinda na silaha za kushambulia. Mtu hawezi kufaulu kwa mazoea, bali ushindi watoka kwa Roho Mtakatifu (Mt.10:19). Silaha za kiroho zina uwezo wa Mungu, na wanadamu hawana uwezo huo. „Kuangusha ngome" ngome zinajengwa na tawala za dunia kwa shabaha ya kulinda mipaka ya utawala wao na kuwazuia adui wasifaulu kuuondoa huo utawala. Lazima hata adui za Injili ambao pia ni adui za Mungu waangushwe. Lakini ngome hizo ni za namna gani? Tazama 1 Yoh.2:15-17: Rum.10:2. Ngome moja ni kiburi cha maisha. Wayunani walijiona sana kwa sababu walikuza mambo ya falsafa, mashairi, uchongaji na ujenzi mstadi n.k. Kwa upande wa dini twakumbuka hali ya Waathene jinsi walivyoabudu sanamu za kila aina. Walipenda kusikia mawazo ya wasomi, na kutegemea elimu za ki-binadamu, wakitafuta kujipatia haki kwa njia hizo (Mdo.17:34).

k.5 “kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya Elimu ya Mungu” Shetani hujengea ngome za namna hiyo ili wanadamu wawaze makuu na kwa njia hiyo wajione kuwa na uwezo wa kutosha, wasisikie haja ya msaada wa neema ya Kristo. Kazi moja ya Paulo kama mtumishi wa Kristo ilikuwa kushambulia “ngome hizo” za uongo wa Shetani zilizowadanganya watu.

“Elimu ya Mungu” ni nini? Tukitazama Yeremia 3l:34 ni ujuzi wa msamaha wa Mungu (Lk.1:77; Yn.17:3) ni mtu kukutana na Mungu nafsini mwake. Shetani hushindwa na mtu aliye na ujuzi huo maishani mwake, maana yake anamjua Mungu. Ngome ya Shetani hutikiswa na utawala wake juu ya yule mtu hutoweka. Hivyo Injili imefaulu na utumishi wa Paulo umefanana na mtu wa kuteka nyara.

k.6 “kupatiliza maasi yote” pengine Paulo alikuwa na maana ya kulipiza kisasi au kurekebisha. Shabaha yake ilikuwa kwa wale watu kutubu, na wasipotubu Shetani amewapata kwa kutokutii kwao. Hivyo alitaka Wakorintho wawe na utii. Kwa hiyo ilionekana kwamba pale Korintho hazikuwapo hali nzuri. Mitume wa uongo waliwafikia, wakaitikisa imani yao, wakiingiza mawazo yasiyopatana na Injili. Haja kubwa ya Wakorintho ilikuwa ya kurudia mawazo na hali zilizopatana na Injili. Ikiwa watakubali kurudishwa Paulo hatakuwa na haja ya kuwashughulikia zaidi, atakuwa huru kueneza Injili mahali pengine, na wao wataweza kumsaidia kufanya hivyo.

10:7-11 <u>Paulo hakuwa na kigeugeu</u>

Twajua Tito alikuwa amemletea Paulo habari njema juu ya Wakorintho. Shida zao zilikuwa zimepungua na ilionekana kwamba hatari imepita hali wakiendelea kujirekebisha; hata hivyo walihitaji kutunzwa kiroho. Mitume wa uongo walikuwa hawajaondoka bado, na baadhi ya waumini waliwajali na kuwasikiliza. Paulo alitambua kwamba itakuwa vigumu wale waumini wawe salama kabisa mpaka hao mitume wa uongo wameondoka. Kila Mkristo alijiona kuwa Mkristo wa kweli kwa kuwa amemwamini Kristo. Ikiwa wao wenyewe walijiona ni Wakristo wa kweli, vivyo hivyo, walipaswa kukubali kwamba hata wale waliowaletea Injili ni Wakristo wa kweli pia. Kama sivyo, mbona waliwaletea Injili? Mitume wa uongo walisema kwamba Paulo hakuwa Mtume halisi, wao wamempita. Kumbe! wamempitaje? Wao hawakuleta Injili kwao wala penginepo. Tabia yao ilikuwa kungoja mpaka kanisa limetokea mahali fulani, ndipo kazi yao ilikuwa kuwafikia waumini waliopatikana na kuwashawishi kinyume cha walivyofundishwa na Paulo na wenzake. Imewapasa kufikiri kidogo na kutambua kwamba Paulo na wenzake ni watumishi kweli wa Kristo, na ya kuwa bila huduma yao wao wenyewe wasingalikuwa Wakristo.

k.8 Paulo aliweza kusema “sisi ni wa Kristo” tena aliweza kudai zaidi ya hilo kutokana na mamlaka aliyopewa na Kristo, ila kwa wakati huo hatadai mengi. Alijua kwamba adui zake walimshtaki kwa Wakorintho kwa kusema kwamba Paulo akiwa mbali huwa hodari bali akiwa karibu, sivyo alivyo. Basi aliona asiongeze madai maana watayakamata na kuyatumia vibaya. Bila shaka ni madai ya kuwa Mtume halisi mwenye mamlaka ya Mungu (Gal.1:1; 2 Kor.12:12). Alipewa mamlaka ya kujenga si ya kubomoa, na hicho kipawa alipewa na Yesu Kristo Mwenyewe. Mitume wa uongo walibomoa imani ya kweli, walibomoa kilichojengwa na Paulo. Paulo alipewa mamlaka ya kubomoa ngome za Shetani, si imani ya kweli ya watu. Wengi walionekana kuwa wajinga kwa jinsi walivyojisifu. Paulo hawezi kuonekana hivyo kwa sababu Wakorintho ni mashahidi wa kuthibitishia kazi yake. Iliwapasa kuifurahia mamlaka yake.

k.9 Angaliweza kutumia mamlaka yake ya Ki-Mitume kwa kuwaogofya ila watakapokumbuka msaada walioupata kwake wangalifurahi badala ya kuogopa. Ni kweli kwamba anapokuwa pamoja nao ni mpole, ila akiwaandikia barua kwa mbali yeye ni hodari na anajisifu sana. Iliyopo ni kwamba Paulo huwa mpole kwa wale dhaifu ki-imani, ila kwa mitume wa uongo ni mkali sana (k.11). Hasa ni washtaki wake waliosema kwamba barua zake ni kali, ila kwa kuonana naye uso kwa uso ni kama mtu dhaifu, asiye na uvutiko, ambaye watu humdharau na kutokumjali. Paulo aliwaonya wasidanganywe na maneno kama hayo, yeye wa barua kali ni yule wa kufika kwao, hamna tofauti, na atakapofika na kukuta hali zao ni mbaya, basi, watauona ukali wake.

10:12-18 <u>Kazi na eneo la utumishi aliopewa na Mungu</u>

Paulo aliwashambulia mitume wa uongo. Yeye alikataa kujilinganisha na watu wasiochoka kujisifia uwezo wao na kazi zao. Kwa uzuri wao, hata Yesu alipaswa kuwashukuru!!!

Walikuwa na nini hata wajisifu sana? Kipimo chao ni wao wenyewe kwa hiyo, si ajabu wafikia mia kwa mia. Kwa nini Wakorintho hawakuwatambua? Polepole Paulo alijaribu kuwafunulia hali yao halisi.

k.13 Ikiwa Paulo alikataa kujilinganisha na wengine atatumia kipimo gani katika kuipima kazi yake? Alisema atatumia kipimo cha Mungu, nacho ni katika kuileta Injili kwao, wala si kwao tu, hata penginepo pia. Popote palipo na sharika ya Kikristo ni thibitisho la kazi yake. Yeye hakuacha kuhubiri hata kwa mateso na dhiki, akifukuzwa mahali fulani alikwenda mahali pengine na kupanda Kanisa. Wale mitume wa uongo hawakufanya hivyo. Ulimwengu u mpana hata kwa wao kuipeleka Injili mahali papya!!!

k.14 Ni nani aliyewaletea Wakorintho Injili kwa mara ya kwanza? Ni Paulo aliyekuwa wa kwanza, analo la kujisifia kweli mbele za Mungu. Je! hao mitume wa uongo wanalo neno kama hilo la kujisifia? Paulo alitaka waumini wa Korintho watambue kwamba kipimo cha Paulo ndicho kipimo cha kweli kwa upande wa kujisifu. Kwa kukubali kipimo hicho watatiwa nguvu ya kuwapinga mitume wa uongo, na kwa moyo kuirudia Injili ya kweli iliyohubiriwa na Paulo kabla ya kufika kwa hao mitume wa uongo, ndipo uhusiano wao na Paulo utakuwa mwema.

k.15-16 Itakapokua imani yao, Paulo atakuzwa machoni pao. Paulo alitamani sana wakue kiroho kwa kadiri watakavyojaliwa na Mungu. Ndiposa tokeo litakuwa katika Paulo kuipeleka Injili kwa nchi zingine hata mpaka Spania (Rum.18:23). Alitazamia kwamba Wakorintho wataweza kumsaidia kufanya hivyo. Kwa mawazo hayo Paulo alionyesha ya kuwa alitazamia watatoka kabisa katika matatizo yao. Itakuwa vigumu akazane na mipango ya namna hiyo mpaka mitume wa uongo wameshindwa na kuondoka Korintho, na haitatokea hivyo mpaka Wakorintho wenyewe wamegundua hila zao, na kuona kwamba kujisifu kwao ni bure, kumekosa msingi wa kweli. Watamsaidiaje? kwa maombi pia wawe kituo, mfano wa Antiokia wa Shamu, mwanzoni wa uenezi wa Injili (Mdo.13n.k).

k.17 Mitume wa uongo walidai sifa katika mambo yasiyostahili sifa. Sifa yote ina nani hasa? Ni ya Bwana, hata Paulo hakustahili sifa, ila kwa kuwaza kwa namna ya kibinadamu, ilikuwa haki apewe sifa. Ni Mungu aliyemchagua na kumweka katika kazi za Injili, vipawa vyake vilitoka kwa Mungu, na ni Mungu aliyemtia moyo na nguvu (1 Kor.15:10).

k.18 Kwa kweli Paulo hakutaka kujisifu ila kwa sababu ya hali ya Wakorintho ilimbidi ajilinganishe na hao wengine kwa kusudi la kutoboa wazi tofauti zilizopo kati yao. Wakati wote alifahamu mafanikio yote ya Injili ni ya Bwana si yeye.

11:1-6 <u>Paulo aliwadai Wakorintho utiifu</u>

Hakuna faida katika kujisifu, ni bure. Sifa itoke kwa Bwana ndipo ni halali. Paulo alifuata kanani hiyo kama msingi wa huduma yake.

Hakupenda kusemasema juu ya uzuri wake, alipenda zaidi kusema juu ya udhaifu wake. Ila aliona ni lazima auvunje ule uhusiano baina ya Wakorintho na mitume wa uongo waliowaloga Wakristo kwa kusema sana sifa zao. Ni kama alisikia kulazimishwa kujisifu ingalau kwa muda mfupi, na hata hivyo alisema ni "ujinga" kufanya hivyo. Ikiwa ni "ujinga" kwa Paulo kujisifu, si zaidi kwa mitume wa uongo wasio na mambo mazuri ya kujisifu?

k.1 Aliomba "wachukuliane naye" maneno hayo ni dalili ya jinsi asivyopenda kujisifu, na hapa nyuma hajafanya hata kwa mara moja.

k.2 Aliwaonea wivu sana waumini wa Korintho, wivu sawa na wivu wa kweli alio nao Mungu. Wivu wa kuleta watu kwa Kristo ili wawe mali yake na watiifu Kwake. Wivu unaofanana na wivu wa mtu anayemwinda msichana fulani kuwa mke wake!! na baada ya kumwoa hamruhusu mwingine aingie kati yao. Alitaka sana sana wawe waaminifu kwa Mungu, hakutaka jambo lo lote liingie kati na kuuharibu uhusiano wao.

k.3 Paulo alianza kusikia hofu juu yao. Alifananisha hali yao na Hawa alipojiwa na nyoka Bustani ya Adeni. Kabla ya kuja kwa nyoka Hawa alimpenda Mungu akawa mwaminifu, lakini nyoka alikuja kwa hila na ujanja akamvuta amwasi Mungu, ndipo uhusiano wake na Mungu ukaharibika. Na Shetani hufanya vivyo hivyo hadi sasa. Paulo aliona ni Shetani aliyewindawinda Wakorintho, akijaribu kupandikiza mbegu za uongo kwa kutumia hao mitume wa uongo na kuuondoa utiifu wao kwa Injili ya Kweli na kwa Paulo mtumishi wake.

k.4 Wakristo walikuwa wameanza kuteleza, kwa sababu Paulo asingalipata shida kama bado wangali waaminifu kwa Mungu. Iwapo mitume wa uongo walisema juu ya Yesu wa Nazareti, si yule Yesu aliyehubiriwa na Paulo, ni "mwingine". Yesu wa kweli ameahidi kuwapumzisha watu, ili wasihangaikehangaike; Yeye huwahesabia haki na kuwapa msamaha na uzima bure.

"roho nyingine" kwa msaada wa Roho Mtakatifu mtu hulia "Aba, Baba". Mtu wa Roho hupenda sana Neno la Mungu na kuifurahia neema ya Mungu na kuzaa matunda kwa kumtii. Kweli Wakorintho walimpokea Roho Mtakatifu walipomwamini Kristo. Ila sasa roho "nyingine" imeingia, roho ya kuhesabu

matendo na kujistahilisha mbele za Mungu. Injili “nyingine” hamna; ikiwa mtu ataongeza au kupunguza lolote haibaki tena kuwa Injili, na yoyote nyingine ni uongo (Gal.I:6-9). K.4: “mnatenda vema kuvumiliana naye” picha ni ya Wakorintho kuwapokea hao mitume wa uongo kwa mikono miwili, ni kama mazoea yao, wamefanya hivyo kwa muda.

k.5 Paulo alihofu sana hayo yote yamekwisha kuwa. Na zaidi ya kuwapokea wale wamempa Paulo kisogo, wakimshambulia na kusema kwamba yeye si mtume halisi, amepungukiwa, na ya kuwa wao humzidi. Kwa njia hiyo walitaka kuitikisa mamlaka yake katika Kanisa la Korintho, kusudi waumini wasimjali wala kumsikiliza. Paulo alisema “sikupungukiwa na chochote” na alisema hayo katika msingi wa kuwaza kazi zake na baraka zilizoandamana nazo. Yeye aliwapita wote wengine katika kuwavuta watu kwa Kristo, hata wale ambao sasa walikuwa wakimwacha.

k.6 Katika kupima walitumia mambo ya nje kama ufundi wa “usemi”. Hata hivyo Paulo alikuwa amefaulu katika kuhubiri ujumbe wa Injili akiutegemea uwezo wa Mungu. Pia katika nyaraka zake ameandika kwa kina sana, akiyagusa mambo makuu ya msingi (Mdo.20:20,27 na Mdo.24:2n.k).

11:7-11 <u>Jibu la Paulo kuhusu kujitegemea</u>

k.7 Walimshtaki kwamba amejinyenyekeza ili Wakorintho watukuzwe, maana yake aliishi kwa kujitegemea bila kudai wamtunze. Alifanya hivyo ili awavute kumpokea Kristo. Walisema kwamba kwa kujinyenyekeza na kwa kuishi kwa shida amepunguza uzuri wa ujumbe wake. Si afadhali angalijiinua na kudai heshima, kwa sababu kwa ujumbe wake hata wao wametukuzwa, wametoka katika hali ya kuwa wenye dhambi na kuwa waumini waliosamehewa dhambi zao na kujaliwa uzima wa milele.

Je! alikuwa amefanyaje? Alitoa ujumbe wa Injili “bila ujira” Lakini Paulo hakuona kwamba Injili imepunguzwa uzuri wake kwa kufanya hivyo. Aliiita “Injili ya Mungu” akihubiri kwa kuiinua sana na kuwakemea vikali wale walioiasi (Mdo.18:6). Ni sawa na Kristo ambaye alijinyenyekeza sana, akawa Mtumishi Ateswaye ili sisi tutukuzwe.

k.8 Alipataje riziki zake? Paulo hakutaja habari za kufanya kazi usiku na mchana kwa kushona mahema. Ila alitaja kwamba Wakristo wa makanisa mengine walimletea vipawa. Huenda ndugu wa Beroya walimlipia nauli (Mdo.17:14-15). Wafilipi walimtumia msaada mara mbili alipokuwa Thesalonike (Flp.1:5; 4:10, 16; 2 Kor.8:2, 3). “Naliwanyang"anya” maana yake, si kwamba waliamriwa kufanya hivyo, ila Paulo alifahamu kwamba baadhi yao walikuwa maskini, hata hivyo, walisikia mzigo juu ya uenezi wa Injili na kumtumia msaada. Ndiyo sababu Paulo alihesabu ni kama kuwanyang"anya, ila, siyo, hasa.

k.9 Wakati fulani, pale Korintho, alipungukiwa sana, lakini hakutaka kuwalemea Wakorintho, alitaka kuendelea na kanuni hiyo ya kutokuwalemea.

k.10 Kwa nini? ni kama amejifunga na kiapo, na ataendelea kuhubiri Injili pale bila ujira, potelea mbali mitume wa uongo waseme nini. Aliona kwamba kule kumshambulia huonyesha kwamba injili yao siyo ya kweli. Injili ya Paulo ni Injili ya neema, haina gharama, kwa hiyo hatawadai chochote.

k.11 Kwa nini aseme kwa lugha hiyo? Je! ameshikwa na uchungu? au Je! ni kwa sababu hakuwapenda? La! hata kidogo, kwa kuwa aliwapenda sana sana akamwita Mungu awe shahidi wa upendo alio nao moyoni mwake.

11:12-15 <u>Hali halisi ya wapinzani wake</u>

k.12 Paulo alikuwa na kusudi maalumu alipokaza juu ya jinsi alivyoihubiri Injili bila ujira. Alitaka kuonyesha wazi kwamba Injili haifanani na falsafa za ulimwengu huu. (Wanafalsafa walitoza ada kwa mafundisho yao). Inaonekana hao mitume wa uongo walifanana na wanafalsafa hao na kuhesabu Ukristo ni kama elimu fulani. Walitaka “ujira” kama “ada” kwa kutoa hiyo elimu. Lakini Injili si elimu au hekima yenye asili katika dunia hiyo, bali ni habari za Matendo Makuu ya Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Wito ni kumwamini Kristo na kukabidhi maisha kwake. Paulo alikuwa akiwaita wajitoe kama yeye alivyojitoa, wavute watu kwa Kristo, badala ya kumlaumu Paulo na njia zake. Walimshambulia Paulo kwa sababu walitaka ujira, wakashindwa kwa vile Paulo alikataa ujira kwa Wakorintho. Katika neno hilo waonekana kama mitume wa uongo.

k.13 “watendao kwa hila” hawakutumwa na Kristo (Yer.14:14).

k.14 Wamejifunza hila kwa nani? kwa Shetani. Katika k.3 Paulo aligusa mambo yaliyotokea Bustani ya Adeni, wakati Nyoka, yaani Shetani, alipomdanganya Hawa, akitumia hila na kusema uongo. Paulo aliona ni hali hiyo iliyopo Korintho, Shetani akiwatumia mitume wa uongo ili awadanganye Wakristo na kuuondoa utiifu wao kwa Paulo na Injili ya kweli.

k.15 Shetani alipomjia Hawa alionekana kama malaika wa nuru, aletaye habari njema, kumbe sivyo. Ndivyo ilivyo kwa mitume wa uongo waliofika Korintho, walidai kuwa “watumishi wa haki”. Paulo alijua wakati utafika wa mambo yote kuwa wazi ndipo watapatwa na hukumu waliyostahili.

11:16-33 <u>Paulo: sifa zake na taabu zake nyingi</u>

k.16 Paulo alikuwa amewaomba wauvumilie upumbavu wake wa kujisifu. Lakini, iwapo anaonekana mpumbavu, sivyo alivyo hasa. Hafanyi katika hali ya ki-jinga kwa kupita jinsi kweli ilivyo. Ni kama amejivuna, lakini ni majivuno juu ya mambo ya kweli na ya maana, vema wayasikilize na kuyajali.

k.17 Alikubali kwamba katika kujisifu hafuati kielelezo cha Bwana Yesu, na si kawaida yake kuitumia njia hiyo, na hata alipokuwa akiandika hayo alifanya kwa kusita-sita. Kama ni hivyo mbona aliendelea ? Ni kwa sababu alifikiri, kutokana na mazingara ya Korintho na hali zilizopo, ni njia itakayofaulu ya kuwafanya wazingatie sana mambo yanayotokea kati yao. Aliposema “si agizo la Bwana Yesu” ana maana kwamba njia ya kujisifu si njia ambayo Bwana Yesu angalitumia, siyo kusema anayosema si ya Bwana.

k.18 Tabia ya wanadamu ni kupenda kujisifu, ni maelekeo ya kimwili, pia hatupendi kusikia majivuno ya wengine. Wakorintho walikuwa wamesikia majivuno mengi, ila bado hawajikinai, kwa hiyo, hata Paulo akijivuna watafurahi kuyasikia majivuno yake, kwa hiyo, eti, ajaribu, labda atawapata.

k.19 “mnachukuliana na wajinga kwa furaha” ajabu ni kwamba Wakorintho waliwafurahia hao wajinga, yaani wale waliojivuna Hawakutambua ni ujinga, walijiona ni “akili” kufanya hivyo.

k.20 Paulo alitoboa wazi matokeo ya wao kuwapokea hao mitume wa uongo. Kwanza “wametiwa utumwani” kinyume cha Injili inayowaweka watu huru. “injili nyingine” ya mitume wa uongo ndiyo ya utumwani, nao wamewaruhusu hao watu kuwatia utumwani, tena wamefurahi!!

“wamewameza” wameondoa uhuru wao wa kiroho, wamewatoza ada, wamewalemea kwa posho, nao waumini wamekubali iwe hivyo!! “wamewateka nyara” wamejifanya kuwa mabwana juu ya imani yao na waumini hawana neno!!

“wamejikuza juu yao” wamedai kuwa wakuu wao, wamewalaumu na kuwadharau. Nao waliona ni sawa. Tofauti na Paulo aliyekuwa mpole kwao. “wamewapiga usoni” waliwaambia kwamba Paulo aliwadanganya, na ya kuwa Injili ya Paulo si sawa, ina upungufu; ni kama kuwapiga usoni. Ajabu ni kwamba wamekubali hata waliona wameheshimiwa kuambiwa hayo.

k.21 Ni picha ya aibu machoni mwa Paulo. Lakini ni akina nani walio na aibu? Kama hayo yametokea ni kama maelezo ya yeye na watumishi wake. Ila Wakorintho wakiyazingatia hayo yote ni wao ambao watasikia aibu kwa kutambua ya kuwa walikubali kudanganywa kiasi hicho, tena kwa urahisi. Amekwisha kuweka msingi tayari, amewaonya kwamba ana mashaka ya kuwa wamekosa unyofu wa moyo na uaminifu kwa Kristo. Katika kuwakaribisha mitume wa uongo wameondoka katika msimamo wao. Bila shida yoyote hao mitume wa uongo wamefaulu kuharibu sifa na kazi za Paulo, wakitumia njia ya kujisifu.

Wakorintho wamependa wenye kujisifu iwapo kwa njia hiyo wao wenyewe wametekwa nyara na kutiwa utumwani kwa upande wa kiroho. Hivyo Paulo aliwaza kwamba hata na yeye atumie njia hiyo; huenda na yeye atafaulu kuukamata usikivu wao, hata hivyo hatazidi mpaka. Atatoa habari za kweli tu ambazo ni dhahiri. Wapinzani wake wamedai makubwa na kazi za Paulo zimeonekana hafifu kwa vile zilipinduliwa haraka.

k.22 Mitume wa uongo walijivuna katika mambo matatu: kuwa Waebrania, kuwa Waisraeli, na kuwa wazao wa Ibrahimu. Paulo alijibu kwa kuonyesha kwamba hata na yeye pia ni Mwebrania, na Mwisraeli, na mzao wa Ibrahimu, tena kwa kuwazidi.Alizidi kwa upande wa kuzaliwa, kwa desturi na mila, kwa lugha, na kwa hali zote (Flp.3:5 Rum.9:6, Gal.3:7).

Kuvunjikiwa meli baharini

k.23 Walidai kuwa wahudumu wa Kristo. Paulo aliwazidi, alikuwa “mtumwa” wa Kristo aliyeyashika maagizo yote ya Kristo, hakufuata mapenzi yake katika jambo lo lote. Katika kazi za kumtumikia Kristo alifanya kwa bidii sana, alipatwa na shida na taabu, alikubali kufungwa na kupigwa, ingawa hakustahili hayo kwa sababu hakukosa sheria. Je! hao mitume wa uongo wamekubali kufungwa au kupigwa kwa ajili ya kuihubiri Injili? La! hata kidogo! Mara nyingi Paulo alikuwa katika hatari ya kufa na kuuawa. Je! hao wamepatwa na shida za namna hiyo mara ngapi? Paulo alipigwa bakora mara 5, mapigo 39,

walipunguza moja katika hesabu ya 40 ili wasipite 40, (waliwekea akiba ya 1 wakikosea hesabu wakati wa kupiga (Kum.25:3). Mapigo hayo yalikuwa makali na wengine walikufa kabla ya kufikia pigo la mwisho. Pia katika safari za kuvuka baharini alikuwa hatarini mara nyingi.

k.26 Orodha ya hatari mbalimbali ni thibitisho la ukweli wa kujitoa kwake katika kuhubiri Injili, ni kama aliishi kwa kupumua "hewa" ya hatari. Hata hivyo hakukata tamaa wala kuzipunguza bidii zake au kuubadili mwenendo wake.

k.27 Alieleza hali ya kazi kwa maneno "taabu" "masumbufu" "kuchoka", hakuwaza apate pumziko, hakutafuta siku ya "off", alikosa riziki, alikosa usingizi, alikosa starehe, alikosa raha. Licha ya hayo, alikesha na kufunga mara nyingi, alikubali hata kukosa nguo za kuvaa, akawa uchi na kusikia baridi. Je! hao mitume wa uongo wamekubali, ingalau kwa sehemu tu, taabu zozote kwa ajili ya Injili?

k.28 Kama hayo ya kimwili hayakutosha lilikuwapo jambo moja lililo zito zaidi, nalo ni "maangalizi ya makanisa" yaani mzigo wa kuwashughulikia Wakristo katika shirika zao. Mzigo wa kuwaelekeza vema katika maisha ya Kikristo, na kuwaonya na kuwarekebisha wakiteleza. Katika maangalizi hayo ilimbidi aende kuwaona, hasa akisikia habari za shida fulani; au pengine kuwaandikia barua, na zaidi ya yote kuwakumbuka, tena kwa majina, katika maombi yake. Kazi hiyo ilikuwa ya kila siku.

Hao mitume wa uongo wamefanya nini katika kuwahudumia watu? Walionyesha mzigo gani katika kuongoza watu kuwa waaminifu kwa Kristo? Bila shaka jibu ni, hawakufanya lolote.

k.29 Kwa kulingana na hayo yote Paulo alijiona kuwa dhaifu na mtu wa kupatwa na maumivu na mashambulizi mengi. Na wote waliojisikia kuwa dhaifu na wamekwazwa walijua kwamba Paulo naye alishiriki nao katika taabu zao.

k.30-33 Paulo amefuata mitume wa uongo katika neno la kujisifu, ila kujisifu kwake kumehusu taabu na dhiki na udhaifu wake. Alipojilinganisha na wapinzani wake, akaona ya kuwa amewazidi. Kweli hao hawakuonyesha dalili yoyote ya "udhaifu" hawakutambua upungufu wowote, wao ni wazuri, wao ni bora! Lakini kudai hivyo si thibitisho la "ubora" wao, maana walijifanya, na kuwadanganya watu tu. Katika 4:7 Paulo aliandika kwamba tunayo hazina ya Injili katika vyombo vya udongo, ubora ni ile hazina si vyombo, ili uwezo wa Mungu hudhihirika, ni kama Paulo alisema kwamba wahudumu wa kweli wa Bwana watakuwa "dhaifu".

k.30 Kama ni lazima ajisifu, ataacha mengine yote na kusema juu ya udhaifu wake. Ufalme wa Kristo ni kinyume cha falme za dunia zinazotegemea nguvu na uwezo na mbinu za kibinadamu n.k.(Mt.20:26-28).

k.31 Alimtaja Mungu na kusema kwamba hata Mungu alijua ya kuwa alikuwa akisema kweli.

k.32 Mfalme Aeta alitawala kama K.K.9 - B.K.40, alikuwa baba wa mke wa kwanza wa Herode Antipa. Kwa nini amemtaja huyo? Ni kwa sababu alitaka kuonyesha kwamba alipookolewa mikononi mwake hakupona ki-ajabu, bali kwa njia “dhaifu” maana alishushwa katika kapu bila watu kuwa na habari. Iwapo alikuwa “mwongofu” maarufu, Mungu hakumwokoa kwa mwujiza wa ajabu.

12:1-10 <u>Maono matukufu na mwiba mwilini</u>

k.1 Tumekwisha kuona ya kwamba Paulo alilazimika kujisifu kama itikio kwa kujisifu kubaya kwa mitume wa uongo, waliokuwa na shabaha ya kujiinua mbele za Wakorintho. Kujisifu kwao hakukuwa katika msingi wa kweli, wala juu ya mambo ya maana. Tena walilenga kumdharau Paulo ili aonekane kama mtu duni asiyefaa kuwa mtume.

Hivyo Paulo alijisifu, lakini tofauti na wale, alijisifu katika mambo ya kweli, ya maana, tena kwa kuukubali udhaifu wake. Katika kuukubali udhaifu wake uwezo wa Mungu wa kukitumia chombo dhaifu ulidhihirika, kwa sababu matokeo ya ajabu yalitokea, Injili ilienezwa mahali pengi na makanisa yalipandwa hata katika miji mikubwa kama Korintho.

Katika sehemu hiyo ametaja neno la maono aliyoyapata, jambo ambalo si la kawaida. Maono hayo yalimtia moyo lakini pamoja nayo alipewa “mwiba” katika mwili wake, ili asipate kujivuna kuliko ilivyompasa.

Paulo aliitwa na Mungu kufanya huduma ngumu sana, ni kama Mungu alimwita kuwa kielelezo chema kwa wote watakaofuata kuwa wahudumu. Kwa hiyo, Mungu alimjalia kuona mambo ya ajabu kuhusu utukufu wa Mungu Mwenyewe, kusudi atiwe moyo wa kuvumilia taabu na dhiki zote atakazozipata.

k.2 Hapo Paulo alijieleza kwa kutumia lugha “namjua mtu mmoja katika Kristo”. “Namjua” ni lugha ya binafsi, aliyezungumziwa ni yeye mwenyewe. Tena ametaja miaka 14 iliyopita kuwa wakati wa jambo hilo kutokea, kama B.K.42 baada ya kuokolewa kwake na baada ya kuondoka Dameski salama. Bila shaka ni kabla ya kutafutwa na Barnaba na kuletwa Antiokia kwa kazi (Mdo.11:25-26).

Hakujua kama mwili wake mwenyewe ulipandishwa mpaka mbinguni au sivyo, ila kwa ghafula na haraka alijikuta yuko katika “mbingu ya tatu” yaani Peponi/Paradiso. (huenda mbingu ya 1 na ya 2 ni eneo la nyota n.k.) Kusema “ya tatu” huenda ni kuonyesha ubora wake. Ni kwa neema ya Mungu alipatwa na hayo, si kwa kustahili kwake.

k.3 Alikuwa na uhakika juu ya tukio hilo, akitambua ni Mungu tu ajuaye ukweli wote juu ya tukio hilo.

k.4 Alipokuwa huko juu alisikia mambo ya ajabu yasiyoweza kujulikana na mwanadamu, wala kuelezwa na mwanadamu, ni kama mambo ya siri yasiyowahusu wanadamu. Iwapo hasemi ni nini hasa aliyoyasikia ni dhahiri yaliuhusu utukufu wa Mungu.

k.5 Aliona kwamba kujisifu kuhusu jambo hilo ni sawa kwa sababu lilimhusu Mungu na utukufu wake, hata hivyo, yeye mwenyewe atajisifu juu ya udhaifu wake tu.

k.6-10 „Mwiba" katika mwili na Neema ya Mungu kutosha
Kutokana na maono hayo aliyojaliwa kupata ingekuwa rahisi kwa Paulo kuwa na kiburi cha kiroho. Mungu alimnyenyekeza na kuruhusu awe na „mwiba" mwilini mwake ili wakati wote akumbushwe udhaifu wake kusudi azidi kumtegemea Mungu. „mwiba" umeelezwa kuwa "mjumbe wa Shetani ili anipige". Neno "mwiba" linaonyesha kitu chenyewe kilikuwa kikali, tena umetokea kwa sababu ya kazi yake. Shabaha ya kupewa "mwiba huo" ilikuwa "nisije nikajivuna kupita kiasi". Aliupokea "mwiba" huo bila manung'uniko, ila kwa sababu ilimsumbua katika kazi yake ya kuhubiri Injili alimwomba Bwana uondolewe.

k.8 Alimsihi Bwana kwa mara tatu amwondolee huo mwiba. Yawezekana aliweka vipindi vitatu maalumu kumwendea Bwana na kumwomba juu yake. k.9 Bwana alimjibu, si kwa kumwondolea huo mwiba, bali kwa kumhakikishia kwamba atampa neema ya kutosha kuuvumilia. Iwapo atakuwa na maumivu yatakayomsumbua hasa katika kazi yake ngumu, hata hivyo, kwa kumtegemea Bwana atajikuta kwamba atawezeshwa kuendelea na kazi hiyo.

Zaidi ya kuyavumilia hayo maumivu na masumbufu ataufurahia udhaifu wake na kuonja kwa wingi uweza wa Kristo utakaomwezesha. Watu watamwona na hali dhaifu ya mwili wake nao watajua kwa hakika kwamba Bwana yu pamoja naye akimfunika kwa neema yake.

k.10 Kwa hiyo ataufurahia udhaifu wake, na dhiki, na mashutumu anayopata, pamoja na maudhi mbalimbali, dhihaka za mitume wa uongo n.k mradi hayo yote yametokana na kusababishwa na utumishi wa Kristo na Injili yake. Daima alifarijika alipokumbuka maono matukufu ya Mungu aliyojaliwa kupata alipoanza huduma.

Katika habari hiyo twajifunza kwamba twapata neema kwa kutuwezesha kupita salama katika magumu si kwa kuondolewa magumu. Neema ya Mungu hutosha kila hali tuliyo nayo.

12:11-13 Matokeo ya kufika Korintho hapo nyuma

k.11 Kifungu hicho chajumlisha sehemu hiyo yote juu ya kujisifu. Paulo alikiri kwamba amekuwa mpumbavu, ila alilazimika kujisifu kwa jinsi walivyokuwa. Wakorintho walipaswa kumsifu, maana alikuwa mtume halisi na kazi zake zilimthibitisha kabisa kuwa hivyo. Kanisa la Korintho halikupungua makanisa mengine kwa vipawa na kwa miujiza iliyofanyika kati yao n.k. Ila Paulo alikosa heshima machoni pao katika neno moja tu la kutokuwalemea kwa riziki. Katika kujisifu alitaja mambo ya kweli, na hasa mambo ya udhaifu wake, magumu, dhiki, mateso, mashutumu. Pamoja na kutaja maono ya utukufu aliyojaliwa kupata. Wakilinganisha sifa zake na zile za mitume wa uongo watatambua kwamba iko tofauti kubwa kati ya huduma yake na yao, na juu ya hali zake na zao. Ndipo watajua wa kweli ni akina nani, nao watamrudia Paulo na Injili yake. Hawataendelea kuwakubali mitume wa uongo wakizingatia sana hayo yaliyosemwa na Paulo. Alijua kwamba yeye “si kitu” (k.11) pia alifahamu neema ya Mungu yu pamoja naye ikimwendesha, na neno hilo limethibitika katika yote yaliyotokea kati yao tangu alipofika Paulo na kuhubiri Injili kwa mara ya kwanza, hadi kuja kwa mitume wa uongo ambao kazi zao zilikuwa kubomoa siyo kujenga imani zao.

12:14-21 Jinsi atakavyofanya atakapokuja tena

k.14 Kisha Paulo aliacha hayo mazungumzo juu ya kujisifu na kadhalika na kuwaambia juu ya kuwajia tena, ambayo itakuwa mara ya tatu kuwafikia. Hatabadili kawaida yake ya kujitegemea. Kitu anachotafuta si mali au riziki zao, bali ni wao wenyewe. Hapo twaweza kujiuliza; Je! ni lazima watumishi wa Bwana wajitegemee, wasitunzwe na watu? La! hata Paulo mwenyewe hakujitegemea kila mahali alipokwenda. Twajua Wafilipi walimtunza na hata makanisa mengine. Kwa nini alikazana kujitegemea alipokuwa Korintho? Bila shaka hali fulani ilikuwapo au ni tabia fulani ya Wakorintho iliyomwongoza kufanya hivyo. Pengine ni kwa sababu pale Korintho watu waliozoea kuwaza pesa na kuithamini sana na Paulo kwa kielelezo chake alitaka kuyaelekeza mawazo ya Wakristo wasiwe na tabia ya kupenda fedha. Pengine aliwaza ya kuwa watamsemasema kuwa anayo choyo n.k. Katika 11:7 alisema sababu moja ni wao watukuzwe. Kwa njia hii watatambua wokovu ni kipawa kinachotoka kwa neema ya Mungu, nacho ni bure. Hatujui kama zilikuwapo sababu zingine.

k.15 Alishuhudia kwamba alikuwa tayari kuendelea kujitoa kwa ajili ya usalama wa roho zao. Alifurahi kumwaga maisha yake na kujigharimia afya yake, nguvu zake, nafasi zake na upendo wake katika kuwatumikia (Flp.2:17). Ila aliuliza swali gumu kwao; kadiri anavyozidi kuwapenda kwa kiasi hicho Je! wao watazidi kuupunguza upendo wao kwake?

Inaonekana wale mitume wa uongo walikuwa werevu wakiwaambia kwamba iwapo Paulo ameonekana mnyenyekevu na mpole, tena yu tayari

kutokuwalemea, hasa kweli ilivyo, hali hizo zote ni maficho yake ya kujiingiza na kuwapata.

k.17-18 Paulo aliwakumbusha kwamba hata alipomtuma Tito na wale wengine hawakuitwa kuwatunza; watumishi wote waliotumwa kwao waliutegemea uongozi wa Roho na kukifuata kielelezo cha Paulo wa kujitegemea.

Iwapo Tito alikuwa amemletea Paulo habari nzuri ni wazi kwamba mambo hayajawa mazuri. Wamepata nafuu kwa kuyarekebisha mengine. Katika sehemu hiyo Paulo alikuwa akiwaandaa kwa kufika kwake. Alitaka waendelee kuyatengeneza mengine yaliyobaki ili yeye asihuzunishwe na wao wasiaibishwe. Twajua kwamba hata kabla ya kufika kwa mitume wa uongo walikuwa na matatizo mbalimbali. Katika Waraka wa kwanza ilimbidi Paulo aseme sana juu ya mafarakano, uasherati, Chakula cha Bwana, na mengineyo. Kufika kwa mitume wa uongo kulizidisha shida zao na zaidi kulisababisha ufa utokee katika uhusiano wao na Paulo kwa sababu ya hila ya mitume wa uongo ya kutia mashaka juu ya nia na sababu za Paulo.

k.19 Baadhi ya Wakorintho waliwaza kwamba Paulo alipotoa maelezo ya Utume wake alikuwa akijitetea kama mtu aliyeshtakiwa barazani. Lakini haikuwa hivyo. Paulo hakukubali ya kuwa Wakorintho ni mahakimu wa kuuhukumu Utume wake. Paulo alifahamu kwamba hapo nyuma walijiweka kuwa waamuzi wa watumishi waliposema “mimi ni wa Apolo” n.k.(1 Kor.1:12). Tena katika kuwasikiliza mitume wa uongo wamekuwa waamuzi.

Lakini alijitetea kwa shabaha na maana nyingine. (2:14-17)
Hata alipoueleza utume wake kwa njia ya majivuno ya ki-jinga lengo lake lilikuwa kuidhihirisha Injili ya Kristo na uwezo wake wa kumwezesha mtu dhaifu kama yeye. Wakati wote alikuwa na shabaha ya kuwajenga kiroho.

k.20 Paulo alihofu kwamba atakapofika atawakuta bado wangali wakiendelea katika dhambi mbalimbali. Kweli atasikitika sana sana ikiwa itambidi kuwa mkali. Si afadhali wayatengeneze mambo mapema kabla hajafika, ndipo atakapofika watashirikiana pamoja kwa furaha na amani. Wasipokuwa tayari kufanya hivyo basi wao wataumia na yeye pia ataumia. Neno kuu ni wao watubu dhambi zao.

13:1-10 Mpango atakaofuata

k.1-2 Kwanza aliwahakikishia uhakika wa kuja kwake. Bila shaka wengine walidhani kwamba hawezi kuja kwa sababu ya kukumbuka ilivyompata alipofika mara ya pili.

Kuhusu mambo yenyewe, kwanza atalichunguza kila neno na kuuthibitisha ukweli wake, ndipo ataamua la kufanya. Ni wazi kwamba hatawahurumia wale

ambao wamefanya dhambi na wamekataa kutubu. Aliwaonya kwamba atakapofika atafanya sawa na alivyowaandikia. Hatafanya upendeleo wa kuwaachilia wengine.

k.3-6 Kwa nini hatawahurumia wale ambao atawakuta bado wangali wanaendelea katika dhambi? Ili, waone dalili ya Kristo ndani yake. Kurudi watu ni sehemu mojawapo ya maisha ya Kikristo na ya maisha ya shariki zima la Wakristo wanapoishi pamoja mahali pao. Walikuwa wakitafuta dalili ya Kristo kuwa ndani yake, basi, kwa njia ya kuwarudi wataiona, ataitumia mamlaka ya KiMitume aliyopewa na Kristo kwa kuongoza watu wake. Inaonekana baadhi walisita-sita katika kujirekebisha, wakisema kwamba, kweli katika barua Paulo asema kwa nguvu na ukali, lakini atakapofika hatakuwa na nguvu na ukali ya kufanya lo lote la kuwarudi watu.

Wakorintho walikuwa na dalili nyingi za Kristo kuwa ndani ya Paulo. Imekuwaje liko sharika la Wakristo pale Korintho? ilikuwaje waliyapokea mahubiri hafifu ya Paulo, mhubiri mnyonge? Jibu ni Kristo alikuwa pamoja naye na kufanya kazi kwa uwezo!! Ni kama Wakorintho bado hawajafahamu vizuri namna ya uwezo wa Kristo na kanuni za kufanya kazi yake. Wamesahau kwamba Kristo Mwenyewe alisulubiwa katika udhaifu, hata hivyo, anaishi kwa nguvu ya Mungu iliyomfufua katika wafu. Kwa nini alisulubiwa? Ni kwa sabbu alikubali kuwa dhaifu, kwa hiari alijidhili hata mpaka kufa msalabani kama mhalifu wa hali ya juu, alikuwa kama kondoo aliyeletwa machinjoni, hali amenyamaza. Je! ni kweli alikuwa dhaifu? Je! ni kweli alipata hasara? Matokeo makubwa yalisababishwa na Kujidhili Kwake: ulimwengu ulikombolewa na watu walipatanishwa na Mungu. Dhambi, mauti, na Shetani vilishindwa.

Sasa Kristo yu hai, amepewa mamlaka yote, yu mkono wa kuume wa Mungu, akiongoza mambo yote. Je! kama ni hivyo, mbona Wakorintho wanauliza maswali juu ya wahudumu wanaowajia kwa unyenyekevu na katika hali za udhaifu mbalimbali. Wao wameungana na Kristo “katika udhaifu”. Wale ambao hawatambui neno hilo wamepungua katika ufahamu wao wa huduma ya Kikristo (1 Kor.2:1-5). Wamechanganya mambo ya kiroho na mambo ya ki- dunia.

k.5 Paulo aliwaita wazipime hali zao na kujihakikishia kwamba imani yao ni kweli ili wawe na uhakika wa Kristo kuwa ndani yao.

k.6 Vilevile kwa kufanya hivyo watajua ya kuwa hata Paulo na wenzake wamekubalika na Mungu.

k.7-10 Hapo Paulo alikaza kwamba imewapasa kuishi maisha yanayotakiwa na kuacha neno lolote baya. Paulo hakutaka wamtangaze yeye na wenzake kuwa wazuri ila neno kubwa ni mwenendo wao uwe safi bila lawama. Alitaka wajisimamie katika imani na maisha yao, bila kuambiwa la kufanya kila wakati

na Paulo. Si kitu kama wao wataona hana dalili ya Kristo, mradi wao wenyewe waishi kama iwapasavyo.

k.8 Pengine hapo Paulo aliwaza mitume wa uongo waliofanya kwa hila katika Kanisa la Korintho. Walikuja Korintho na kukuta Kanisa linalositawi, ambalo wao hawakulianzisha. Walijipatia sifa kama mitume wakuu, ndipo wakafanyaje? Baada ya kuingiza miguu, wakamhukumu Paulo, na kudharau kazi zake, na Injili yake. Wakaiharibu kazi yake iliyokuwa imechukua muda wa kuisimamia, tena kwa kuzivumilia taabu nyingi. Ukuu wao ulionekana katika kubomoa!! Paulo hakuweza kukifuata kielelezo chao. Paulo alihesabu kazi ya kubomoa ni kazi ya Shetani. Kwa upande wake Paulo atayashughulikia mambo ya kuwajenga kiroho.

k.9 Paulo hakuona shida ya kuonekana kuwa mtu dhaifu, wala hakusikia shida kwa Wakorintho kuonekana hodari, mradi tu, waishi kwa kweli ya Injili Bado angali aliwatumaini kwamba shida zao zitatengenezwa, maana aliomba watimilike.

k.10 Paulo alitamani sana ya kuwa watayatengeneza makosa yao na kuimarika ili atakapowafikia asiwe na haja ya kutumia uwezo ule aliopewa na Bwana ya kuwakemea na kuwarudi kwa ukali. Hasa alitaka awe na nafasi nzuri za kuwajenga katika imani yao. Hata ikimbidi awarudi atafanya kwa shabaha ya kuwajenga kiroho. Huenda marudi yenyewe yatakuwa ya kuwatenga na sharika, wasishirikiane na wenzao, ili wajifunze nje ya sharika jinsi ilivyo baraka kubwa kuwa ndani ya shariki.

13:11-14 <u>Maneno ya kuagana nao</u>

Aliwaita “ndugu” iwapo wamemhuzunisha na hali zao hata hivyo aliendelea kuwawaza kuwa ndugu zake katika Kristo. Aliwasihi watimilike, yaani wakue kiroho, tena wapate faraja ipatikanayo kwa Mungu, wasizidi kuyasikitikia yaliyopita, tena wanie mamoja, wawe na amani kati yao. Bila shaka ilikuwapo hatari ya wale ambao hawakukosa kuwalaumu wenzao walioanguka. Wahesabu yaliyopita kuwa kweli yamepita, wajifunze kwayo, ndipo waanze kwa upya kwa neema na uweza wa Kristo. Ahadi ipo ya Mungu kuwa pamoja nao, na Mungu huyo ni Mungu wa upendo na amani, si Mungu anayekumbuka makosa.

k.12 Ushirika wa Kikristo ni kitu cha maana, nao kwa tendo la nje la kutumia busu takatifu washuhudia uzuri wake. Yawezekana baadhi yao wameacha desturi hiyo wakati wa matatizo. Paulo alitaka waendelee na tendo hilo.

k.13 Paulo aliwaletea salaam za Wakristo wenzao wa mahali pengine ili wasisahau kwamba wako waumini mahali pengi. Bila shaka wengine walikuwa

wakiwakumbuka na kuwaombea hasa walipojua kwamba walikuwa na matatizo mbalimbali.

k.14 Tumezoea kuyatumia maneno hayo katika mikutano na ibada zetu. Ni ushuhuda wa Utatu wa Mungu. Kristo ametajwa kwanza kwa sababu ya neema yake iliyosababisha kuokolewa kwetu. Asili ya huo wokovu ni katika Pendo la Mungu aliyemtuma Mwana wake kuishi na kufa kwa ajili yetu.Tumepewa Roho Mtakatifu ili tupate kushirikishwa yote yaliyomo katika Ukombozi uliofanyika na Kristo. Pia waumini waungamanishwe na Kristo, pia wao kwa wao, kusudi Roho afanikiwe kufanya kazi ndani ya Kanisa, ili mapenzi ya Mungu yatimizwe

MASWALI

Sura za 10 - 13 Kuna tofauti gani katika hali ya sura hizo za mwisho na zile zilizotangulia?

10: 1-11 Paulo alitaka Wakorintho wajiandaa kwa njia gani tayari kwa kuja kwake? Adui zake walisema nini juu ya Paulo, na walikuwa na shabaha gani? Kwa nini walimlaumu Paulo kwa kuwa alijitegemea kwa riziki alipokuwa Korintho?

10:12-11:33 Kwa nini Paulo alikubali kujisifu? Alijisifu juu ya mambo gani? Adui zake walijisifu juu ya nini? Je! sifa zao zilikuwa za kweli?

12:1-12 Kwa nini Paulo alijaliwa kuyapata maono? Pamoja na maono alipewa nini? na kwa sababu gani? Mungu alimwahidi nini?

13:1-14 Atafanya nini atakapofika kwao? Wawahi kufanya nini?
Waonaje? Katika Kanisa la leo ni vizuri Kanisa liwe na marudi kwa wale wanaoendelea katika kosa baada ya kushauriwa? Eleza.
Marudi yawe na shabaha gani na kufuata kanuni gani? Eleza.

KUHUSU KITABU KIZIMA: Andika insha ya kuonyesha umejifunza nini kuhusu utumishi wa kumtumikia Kristo. Manufaa ya Kitabu hicho kigumu ni nini?